

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Thelathini na Tisa – Tarehe 30 Mei, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Kumi na Tano, leo ni Kikao cha Thelathini na Tisa. Katibu.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI - K.n.y. WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Taarifa ya Mwaka ya Hesabu za Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kwa mwaka 2017/2018 (*The Annual Report and Audited Accounts of The Arusha International Conference Center for the Year 2017/2018*).

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

MHE. FATMA H. TOUFIQ - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Taarifa ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza litaelekea TAMISEMI na litaulizwa na Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga, Mbunge wa Ulanga, tafadhali.

Na. 324

Ukarabati wa Majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Ulanga

MHE. GOODLUCK A. MLINGA aliuliza:-

Majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Ulanga ni machache, madogo na machakavu hasa yale ya kulaza wagonjwa:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo na ujenzi wa majengo mapya?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Goodluck Mlinga, Mbunge wa Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kutekeleza mpango wa kuikarabati na kuipanua Hospitali ya Wilaya ya Ulanga ambapo mwezi Mei, 2019, Serikali imepeleka kiasi cha shilingi milioni 400 katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ulanga. Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri imetenga shilingi milioni 60 kupitia mapato yake ya ndani kwa ajili ya kukarabati Hospitali ya Wilaya hiyo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Goodluck.

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kwa niaba ya wananchi wa Ulanga, naomba niishukuru Serikali ya CCM kwa kutupa kipaumbele kwenye Sekta ya Afya. Maana yake tumepeata shilingi milioni 400, Kituo cha Afya cha Lupilo kimeisha na shilingi milioni 400 imeingia juzi.

(a) Hospitali hii ya Wilaya wakati inajengwa, mwaka 1905 wilaya ilikuwa na watu 23,000, leo hii wilaya ina watu zaidi ya 200,000: Serikali haionti kiasi hiki cha fedha, shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa hospitali hii ni kidogo sana?

(b) Hospitali yetu ya Wilaya ya Ulanga imekuwa na changamoto kubwa sana ya watumishi wachache na wasio na sifa: Je, lini Serikali italeta watumishi wa kutosha na wenye sifa?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza tunapokea pongezi za Serikali kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge na kwa niaba ya wananchi wa Ulanga. Mheshimiwa Mbunge ana maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, tumepeleka shilingi milioni 400, anadhani kwamba ni pesa kidogo.

Naomba tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni awamu ya kwanza, tunapeleka fedha katika maeneo mbalimbali ya nchi hii kama alivyosema kwa kuzingatia kipaumbele cha afya. Baada ya awamu hii kwisha tutaangalia pia kutokana na uwezo wa Serikali tutaongeza fedha nyagine. Lengo ni kuimarisha hospitali hii iweze kutoa huduma inayostahiki na hata kadri ambavyo wananchi wapya wataendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili Mheshimiwa Mlinga anauliza habari ya watumishi. Muda uliopita Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Kandege, alitoa taarifa kwenye Bunge hili Tukufu kwamba tumeshapeleka barua kuomba kupata kibali cha kuajiri watumishi kwa upande wa Sekta za Elimu na Afya. Kwa hiyo, wakati wowote tukipata kibali hicho, tutakapoajiri tutazingatia maombi ya Mheshimiwa Mbunge lakini pia na maeneo mengine ya nchi hii. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Ishengoma na Mheshimiwa Mnyika.

MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Hospitali yetu ya Ulanga ina tatizo na tatizo ni kuwa haina gari la wagonjwa: Je, Serikali ni lini itatupatia gari la wagonjwa kwenye Hospitali yetu ya Ulanga?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. Hospitali ya Ulanga haina gari la wagonjwa.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli kwamba kuna maeneo mengi ambayo bado tuna upungufu wa vitendea kazi. Tunaomba tulipokee swali hili. Kadri tutakavyopata uwezo tutapeleka gari katika eneo hili pamoja na maeneo mengine ya nchi ambayo kwa kweli kuna changamoto ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa tumeelekeza kwamba katika maeneo ya jirani au kwenye Hospitali ya Wilaya ya jirani inapotokea shida au hata magari ya Halmashauri yatumike kutoa huduma hiyo. Tutajitahidi kadri itakavyowezekana magari yapatikane katika Hospitali ya Wilaya, ikitokea shida ya mgonjwa basi apate huduma haraka kupelekwa kwa hatua nyingine ya mbele.

SPIKA: Mheshimiwa Mnyika nilishakutaja. Swali la nyongeza.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Majimbo ya Kibamba na Ubungo kabla haya jaondolewa kwenye Manispaa ya Kinondoni yalikuwa yanahudumiwa na Hospitali ya Mwananyamala. Sasa baada ya kuanzishwa kwa Wilaya mpya ya Ubungo, huduma tunazipata kwenye Hospitali ya Sinza Palestina ambayo hailingani na wingi wa watu wa Majimbo haya mawili ya Kibamba na Ubungo na haina eneo kubwa kwa ajili ya kuipanua kuwa hospitali kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa je, Serikali iko tayari sasa kwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Ubungo yako ndani ya Jimbo la Kibamba eneo la Kwembe na kuna ardhi kubwa imepimwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa *satellite town* Luguruni: Je, Serikali iko tayari sasa kwenda kujenga hospitali ya wilaya kule ili wananchi wa maeneo ya kule wapate huduma ya eneo la karibu zaidi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anazungumza, lakini katika Mkoa wa Dar es Salaam tumepeleka fedha kuimarisha kituo pale Kinondoni, tumepeleka fedha shilingi milioni 200 pale Sinza, tumepeleka fedha Kigamboni shilingi milioni 1.5 kwa awamu ya kwanza na pale llala na tumeongeza shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, naomba tupokee ombi hili. Ukweli ni kwamba kila palipo na Makao Makuu ya Wilaya patakuwa na huduma ya wananchi. Awamu hii ikimalizika tutapeleka fedha katika eneo hilo ili wananchi wetu waweze kupata huduma. (*Makof!*)

SPIKA: Ahsante sana. Tunahamia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, swali la Mheshimiwa Ruth Hiyob Mollel, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi.

Na. 325

Kupanga Matumizi ya Ardhi Nchini

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI (K.n.y. MHE. RUTH H. MOLLEL) aliuliza:-

Migogoro ya wakulima na wafugaji imekuwa tatizo sugu katika maeneo mengi nchini pamoja na kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali:-

(a) Je, Serikali imetenga kiasi gani cha bajeti kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi nchi nzima?

(b) Kijiji cha Matenzi Kata ya Beta Wilayani Mkuranga kina wafugaji takribani 10,000: Je, Serikali ina mkakati gani wa kupima eneo hilo kabla migogoro haijaanza?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA
MAKAZI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Ruth Mollel, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kwa mujibu wa Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007, ni jukumu la mamlaka ya upangaji ambazo ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi kwa ngazi ya Taifa na Halmashauri za Wilaya na Vijiji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitenga fedha za kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi kila mwaka. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 hadi 2019/2020 Serikali imetenga shilingi bilioni saba za matumizi ya kawaida na maendeleo kwa ajili ya kupanga matumizi ya ardhi na kutatua migogoro ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2018/2019 Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, iliendelea kuwezesha upangaji wa matumizi ya ardhi katika vijiji vyote vinavyozungukwa na hifadhi za misitu na hifadhi za Taifa. Kazi hii itaendelea katika mwaka wa fedha 2019/2020 ikijumuisha upangaji wa matumizi ya ardhi katika vijiji vyote vinavyopitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta pamoja na wilaya zote mpakani mwa nchi jirani. Aidha, wadau mbalimbali wa maendeleo wamekuwa wakiwezesha mamlaka za upangaji kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uandaaji wa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya mwaka 2007, kifungu cha 33(1) kinatoa mamlaka kwa Halmashauri za vijiji kujandalia mipango ya matumizi ya ardhi. Vilevile, vifungu vya 9(1) na 21(2)(b) vya Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 ya mwaka 1999 na miongozo ya kuandaa mipango ya vijiji wa mwaka 2013

vinatoa mamlaka kwa Halamshauri za Wilaya kujengea vijiji vyake uwezo na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi pamoa na kuratibu kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi imeshajengea uwezo na kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga. Hivyo, ni jukumu la Halmashauri hiyo kuendeleza kazi ya kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji vyake kwa kutoa kipaumbele kwenye vijiji vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi na tishio kwa hifadhi ya ardhi na mazingira, hususan hicho Kijiji ambacho Mheshimiwa amekitaja cha Beta ambacho anasema kina mifugo zaidi ya 10,000.

SPIKA: Mheshimiwa Dkt. Sware nilikuona.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa niaba ya Mheshimiwa Ruth Mollel, bado ana maswali amwili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ni moja na Serikali Kuu alikasimu baadhi ya madaraka yake katika Serikali za Mitaa, basi Serikali Kuu haina budi kusimamia na kuratibu shughuli mbalimbali za Serikali za Mitaa. Serikali haioni ni vyema sasa kusimamia na kutoa maelekezo mahususi katika Serikali za Mitaa katika kujikita kupanga ili tujue kwamba matumizi ya ardhi ni nani anatumia nini kwa ajili ya shughuli za kiuchumi?

Mheshimiwa Spika, vilevile kwa kuwa Serikali Kuu imechukua vyanzo vikuu vya mapato katika Serikali za Mitaa, Serikali Kuu haioni sasa ni muhimu ku-*ring fence* fedha fulani kwa ajili ya shughuli mahususi za kuratibu shughuli za upangaji wa matumizi ya ardhi? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Lukuvi, tafadhalii.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Spika, kwanza ni kweli Wizara ya Ardhi ina wajibu ya kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Ardhi Na. 5 na utekelezaji wa Sheria ya Mipango Miji zote zinahusiana na mambo ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa tunafanya hivyo, tunatoa mwongozo wa kusimamia na kupitia wataalam wetu waliopo kila Halmashauri wanashiriki, kwa sababu kazi hii inasimamiwa na wataalam wa Sekta ya Ardhi ambao wako katika kila wilaya. Ndiyo maana imeweza leo hii Wilaya hiyo ya Mkuranga anayoiulizia swalii, Mheshimiwa Ulega, Mbunge wa Jimbo la Mkuranga, ni shahidi, vijiji 21 tayari vimeshafanyiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafunzo ambayo Wizara tumeyatoa na uwezeshaji tuliofanya katika Wilaya ya Mkuranga, wale viongozi, Madiwani pamoja na watendahi wa Sekta ya Ardhi wa Mkuranga wameweza kujiongeza wenyewe kutekeleza wajibu wao na kwenda kufanya sasa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 21. Kwa hiyo, kazi hiyo ndiyo tunayofanya.

Mheshimiwa Spika, la pili ni fedha. Sisi kama Wizara, hata kwenye bajeti yangu kesho mtaona, tumekuwa tunapanga fedha kusaidia kazi hii tunayofanya. Leo kwa mfano tunapanga matumizi bora ya ardhi na kupanga na kupima kila kipande cha ardhi. Tumeanza Mkoa wa Morogoro katika wilaya tatu. Namwalika mwuliza swalii siku moja katika Wilaya za Kilombero, Malinyi na Ifakara ili aje uone kazi inayofanya.

Mheshimiwa Spika, tumeanza mpango mwiningine ambao tunakamilisha sasa wa kutaka kupanga na kupima kila kipande cha ardhi nchi nzima. Sasa huo ndiyo mpango wa Serikali Kuu kwa uwezo wa Serikali Kuu. Kwa hiyo, yote mawili tunafanya; hatuwezi kuwaacha wenyewe jukumu lao wasifanye, lakini Serikali Kuu nayo imekuwa ikishiriki katika kufanya kazi hii tukijua kwamba tuna wajibu wa kufanya hivyo.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Mary Deo.

MHE. MARY D. MURO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa tatizo la migogoro ya ardhi Mkao wa Pwani inasababishwa na makundi makubwa ya mifugo inayotoka sehemu mbalimbali: Je, Serikali ina mpango gani kukaa Wizara ya Mifugo na Wizara ya Ardhi kupanga na kuzuia makundi hayo ya mifugo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri. Kama kijiji kweli kina wafugaji 10,000, iko shughuli.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, anasema ng'ombe.

Mheshimiwa Spika, dawa siyo kuzuia. Tunashirikiana kama Serikali moja na Wizara zote zinazohusika na matumizi ya ardhi ambao ni wadau kupanga matumizi bora ya ardhi, kupanga maeneo ya malisho na kuweka miundombinu. Hiyo ndiyo dawa ya kuwawezesha wafugaji watulie, wafanye shughuli zao za ufugaji kwa tija zaidi. Dawa siyo kuwaondoa wala kuwafukuza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali kwa ujumla kwa pamoja tunafanya hiyo mikakati na katika kazi ambayo alitutuma Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, katika ile timu ya Mawaziri wanane tumeandaa utaratibu ambao tunapendekeza utakuwa ndiyo mwarobaini ambao utawezesha kuainisha maeneo, kuyatambua, kuyapanga na kupanga miundombinu katika maeneo hayo ili wafugaji na wakulima waweze kukaa mahali salama ili waweze kuzalisha na kuongeza tija katika nchi hii.

Kwa hiyo Serikali kwa ujumla kwa pamoja tunafanya hiyo mikakati na katika kazi ambayo alitutuma Dkt. John Pombe Magufuli, katika ile timu ya Mawaziri nane tumeandaa utaratibu ambao tunapendekeza utakuwa ndiyo muarobaini ambao utawawezesha kuainisha maeneo kuyatambua, kuyapanga na kupanga miundombinu katika maeneo hayo

ili wafugaji nao na wakulima waweze kukaa mahali salama ili waweze kuzalisha na kuongeza tija katika nchi hii.

SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea swalii la Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri kwa Wizara hii hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Na. 326

Ujenzi Holela

MHE. ZAINAB M. AMIR aliuliza:-

Wananchi wengi wamejenga makazi yao bila kuzingatia mipangomiji na matokeo yake kuvunjwa nyumba zao bila kupata fidia pindi Serikali inapoanza ujenzi unaozingatia mipangomiji:-.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia wananchi elimu stahiki ili waepukane na adha hiyo?

SPIKA: Bado tuko kwako Mheshimiwa Lukuvi, majibu ya swalii hilo la Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri, tafadhalii

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amiri, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuwaelimisha wananchi kuhusu ujenzi unaozingatia mipangomiji ili kuepuka madhara mbalimbali ikiwemo kubomolewa nyumba zao bila kulipwa fidia. Mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kwa njia ya vyombo vya habari kama vile redio, luninga, magazeti, vipeperushi, machapisho mbalimbali, mitandao ya kijamii pamoja na tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utoaji wa elimu kuititia vyombo vya habari, viongozi wa Wizara wamekuwa wakitumia mikutano ya hadhara katika ziara zao nchini kutoa elimu kuhusu umuhimu wa wananchi kujenga kwa kufuata utaratibu hususan katika maeneo ambayo yametangazwa kuwa ni maeneo ya kimipangomiji. Aidha, kuititia kaulimbiu ya 'funguka kwa Waziri wa Ardhi' Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na mambo mengine amekuwa akipokea changamoto mbalimbali kuhusu ujenzi holela mijini na kutoa elimu stahiki kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kujenga kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo yameendelezwa bila kupangwa, Serikali imetoa fursa kwa wananchi kurasi mishiwa makazi yao na kupatiwa hatimiliki. Urasimishaji makazi pamoja na mambo mengine unasa idha kuwapatia wananchi fursa ya kutumia ardhi yao kama mtaji, kutoa miundombinu ya msingi, kupunguza migogoro, kuvutia uwekezaji na kuweka huduma za kijamii. Katika maeneo mengine ambayo urasimishaji haufanyiki, utambuzi wa milki na uhakiki hufanyika na wananchi wa maeneo hayo kupewa leseni za makazi ambazo zinasaidia kuimarisha usalama wa milki na kutumika kama dhamana za mikopo kutoka katika taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kusisitiza kuwa wananchi wazingatie sheria na taratibu za uendelezaji miji ili kujiepusha na ujenzi holela. Aidha, wananchi waepuke kujenga mijini bila kuwa na vibali vya ujenzi ili kuepuka maafa na madhara kwa mali zao.

SPIKA: Mheshimiwa Zainab Mndolwa, uliza swali la nyongeza.

MHE. ZAINAB M. AMIR: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nina maswali madogo ya nyongeza; kuna baadhi ya watu wanajenga katika mabonde na wengine wanajenga katika hifadhi za barabara na pia karibu kabisa na njia za reli lakini Serikali yetu kuititia halmashauri zetu kila mwaka

hukusanya kodi za majengo na kodi za ardhi katika maeneo hayo. Je, Serikali inatueleza nini kuhusu kadhia hii?

Mheshimiwa Spika, Swali langu la pili ili mwananchi aweze kujenga katika eneo husika ni lazima apate kibali kutoka katika mamlaka na sasa nauliza swali langu. Je, ni nini adhabu ambazo wanapewa watendaji ambao wanatoa vibali katika maeneo ambayo ni hatarishi? Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri tafadhalii

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wako watu ambao wamejenga katika hifadhi za barabara, hifadhi za miundombinu mbalimbali na mabondeni lakini wamefanya hivyo kinyume cha sheria na Serikali hairuhusu na hata zoezi la urasimishaji na utoaji wa leseni za makazi hautafanyika wala hatutarasimisha makazi kwa watu ambao wamejenga katika maeneo hatarishi na maeneo ambayo yamepangwa na wapangamiji kama maeneo ya hifadhi ya barabara au maeneo ya miundombinu. Kwa hilo nakiri ni kosa wako watu wamefanya namna hiyo na sheria lazima ichukue mkondo wake kwa sababu ya kuwasaidia wao lakini kusaidia maendeleo ya miji yetu.

Mheshimiwa Spika, pia ni kweli kwamba kodi inakusanya kwa sababu hawa watu lazima walipe kodi, kuishi kwao kule wanatumia rasilimali za Halmashauri husika, kwa hiyo halmashauri zile zinapaswa kuwatoza kodi katika maeneo yale kwa sababu na wenyewe wanatumia rasilimali na *infrastructure* zilizoko kule lazima wachangie, Hilo linafanyika na ni kweli lazima watoe kodi, lakini ujenzi katika maeneo hayo hairuhusiwi. Kwa hiyo huwezi kujenga tu eti kwa sababu unataka kukaa mabondeni halafu usitozwe kodi kama wanavyotozwa Watanzania wengine. Ni kweli kodi za

majengo zitatozwa na kodi mbalimbali za halmashauri wanazotoza raia wengine zitazozwa, lakini hiyo haihalalishi kwamba wewe hapo umekaa kihalali. Lolote likitokea linaweza likatokea kama wapangaji na halmashauri husika wakiamua kuchukua hatua za kisheria.

Mheshimiwa Spika, la pili vibali vya ujenzi zamani vilikuwa vinatolewa zamani vilikuwa vinatolewa na Kamati ya Mipangomiji ya Madiwani lakini sasa utaratibu Serikali ya Awamu ya Tano imebadilisha kwa sababu ilikuwa inachelewesha sana na ilikuwa inachukua gharama kubwa sana, inamaliza hela nyingi kwa ajili ya posho ya vikao na kila kitu. Sasa hivi iko timu ya wataalam tu wa Serikali ambao ndiyo wanatoa vibali vya ujenzi na tumesema vibali visichukue zaidi ya siku tatu viwe vimeshatoka, kwa sababu watu wako pale wana uwezo wa kwenda kufanya ukaguzi na ni wataalam waliobobea katika kazi hiyo na vibali vya ujenzi lazima zitolewe. Kwa hiyo vibali sasa vinatolewa kwa kasi na hii imesababisha kupunguza hata gharama kwa wananchi za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni kweli kwamba siku za nyuma ilionekana kwamba watu waliweza kutoa vibali hata kwa watu ambao wametakiwa kujenga kwenye maeneo yasiyoruhusiwa. Serikali kwa wakati tofauti imechukua hatua kali na wengine wameachishwa kazi kwa wale ambao wametoa vibali katika maeneo ambayo hayastahili. Kwa hiyo Serikali imekuwa inachukua hatua za kinidhamu mara kwa mara, lakini nataka kumhakikishia katika Awamu hii ya Tano hilo halifanyiki. Awamu ya Tano imejenga nidhamu tofauti, watu ni wale wale lakini nidhamu yao imekuwa tofauti, hawatoi vibali tena hovyo hovyo na hawatatoa tena vibali katika maeneo ambayo ni hatarishi.

SPIKA: Mheshimiwa Hongoli na Mheshimiwa Ester.

MHE. JORAM I. HONGOLI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tatizo la makazi holela sehemu nyingi linasababishwa na kukosa wataalam wa kupanga, kupima na hatimaye kutoa

hati. Jimbo la Lupembe, Halmashauri ya Wilaya ya Njombe hatuna Afisa Ardhi wala hatuna Afisa Mpima, tuliyenaye pale ni afisa tu ni kama *technician*. Je ni lini Halmashauri ya Wilaya ya Njombe itapata Afisa Ardhi ili aweze kutusaidia katika kupanga na kupima na baadaye kutoa hati? (*Makofi*)

SPIKA: Tatizo hilo lilo katika halmashauri nyingi nchini, Mheshimiwa Waziri majibu halmashauri nyingi hazina seti kamili ya Mabwana Ardhi

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA

MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la ndugu yangu Mbunge wa Njombe la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maswali haya bila shaka yananipunguzia muda wa kujadili kesho pengine utapungua utakuwa siku moja, maana ni haya haya ambayo nitasema kesho.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kama ulivyo sema mwenye tunao upungufu wa Maafisa Ardhi na katika *speech* yangu nimetoa uwiano ikama inasema nini lakini tulionao ni wangapi. Nataka kukuhakikishia zoezi hili litapunguza makali kidogo mwezi wa Saba ambapo Wizara yangu sasa itaanza kupanga upya hawa maafisa, wanahamishwa na kupangwa na Wizara yangu, kwa sababu tumegundua siyo kwamba ikama ilikuwa inasababisha lakini upangaji ulikuwa hauzingatii mahitaji. Ukienda Mkoa wa Mwanza kwa mfano Wilaya za Nyamagana na Ilemela unakuta kuna Maafisa Ardhi themanini lakini Njombe hakuna hata mtu mmoja. Kwa sababu tatizo ni kwamba wale wapangaji pengine pale walipokuwa wanasimamiwa hawakuwa na fani zinazofanana nao, kwa hiyo walikuwa hawajui fani gani ipangwe namna gani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nataka niwahakikishie Wabunge wote mwezi wa Saba tutawapanga hawa hawa wachache, lakini tutajitahidi angalau kila wilaya iwe na afisa angalau wa taaluma moja ya ardhi aweze kuwepo. Nazijua baadhi ya wilaya ambazo hazina hata mtu mmoja wa sekta

nzima ya ardhi ambayo ina vitengo vitano, hawawezi kufanya shughuli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi lako tutalitekeleza mwezi wa Saba na la Waheshimiwa Wabunge, tutawapanga upya na Njombe, tatizo la Njombe Afisa Ardhi alikuwa mtendaji mzuri sana nimempandisha cheo amekuwa Kamishna Msaidizi. Kwa hiyo nitampelekea mtu mwingine baada ya hapo na Waheshimiwa Wabunge wote wenye swali kama hili watusubiri mwezi wa Saba Mungu akipenda tumeamua kuwapanga upya, nitawaita hapa kwanza niwaelekeze lakini tutawapanga upya ili angalau kila wilaya tuwe na afisa anayeweza kufanya kazi fulani.

SPIKA: Mheshimiwa Ester Bulaya nishakutaja, uliza swali la nyongeza

MHE. ESTHER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi tunajua moja ya Serikali kuwa na mikakati ya mipango bora ya ardhi ni pamoja na kuzuia watu kujenga mabondeni na pamoja kwenye mikondo ya mito na Serikali ilianzisha operesheni ya kubomoa nyumba za watu ambao wamejenga kwenye mikondo ya mito na hili ni tangu Bunge liliopita Mheshimiwa Lukuvi nadhani analijua na amebomoa nyumba nyingi tu kule Kawe lakini kuna nyumba ya kigogo mmoja tu ameiacha na wamekuwa wakitoa ahadi humu ndani hiyo nyumba itabomolewa. Nataka kujua ni lini ile nyumba itabomolewa?

SPIKA: Bado naangalia kama hili swali kweli liruhusiwe au. Mheshimiwa Waziri ufanuzi tafadhal kama umelielewa swali.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Bunda Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali imekuwa inachukua hatua za mara kwa mara na nikisema Serikali maana yake kwa umoja wetu na wasimamizi wa sheria zote

za mipangomiji ni mamlaka ya upangaji ambayo ni halmashauri yenyewe. Ukitikia operesheni ya vunja vunja au kuondoa watu waliojenga kinyume cha sheria katika halmashauri fulani, ujue inaendeshwa na halmashauri ambayo ndiyo yenyeye mamlaka na hata ile *eviction order* ya kwenda kuwavunja haitolewi na Wizara yangu, hapana inatolewa na Afisa Ujenzi wa Wilaya. Kwa hiyo mazoezi haya yamekuwa yanafanyika katika wilaya mbalimbali ili kuwaondoa watu ambao wamevunja sheria naamini ni kweli katika wilaya mbalimbali ikiwepo Dar es Salaam Kinondoni operesheni kama hizo zimeendeshwa kwenye bonde la Msimbazi kwa watu ambao wamevunja sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninachoomba tu ni kwamba wananchi wazingatie sheria. Wasijenge bila vibali, wahakikishe kwamba kila wanapojenga wanajenga maeneo ambayo siyo hatarishi, wanafuata sheria illi angalau hatua kama hizi zinazozungumzwa na Mheshimiwa Mbunge zisiwapate. Hilo ndilo ombi langu.

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano swali litaulizwa na Mheshimiwa Mattar Ally Salum, Mbunge wa Shauri Moyo. Mheshimiwa Mattar.

Na. 327

Kampuni ya Azam Marine

MHE. MATTAR ALI SALUM aliuliza:-

Kampuni ya *Azam Marine* ambayo inafanya biashara ya kusafirisha abiria kwa kutumia boti kuititia baharini, huuza tiketi kwa abiria kwa ajili ya safari lakini abiria anapochelewa safari tiketi hiyo huwa haitumiki na hivyo kusababisha hasara kwa abiria pamoja na usumbufu;-

(a) Je, Serikali inalijua hilo?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua tatizo hilo?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Injinia Atashasta Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mattar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina taarifa ya jambo hili kwa kuwa limekuwa likijitokeza mara kwa mara. Ufutiliaji uliofanywa na Wizara yangu kupitia *TASAC* umebaini kuwa Kampuni iliyotajwa ina utaratibu wa namna abiria anavyoweza kuahirisha safari na namna nau li itakavyorejeshwa. Aidha, Kampuni hiyo imekuwa kuahirisha safari na namna nau li itakavyorejeshwa. Aidha, Kampuni imekuwa ikiruhusu abiria kutoa taarifa na kubadili muda wa safari bila gharama ya ziada ikiwa msafiri atatoa taarifa kabla ya chombo kuondoka. Utaratibu huu unatoa fursa kwa kampuni kuuza nafasi iliyoachwa wazi kwa wasafiri wengine ili kuepuka hasara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa vyombo vya kampuni hii vimesajiliwa katika daftari la usajili linalosimamiwa na Mamlaka ya Bandari Zanzibar (ZMA), Wizara yangu kupitia *TASAC* itaendelea kufanya ufuutiliaji kwa kushirikiana na Wizara husika Zanzibar kupitia ZMA ili kusimamia utekelezaji wa utaratibu huu wa Kampuni ili uwasaide abiria wanapoahirisha safari na kutoa taarifa kwa wakati.

SPIKA: Mheshimiwa Mattar Ali Salum, uliza swali lako la nyongeza.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana. Watanzania wengi wanapata hasara kubwa sana katika hili suala abiria akichelewa boti tu tiketi yake imekufa kabisa hawezi kutumia kwa wakati mwingine wowote inasababisha kadhia kubwa kwa Watanzania wetu.

Hakuna Shirika lolote la Ndege duniani ambalo ukichelewa tiketi yake inakuwa imekufa, unalipa kiwango cha fedha kama ni dola 50 tiketi yako inaweza kuendelea kufanya kazi, hata Shirika letu hili la Tanzania pia hata ukichelewa unaweza kupanda ndege kwa wakati mwingine lakini Kampuni hii ya *Azam Marine* ukichelewa tiketi imekufa kabisa wala huwezi kutumia tena ni jambo la ajabu sana. Sasa ni lini Serikali itaondosha kadhia hii ili hawa abiria wetu wapate maslahi makubwa kutumia vyombo hivi? Ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, naona swali limejirudia.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, kwanza siyo kweli kwamba mashirika yote ya ndege huwa tiketi yake ukichelewa yanarudishwa kuna zile *Easy Jets* ambazo kwa mfano *Fastjet* ukichelewa tiketi huwa haurudishiwi wala haupangiwi safari siku nyingine kwahiyio siyo kwamba ni mashirika yote ya ndege.

Mheshimiwa Spika, pia najaribu kuwashauri hata Watanzania wenzetu unapokuwa umepanga safari basi ujue kwamba kuna muda wa kuondoka na muda wa kufika. Haiwezekani tuwe tuna panga safari halafu unafanya mambo mengine tofauti na safari yako.

Katika majibu yangu ya msingi nimeeleza tu kwamba Shirika la *Azam Marine* huwa lina utaratibu ukitoa taarifa mapema tena waliandika kwenye tiketi yao nyuma ukitoa taarifa mapema kabla ya safari kwamba hutasafiri wana utaratibu wa kuiiza hiyo tiketi kwa watu wengine ili wewe wakupangie wakati mwingine, lakini sasa muuliza swali Mheshimiwa Mbunge ye ye nafikiri anafikiri kwamba akishachelewa bila kutoa taarifa anaweza akapewa, sasa ye ye Azam Marine atakuwa ameingia hasara kitu ambacho siyo kweli.

Mheshimiwa Spika, nawashauri Watanzania tupange safari zetu tuwe na uhakika wa kusafiri siku husika, tujiandae,

halafu tuweze kuwahi ili tusipate matatizo kama hayo.
(*Makofii*)

SPIKA: Ndiyo maana mwenye chombo ile *seat* inaenda tupu, sasa nani ale hasara hapo? Mheshimiwa Khadija Nassir nimekuona, uliza swali la nyongeza

MHE. KHADIJA NASSIR ALI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniona. Serikali imekuwa ikitoa utaratibu elekezi wa kibei kwa maeneo mengi ya usafiri wa umma kwa wenzetu wenye mahitaji maalum na wanafunzi. Ni upi utaratibu uliowekwa kwenye usafiri wa maji kwa wenzetu hawa wenye mahitaji maalum? Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi wa swali hilo, tafadhalii.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Khadija Nassir kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vyombo vya Serikali utaratibu upo tunazo meli za *MSCL* ambao kwa kweli utaratibu wa nauli huwa upo na uko wazi, lakini kwa vile vyombo ambavyo ni vya binafsi ambavyo vinasaidiana na Serikali katika kuhudumia wananchi, huwa tunaacha soko lijipeleke lenyewe, lijiendeshe. Kwa hiyo wale watu wanaomiliki vyombo vya usafiri wa majini huwa wanapanga bei kutokana na faida wanahisi wataipata pamoja na huduma ambazo wanawenza wakawasaidia wananchi.

SPIKA: Nilikuona Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza kwenye eneo hilo.

MHE. NAPE M. NNAUYE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutambua jitihada za Serikali katika kuboresha mawasiliano na uchukuzi katika nchi

yetu na hasa maboresho yaliyofanyika katika Shirika la Ndege la Tanzania sasa hivi kumeanza kujitokeza tatizo la ucheleweshaji wa ndege. Kila mara unaposafiri ndege inasogezwa, inasogezwa, inasogezwa na hili jambo linakera sana. Chanzo cha tatizo hili ni nini na Serikali mnachukua hatua gani kurekebisha? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, wanasema *ATCL* ndiyo imekuwa kidogo na ucheleweshaji wa ndege.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Mbunge wa Mtama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika siku za karibuni kumetokea changamoto ya uchelewaji (*cancelation*) kwa Shirika letu la Ndege la Tanzania. Tatizo hili limetokana na sababu mbalimbali za kiufundi ambazo zimerekebishwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye hotuba ya kuhitimisha bajeti yetu tulitoa maelekezo Menejimenti na Bodi ya *ATCL* kwamba kama kutakuwa na *cancelation* yoyote au *delay* ya zaidi ya nusu saa tupate taarifa ya maandishi ya sababu zilizobabisha hiyo ndege ichelewe kuondoka kwa zaidi ya nusu saa. Hilo limeshaanza kufanyika na huwa tanapata taarifa.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kuwasisitiza *ATCL* kwamba wateja ndiyo watu wa thamani sana. Kwa hiyo, *delay* ambazo hazina sababu ya msingi ziepukwe sana.

Mheshimiwa Spika, nikutaarifu wewe na Bunge lako kwamba sasa hivi marekebisho yameshaanza kufanyika. Sasa hivi *ATCL* wameshaanza kwenda vizuri, *delayna cancelation* ambazo sio *technical* hazitokei tena.

SPIKA: Nilikuona upande wa *CUF*, Mheshimiwa Yussuf.

MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Adhabu ya kaburi aijuaye maiti. Sisi tunaosafiri na Azam ndiyo tunafahamu adha yake.

Mheshimiwa Spika, hata ukisafiri na ile *charter* ya abiria 11 mzigo wa kilo 15 - 20 hulipishwi lakini ndani ya boti ya Azam unalipishwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri achukue mfuko mmoja wa mchele tulioingia asafiri nao aone kama hatalipishwa. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ifuatilie suala hili na itupatие ufumbuzi.

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu, kulipia mzigo ni sawasawa au siyo sawasawa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yussuf, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la huduma ya safari za majini mara nyingi ni kati ya abiria na mwenye mali. Ukifugua nyuma ya tiketi ile kuna masharti ambayo yanaandikwa kwa uwazi na kwa lugha nyepesi kabisa. Ninawashauri sana Watanzania tuwe tunasoma masharti yale ili kama ukiona hayakidhi mahitaji yako basi usiende. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nyuma tiketi ya Azam kuna maelezo yanayoeleza mpaka kiwango cha mzigo unachotakiwa kwenda nacho ndani ya meli. Sasa anayepima ni yule mwenye meli kama imezidi anaruhusiwa kukukatalia kwa sababu ndiyo mkataba ulioingia wewe abiria na yule mwenye meli. Kwa hiyo, nawashauri Watanzania tuwe tunasoma vigezo na masharti vyatia kuingia kwenye huduma hizo.

SPIKA: Ahsante kwa majibu mazuri. Tunahamia Wizara ya Maji, swali la Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, uliza swali lako Mheshimiwa.

Na. 328

Mchoro wa Mradi wa Maji – Mto Ruvuma

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA aliuliza:-

Wizara ya Maji ilikubali kurekebisha mchoro wa Mradi wa Maji kutoka Mto Ruvuma hadi Mtwara ili vijiji vingi vya Halmashauri ya Nanyamba vipate maji toka Mto Ruvuma:

- (a) Je, marekebiso hayo yamefikia hatua gani?
- (b) Je, ni vijiji vingapi vya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba vitanufaika na mradi huo
- (c) Je, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Prof. Mbarawa, tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ilikubali kufanya marekebiso ya mchoro wa Mradi wa kutoa Maji kutoka Mto Ruvuma kwenye Manispaa ya Mtwara Mikindani ili kuongeza idadi ya vijiji zaidi vikwemo vya Halmashauri ya Nanyamba.

Mheshimiwa Spika, usanifu wa mradi huo ulishakamilika, hivyo, mabadiliko ya mchoro yatafanyika wakati wa utekelezaji wa mradi huo kabla ya kuanza kwa ujenzi wa kazi hiyo. Idadi ya vijiji vitakavyoongezwa itajulikana baada ya mabadiliko ya mchoro yatakayofanywa na Mtaalam Mshauri atakayesimamia ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa mradi huo unakadiriwa kugharimu kiasi cha Dola za Marekeni milioni 189.9. Kwa sasa

Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha za utelekezaji wa mradi huo na unategemea zaidi upatikanaji wa fedha ili kazi iweze kuanza.

SPIKA: Mheshimiwa Chikota, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, katika mipango yetu ya Halmashauri ya Mji wa Nanyamba kuna vijiji tumeviacha kwa sababu vipo jirani na mradi huu na sasa hivi havijapangiwa mradi wowote. Sasa napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri kwa kuwa amesema marekebisho yatafanywa wakati Mtaalamu Mshauri atakapopatikana, je, Serikali ipo tayari kutoa meeleteko maalum kwa Mtaalam Mshauri ili vijiji 20 vikiwemo Maembe Chini, Maembe Huu, Kiromba na vijiji viingizwe kwenye mradi huu?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kuhusu utekelezaji wa mradi. Ni muda mrefu sasa Serikali inasema inatafuta fedha, je, haioni muda umefika sasa hivi kutekeleza mradi huu kwa kutumia fedha za ndani? (*Makofii*)

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji, tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chikota, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Maji tumeweka mwongozo sasa hivi ambao unaeleza waziwazi kwamba vijiji vyote vilivyo kwenye vyanzo vya maji ndivyo vitapata huduma ya maji kwanza wakati wa kutekeleza mradi. Pili, kila linapopita bomba la maji kilomita 12 pande zote za bomba hilo la maji vijiji vilivyo pembedi vitapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vijiji alivyosema Mheshimiwa Mbunge, kwanza, tuna mpango wa kupeleka maji vijiji, kwa mfano, Maembe Chini na Maembe Juu, Kirombo, Kirombo Chini, Mchanje na Mji Mwema. Vijiji vyote hivi pamoja na vijiji 14 vitapata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili anauliza, je, Serikali tusianze mradi huu kwa kutumia pesa za ndani. Mradi huu gharama yake ni kubwa, kama nilivyo sema ni shilingi bilioni 400. Wizara ya Maji bajeti yake takribani ni shilingi bilioni 673. Kwa kutumia pesa za ndani maana yake miradi yote sasa itashindwa kutekelezwa. Kwa hiyo, kama nilivyo sema kwenye jibu la msingi tunahakikisha kwamba tunatafuta pesa hiyo ili mradi huo uweze kuanza mara moja.

SPIKA: Tullibakize swalii hilo Mto Ruvuma, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

MHE. HAWA A. GHASIA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri alipotembelea Mkoa wa Mtwara alionyesha huu mradi kutokuwa katika mipango yake. Je, amebadilisha mawazo lini kwamba huo mradi utatekelezwa sasa hivi?

SPIKA: Majibu ya swalii hilo, Mheshimiwa Waziri wa Maji, Profesa Mbarawa, tafadhali.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Ghasia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mipango mingi ya kutekeleza miradi ya maji katika maeneo mbalimbali. Nami kama Waziri siwezi nikabadilisha mpango wowote wa Serikali kwani natekeleza mipango ya Serikali. Mradi bado upo kwa sababu ulipangwa na Serikali na utatekelezwa. Hata hivyo, kwa wakati huu tuna miradi mingine ambayo itatekelezwa huko Mtwara na mipango inaendelea vizuri.

SPIKA: Mheshimiwa Kiruswa.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza kwa Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani zangu za dhati kwa sababu Mheshimiwa Prof. Mbarawa amepambana bega kwa bega nami mpaka yale maji ya Mlima Kilimanjaro yakawafikia wananchi wa Wilaya ya Longido. Sasa hivi ametutengea shilingi bilioni 2.9 kusambaza yale maji na wale wananchi wanaoishi pembezoni mwa bomba watapata maji wao pamoja na mifugo yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kitu kilichobaki kuhusiana na mradi huo ni kwamba Mheshimiwa Rais alipokuja Namanga kuzindua mpaka wa pamoja mwezi Februari, 2019 aliiwaahidi wananchi kwamba mradi huo kwa sababu unaleta maji mengi mpaka Longido utaongezewa *extension* ili uwafikie wananchi walioko njiani mpaka Namanga. Je, ahadi hii ya Rais itaanza kutekelezwa lini?

SPIKA: Ni lini Profesa utekelezaji utaanza, majibu tafadhalii.

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Rais alitoa ahadi hiyo nasi wakati wote tunatekeleza ahadi za Mheshimiwa Rais pamoja na viongozi wote wa juu. Kazi tunayofanya sasa hivi ni kufanya usanifu kutoa maji kutoka Longido mpaka huko kwenye mpaka wetu wa Namanga. Mara baada ya usanifu huo kumalizika kazi ya ujenzi itaanza mara moja.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kazi hii itaanza mara moja na tumejipanga kuhakikisha kazi hii tutaifanya kwa pesa zetu za

ndani na kwa kutumia wataalamu wetu wa ndani. Tunaamini tukifanya hivyo kazi itakamilika haraka iwezekanavyo.

SPIKA: Mheshimiwa Jaku, Mambo ya Nje, uliza swalilako. Kama Mheshimiwa Jaku hayupo basi Mheshimiwa Machano kwa niaba yake.

Na. 329

TRA Kutatua Kero za Wafanyabiashara Nchini

MHE. MACHANO OTHMAN SAID (K.n.y. MHE. JAKU HASHIM AYOUB) aliuliza:-

(a) Je, ni lini *TRA* itakaa na wafanyabiashara wa Tanzania kusikiliza vilio vyao licha ya kila Mkoa unayo Ofisi ya *TRA*?

(b) Je, ni sababu gani zinazofanya mizigo inayotoka Zambia, Uganda, Kenya, DRC haipati usumbufu inapoingia Jijini Dar es Salaam katika bandari lakini mizigo kutoka Zanzibar inakuwa kero kubwa inapoingia Jiji la Dar es Salaam kupitia bandarini?

(c) Je, ni lini *TRA* itaweka Ofisi kila Mkoa kusikiliza kero za wafanyabiashara ambao wanahisi wanaonewa na vilevile kuweka Mwanasheria kila Ofisi ili pasiwepo na manung'uniko ya wafanyabishara kuonewa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji.

***NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO* alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jaku Hashimu Ayoub, Mbunge wa Baraza la Wawakilishi, lenye sehemu (a) (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mionganoni kwa kazi za kila siku za Mamlaka ya Mapato Tanzania ni kusikiliza na kutatua kero za wafanyabiashara ili kuwawezesha kufanyabiashara zao bila usumbufo. Mamlaka ya Mapato Tanzania hufanya mikutano au vikao na wafanyabiashara katika ngazi ya Wilaya, Mikoa na Taifa ili kutoa elimu ya kodi, kusikiliza vilio au kero zao na kuzifanyia kazi; hurusha vipindi maalumu katika televisheni na radio vinavyotoa elimu ya kodi kwa wananchi na kujibu kero za wafanyabiashara; huboresha na kuweka kwenye tovuti ya Mamlaka taarifa mbalimbali za kikodi na pia hubuni na kuanzisha mifumo, vituo na vilabu rafiki vya kikodi ili kujibu vilio vya wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania imeanzisha *call centre*, Makao Makuu Dar es Salaam pamoja na Kituo cha Huduma za Ushauri kwa Mpakodi kilichopo Somara, Jijini Dar es Salaam ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara kuwasilisha maoni na kero za kikodi kwa wakati. Pia, Wenyevitii wa Kamati za Mapato za Mikoa na Wilaya ambao ni Wakuu wa Mikoa na Wilaya wamekuwa wakisilikiza kero za walipakodi katika Mikoa na Wilaya zao na kuzitatuufia ufumbuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii, kuwahimiza wananchi kutembelea Ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania zilizopo katika maeneo yao na kuhudhuria vikao vinavyoitishwa na Wakuu wa Mikoa na Wilaya ili kuwasilisha maoni na kero za kikodi.

(b) Mheshimiwa Spika, siyo kweli kwamba bidhaa za Zanzibar zinapata usumbufo ikilinganishwa na bidhaa za nchi jirani zinapoingia Tanzania Bara kwa sababu bidhaa zote zinafuata utaratibu wa forodha unaofanana. Bidhaa zinazoingia Tanzania Bara kutoka nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika kupata msamaha wa Ushuru wa Forodha lakini hulipiwa Kodi ya Ongezeko la Thamani pamoja na Ushuru wa Bidhaa.

(c) Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mapato Tanzania ina Ofisi katika Mikoa yote ya Tanzania pamoja na baadhi ya Wilaya zake. Aidha, baadhi ya Mikoa ina vituo maalum vya huduma za kodi hususani Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, pili, kila Mkoa una Mwanasheria na Afisa Elimu ya Kodi kwa ajili ya kutoa elimu, kusikiliza na kutatua kero za walipakodi. Pia, Mamalaka imeweka utaratibu wa Mameneja wa Mikoa ya kikodi kukutana na walipa kodi kila Alhamisi ili kusikiliza kero zao na kuzitatu. Hatua hii ina nia ya kujenga imani ya walipakodi, kutatua kero na kukuza ridhaa ya ulipaji kodi kwa hiari.

SPIKA: Mheshimiwa Machano, nimekuona.

MHE. MACHANO OTHMAN SAID: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Pamoja na majibu yake, naomba kuuliza swali moja la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wengi wa Zanzibar shughuli zao ni uvuvi; na kwa kuwa biashara ya dagaa ni kubwa sana kwa Zanzibar na soko lake kubwa ni Congo (DRC) na Rwanda. Ni sababu gani inasababisha kila tani moja ya dagaa kutozwa dola 400 katika mpaka wa Tunduma?

SPIKA: Majibu ya swali hilo kama unayo, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Machano, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nimemsikia vyema amezungumzia na kutaka kujua juu ya mgogoro wa usafirishaji wa mazao ya uvuvi (dagaa) kutoka Tanzania aidha Visiwani na Bara kwenda nje ya nchi na inaonekana tozo ni kubwa na wafanyabiashara kuishindwa kulipa tozo hiyo.

Mheshimiwa Spika, hapa karibuni Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi tulifanya mabadiliko ya tozo mbalimbali za mazao yetu ya mifugo na uvuvi. Tozo zile tulizoziweka zimepeleke wa fanyabiashara hasa wa Ukanda wa Pwani kuwa juu ya uwezo wao. Baada ya malalamiko makubwa, Wizara imeyapokea malalamiko yao, imeyafanyia kazi na tumefanya marekebisho ya tozo zile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya bajeti ya Wizara ya Fedha na tozo mpya kuitishwa na Serikali na kutangazwa katika Gazeti la Serikali, kuanzia tarehe 1 Julai, tunayo matumaini kwamba tozo zile zitashuka sana na wafanyabiashara wataendelea kutoa mazao yale ya mifugo kupeleka katika nchi zingine zinazohitaji. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mbunge na wafanyabiashara wote wawe na subra muda si mrefu majibu ya jambo hili yatakuwa yamepatikana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Khatib halafu Mheshimiwa Frank Mwakajoka ambaye yupo mpakani huko huko.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda nimuulize Mheshimiwa Waziri, umekuwepo utaratibu wa Waafrika wote, kutoka nchi mbalimbali wanapotaka kuja ndani ya Tanzania na usafiri wao binafsi wanaingia kwa kupata *permit* katika mipaka yetu. Je, ni kwa nini Wazanzibar ambao wanataka kuingia na magari yao Tanzania Bara kwa ajili ya matumizi na kurudi Zanzibar, hawapati ruhusa hiyo na badala yake wamekuwa wanawekewa vikwanzo kuingia na magari yao kwa matumizi binafsi na baadaye kurudi nayo Zanzibar?

SPIKA: Sijui kama swali hilo ni la Wizara ya Fedha au ni la wapi? Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali moja la Mheshimiwa Khatib, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, amesema vizuri Mheshimiwa Khatib lakini angetusaidia pia kama hata yeye wakati ameingia Tanzania Bara na gari lake alipewa *permit* kwa ajili ya kuendesha gari lake hilo huku Tanzania Bara?

Mheshimiwa Spika, niliambie Bunge lako Tukufu kwa nini tuko katika mkanganyiko huo. Siku zote naposimama hapa nimekuwa nikisema kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania Bara na Mamlaka ya Mapato Tanzania Visiwani wanatumia mifumo tofauti ya uthaminishaji wa mizigo. Ndiyo maana magari yanapopita Zanzibar kuja huku Tanzania Bara lazima yafanyiwe uthamini upya ili kujiridhisha na kodi ambayo imelipwa ili kuleta *fair competition* kwenye biashara zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hilo linafahamika vizuri na nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar wengi wao katika hilli hawakuballiani. Kwa hiyo, niombe tuweze kukubaliana kwenye jambo hilli ili tuondoke kwenye mkanganyiko huu na tuweze kuwahudumia watu wetu vizuri.

SPIKA: Nilishakutaja Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swalii la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nakumbuka mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga karibuni shilingi 900 kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwenye Wizara ya Fedha. Fedha hizi zilikuwa zinaenda kutoa elimu kwa walipa kodi wa Tanzania. Sasa hivi kumekuwa na kero kubwa sana ya kodi kwenye nchi hii na biashara nyingi zinafungwa katika Taifa hilli. Je, Serikali imejipanga namna gani kutoa elimu kwa walipa kodi ili Watanzania hawa waweze kujua wanalipa kodi kutoka kwenye faida au kwenye mtaji kwa sababu elimu hiyo mpaka sasa hivi hawana?

SPIKA: Elimu ya mlipa kodi, ufanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

SPIKA: Nilishakutaja Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nakumbuka mwaka 2017/2018 Serikali ilitenga karibuni bilioni 900 kwa ajili ya shughuli za maendeleo kwenye Wizara ya fedha, na fedha hizi, zilikuwa zinakwenda kutoa elimu kwa walipa kodi watanzania, na sasa hivi kumekuwa na kero kubwa sana ya kodi kwenye nchi hii, na biashara nyingi zinafungwa katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Je, Serikali imejipanga namna gani, namna ya kutoa elimu kwa walipa kodi ili Watanzania hawa waweze kujua wanalipa kodi kutoka kwenye faida, au wanalipa kodi kutoka kwenye mtaji? Kwa sababu elimu hiyo hawana mpaka sasa hivi, ahsante sana. (*Makofii*)

SPIKA: Elimu ya mlipa Kodi, ufanuzi Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwenye jibu langu la msingi, nimeelezea Elimu ya Kodi hutolewa katika ngazi mbalimbali, kuanzia ngazi ya Taifa Mamlaka ya Mapato Tanzania hukaa na Wafanyabiashara kuwapa Elimu ya Kikodi *physically* yaani uso kwa uso lakini pia kupitia Vyombo mbalimbali vya Habari.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata sisi Viongozi Wakuu wa Wizara ya Fedha tumekuwa tukizunguka katika Mikoa mbalimbali kukutana na wafanyabiashara na kupeana Elimu ya Kikodi tukiwa na Wataalamu wetu wa Kikodi. Lakini pia kila mwezi Wakuu wa Mikoa huwa na Mabaraza ya Biashara kwenye Mikoa yao, hukutana na wafanyabiasha na kutoa Elimu ya Kikodi Wataalamu wetu wa Kikodi wanakuwepo.

Vilevile Wakuu wa Wilaya wana Mabaraza ya Biashara ya Wilaya ambapo hukutana na wafanyabiashara, wataalam wetu wa Kodi wakiwepo na Elimu ya Kikodi hutolewa.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa Watanzania, kwa Wafanyabiashara wote kuchukua jukumu la kuhudhuria Mikutano hii ili waweze kupata Elimu ya Kikodi na kero zao mbalimbali za Kikodi ziweze kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Mwakajoka amesema biashara nyingi zimefungwa, hili ni suala ambalo linaongelewa katika ujumla wake, nilishaliambia Bunge lako Tukufu kufungwa na kufunguliwa kwa Biashara ni jambo la kawaida katika Mataifa yote Duniani, siyo kwa Tanzania peke yake, na nilishaeleza, *rate* ya Biashara kufungwa ni ndogo kuliko *rate* ya Biashara zinazofunguliwa, nashukuru sana.

SPIKA: Mheshimiwa Rukia swali la mwisho kabisa la nyongeza.

MHE. RUKIA AHMED KASSIM: Mheshimiwa Spika, ahsante, nami kunipa nafasi ya kuweza kumuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha swali la nyongeza, nilitaka kujua kwa sababu Mbunge ana haki ya kuleta gari yake kwa kuititia *exemption* kama Mbunge, ana haki ya kuileta Tanzania Bara au Tanzania Visiwani. Ni kwani basi anapoleta gari yake Tanzania Visiwani, akileta Bara hawezikupewa namba ya hapa mpaka anaambiwa ailiipie *difference?* (*Makofii*)

SPIKA: Swali linawahu su Waheshimiwa Wabunge kutoka Zanzibar, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nimeshaeleza changamoto ya Kimfumo tuliyonayo, unapopewa namba ya Tanzania Bara, maana yake gari ile inasajiliwa kutumika Tanzania Bara, kwa hiyo, kama inasajiliwa kutumika Tanzania Bara na utofauti wa Kimfumo nilioueleza ni lazima tuweze kuthaminisha gari yako sasa inasajiliwa Tanzania Bara tukupe namba ya Tanzania Bara na uweze kulipia utofauti ule wa Kodi uliopo kwa sababu ya mfumo wetu wa utofauti kati ya Mamlaka mbili hizi ili gari lako liweze kutumika Tanzania Bara.

SPIKA: Muda leo ni siku ya Wizara ambayo ni ya siku moja, kwa hiyo inabidi tuendelee na tuna wageni wengi sana, kwanza Wageni wa Mheshimiwa Spika, Wageni 32 ambaao ni Walimu na wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya Laikala iliyopo Wilayani Kongwa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo Ndugu Maine Tendewa, naomba wanafunzi wa Laikala msimame, Laikala Sekondari, ahsanteni sana, karibuni sana, karibuni sana kutoka kule Kongwa. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge endeleeni tu kusimama, Waheshimiwa Wabunge watoto hawa wanatoka kwenye ambacho ndiyo nilikulia toka nikiwa mdogo kabisa. (*Makof*)

Ni moja ya vijiji vya ndani kabisa kule Wilayani Kongwa, *Interior* yaani, wako vijana huwa wanasesma humu wametoka kwenye familia maalum, mimi natokana na familia hizi, wakati huo, wakati huo nilipokuwa nasoma Shule ya Msingi, hatukuwa na Shule ya Msingi kwenye Kijiji chetu, hichi wanachotoka hawa. (*Makof*)

Kwa hiyo, nilikuwa natembea kwenda Kijiji jirani maili tano, ambako ni kilometra 8 kwenda na kilometra 8 kurudi, kwa siku moja nilikuwa natembea kilometra 16, kwa hiyo kwa wiki moja nilikuwa natembea kilometra 80. Mnaweza mkaelewa kwa mwaka ilikuwa ni km ngapi? Lakini, leo tuna maendeleo kiasi fulani tuna Shule za Msingi, na tuna Sekondari sasa na ushahidi ni watoto hawa, kwa kweli nchi inasonga mbele. (*Makof*)

Na, ni Kijiji cha wafugaji na mnafahamu *plate* ya wafugaji na mimi nilichunga ng'ombe sana, kwa hiyo, wanangu karibuni sana Bungeni, karibuni sana Dodoma, ahsanteni sana na mna karibishwa. (*Makof*)

Lakini, pia nina wageni 60, Diwani wa Kata ya Mtanana, Mheshimiwa Musa Chiwanga na wanafunzi wa kutoka Mtanana Shule ya Msingi, Mtanana simameni wote. (*Makof*)

Ni walimu hawa, ni walimu wa wafanyakazi wa Kata ya Mtanana walikosea kuandika hapa, karibuni sana, karibuni sana, Mtanana ni pale njiani mkitoka Kibaigwa mnapotremka pale kabla hamjaingia Ranchi ahsanteni sana na karibuni sana hapa Bungeni, ahsanteni sana. (*Makofi*)

Lakini, kipekee nina Mgeni pia ambaye ni Meneja wa Ranchi ya Kongwa Raymond Lutege, naomba usimame Raymond, huyu ndiyo Meneja wetu pale, basi mkipita kwenda Dar es Salaam mkirudi iko nyama pale *first class*. (*Makofi*)

Sisi kwa masuala ya Ufugaji ni wataalam kabisa, kwa hiyo kuna nyama nzuri kabisa Meneja wetu yuko pale kuwahudumia na huduma ni ya daraja la kwanza, ahsante sana Meneja. (*Makofi*)

Sasa, tuje kwa Wageni wa Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe, Katibu Mkuu, ahsante karibu. (*Makofi*)

Naibu Katibu Mkuu, Balozi Ramadhan Mwinyi, karibu sana, Wageni wengine wa Mheshimiwa Kabudi ni Mbunge na Mwenyekiti wa Wabunge wa Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki Dkt. Abdullah Makame, karibu sana. (*Makofi*)

Mbunge wa Afrika Mashariki Happiness Lugiko, karibu, Mbunge wa Afrika Mashariki *Engineer* Habibu Mnyaa karibu, Mbunge wa Afrika Mashariki Dkt. Ngwali Maghembe karibu sana, Mbunge wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Josephine Lemoyani karibu sana. (*Makofi/Vigelegele*)

Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *Engineer* Steven Mlote, karibu sana. (*Makofi*)

Pia wapo wageni kutoka Balozi mbalimbali, na Mashirika ya Kimataifa kama ifuatavyo Balozi wa Afrika Kusini

yupo hapa, Mheshimiwa Thamsanqa Mseleku, karibu sana Balozi. (*Makofi*)

Balozi wa Rwanda, Mheshimiwa Eugene Segore Kayihura, Balozi wa Rwanda, Balozi wa Zambia, Benson Keith Chali karibu, Balozi wa Poland Krzysztof Buzalski karibu sana, Balozi wa jirani Uganda Richard Kabonero karibu sana, Balozi wa Burundi Gervais Abayeho, karibu sana jirani. (*Makofi*)

Balozi wa Ireland Paul Sherlock karibu sana, Balozi wa Jamhuri ya Korea Mheshimiwa Choe Toe - Ick, karibu sana, Balozi wa Sweden Anders Sjoberg karibu Balozi, Balozi wa Italia, Roberto Mengoni yuko Balozi wa Denmark Einar Hebogard Jensen, Balozi wa Cuba Comrade Lucas Domingo Hernandez. (*Makofi*)

Jirani, Balozi wa Kenya Dan Kazungu, Balozi wa Norway Elisabeth Jacobsen, ahsante sana, Balozi mdogo wa Ujerumani Joerge Herrera Katibu Mkuu wa Pan African Postal Union (PAPU) Younouss Djibrine karibu, Mwakilishi wa UNIDO Stephen Kargbo karibu pia, Mwakilishi wa Angola Joel Cuvuna. (*Makofi*)

Mwakilishi wa India Chandramouli, Mwakilishi wa Nigeria Bintu Bwala Ekikor, Mwakilishi wa Jamhuri ya Kidemokrasia DPRK Korea hii, Kim Yong, Korea Kaskazini, Mwakilishi wa Zimbabwe Martin Tavenyika karibu, Mwakilishi wa Kuwait Nassir Aramzi karibuni, Mwakilishi wa Namibia Jason Nendongo karibu sana Mwakilishi wa Namibia, Mwakilishi wa Urusi Chitaev Vassily Russia, karibu Mwakilishi wa China Lin Liang karibu, Mwakilishi wa Ufaransa Alexander Peaudeau, ahsante. (*Makofi*)

Mkuu wa Ofisi wa Mwakilishi wa UNESCO Tirso Dos Santos, Mkuu wa Ofisi Dodoma World Food Programme, Neema Sitta, Mkurugenzi Asasi ya Kidiplomasia ya Vijana Emanuel Kasonga. (*Makofi*)

Lakini pia wapo Washindi wa mashindano ya Insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao ni pamoa na Mshindi

wa mwaka 2017 kutoka Sekondari ya Kibaha ameambata na Wazazi wake Michael Msafiri Nyaruga, yuko wapi yule, Nyaruga Michael, eehe! Huyo hapo, ahsante sana Michael unaendeleza Bendera, na mimi nilisoma Kibaha Sekondari pia kwa hiyo ahsante. (*Makofî*)

Lakini, pia kwa Mshindi wa mwaka 2018 kutoka Sekondari ya Moshi ameambata na Mama yake Mzazi anaitwa Innocent Shirima, ahsante sana Innocent Shirima, Shule zangu zote mbili, na mimi A level nilisoma Moshi. (*Makofî*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje, ambao ni familia yake wakiongozwa na Mke wake wa Mheshimiwa Flora Ndumbaro, ahsante Shemeji yuko wapi, Flora yuko wapi? Ehhe, karibu sana Flora, ahsante sana. (*Makofî*)

Mkimuona Ndumbaro amepiga tai hapo basi mjue Flora amerekebisha tai. (*Kicheko*)

Lakini pia, Yuko Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ni Katibu wa CCM Kata ya Lizaboni iliyopo Manispaa ya Songea Ndugu Stambuli Abdilai, karibu sana Stambuli, karibu sana Katibu. (*Makofî*)

Wageni wengine 43 wa Mheshimiwa Ndumbaro ni wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Songea wakiongozwa na Andrew Msuha *UDOM* ahsanteni sana, eehe, hata wangoni mko Vyuo Vikuu sasa, kweli maendeleo makubwa, karibuni sana Mjengoni. (*Makofî/Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Machano Othman Saidi ambaye ni Mheshimiwa Haji Omar Heri Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Idara Maalum ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Mheshimiwa Haji Omar Heri, ahsante sana, karibu sana Mheshimiwa Haji, karibu sana. (*Makofî*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, Wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Aweso Naibu Waziri wa Maji na

Umwagiliaji ambao ni jamaa zake na wapiga kura wake kutoka Pangani Mkoa wa Tanga, wakiongozwa na Ndugu Kiyonga Mohamed, karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Anna Lupembe Ndugu Joseph Kisuo, karibu popote pale ulipo, Mgeni wa Mheshimiwa James Millya Ndugu Omar Elias kutoka Dar es Salaam karibu, karibu popote pale ulipo, Mgeni wa Mheshimiwa George Simbachawene ambao ni wanafunzi 40 na walimu wanne kutoka Shule ya Sekondari ya Mteradam ya Mkoani Dodoma wakiongozwa Mwalimu Tumsifu Mtui, Walimu wa Mtera, wanafunzi wa Mtera karibuni sana, karibu sana, pamoja na walimu wenu, karibuni sana, tuna tumaini mmetuletea samaki toka Mtera, karibuni sana, wale ambao hawaelewi masuala ya Mabwawa, hawa wanatoka kule Bwawa liliiko la Mtera, linalotoa umeme kule, karibuni sana. (*Makofi*)

Pale Bwawani ndiyo kuna Mpaka wa Wilaya ya Mpwapwa na ukivuka Bwawa ndiyo unaingia kwa Mheshimiwa Lukuvi sasa, kwa maana ya Majimbo, karibuni sana watoto kutoka Mtera. Wageni 28 wa Mheshimiwa Edwin Ngonyani ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Namtumbo, wakiongozwa na Mussa Ngonji, wale wa Namtumbo, ehhehe! Yaani Galery nzima hapa leo Songea, hongereni sana, hongereni sana kutoka Namtumbo, wasomi hawa wapo Chuo Kikuu.

Lakini pia wako wageni 28 wa Mheshimiwa George Lubeleje ambao ni Waheshimiwa Madiwani pamoja na Viongozi wa CCM kutoka Mpwapwa, ehhe, karibuni sana, karibuni sana wale wa Mpwapwa jirani zetu, Mheshimiwa Lubeleje yupo kule Mpwapwa anaitwa Muaha, kwa hiyo Muaha yupo jamani, yaani Mkuu, siyo Mpwapwa peke yake Kongwa na Mpwapwa Muaha ni mmoja tu Mheshimiwa Lubeleje, basi. (*Makofi*)

Mwisho, Wageni wawili kutoka Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Dodoma ambao ni Ndugu Michael Semindu na Ndugu Neema Nyalege karibuni sana.

Sio mwisho kwa umuhimu, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mbunge wa Musoma Mjini ananiambia kwamba Timu ya *Biasara United* ya Mkoa wa Mara ambayo imebakia kwenye ligi kuu wako hapa, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Selemani Mataso na Diwani Frank Wabare pamoja na Amri Said, wale wa kutoka Musoma United karibuni sana, sana, karibuni sana na hongereni sana kubakia kwenye ligi kuu. Ahsante karibuni sana, karibuni sana kutoka kule Musoma, (*Makof*)

Lakini yuko Balozi wetu wa Msumbiji, Balozi wa Msumbiji karibu sana Mheshimiwa Monica Clemente Mousa karibu sana, karibu sana Bungeni, karibu sana Mheshimiwa Balozi wa Msumbiji. Basi baada ya matangazo hayo kwa kuwa sasa tunaelekea kwenye hatua nyingine, na mimi nina majukumu mengine ya kufanya hapo Ofisini basi nimuite Mheshimiwa Naibu Spika ili aweze kuja kuendelea na ratiba iliyoko hapa mezani.

Hapa Naibu Spika (Mhe. Dkt. Ackson Tulia) Alikalia Kiti

NAIBU SPIKA: Katibu!

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nimuite sasa Waziri wa Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo katika Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na

Usalama yaani (NUU) naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, naomba Bunge lako tukufu lijadili na kupitisha Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim, mwingi wa Rehema kwa kuniruzuku uhai na kunijalia afya njema kuweza kusimama mbele ya Bunge lako tukufu kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Kwa heshima na taadhima, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunitfea kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais ameonesha imani kubwa kwangu kwa kunipatia majukumu haya. Napenda kumuahidi Mheshimiwa Rais kuwa nitatumia nguvu zangu zote, akili yangu, uzoefu wangu kuhakikisha Wizara hii inatoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi yetu na kuhakikisha watumishi walio ndani ya Wizara wanakuwa wabunifu, wanajituma na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa miongozo na maelekezo anayonipatia mimi binafsi na viongozi wenzangu wa Wizara ambayo inachangia kwa kiasi kikubwa katika ufanisi wa Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kumsadia Mheshimiwa Rais kuiongoza vema nchi yetu na kutekeleza kwa mafanikio makubwa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015. Chini ya uongozi wao nchi yetu imeendelea kuwa ya amani na tumeendelea kudumisha

mshikamano wa kitaifa na kuendelea kuongeza ushawishi wa Tanzania katika nyanja za kikanda na kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Aidha, nakupongeza Mheshimiwa Naibu Spika Dkt. Tulia Ackson Mwansasu, Mbunge, Wenyeviti wa Bunge na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kazi nzuri wanazozifanya kusaidia kusimamia na kuendesha shughuli za Bunge. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia afya njema na hekima katika kuongoza mhimili huu muhimu katika uongozi wa Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu walionitangulia kuwashukuru na kuwapongeza watoa hoja waliozungumza kabla yangu hususani Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye katika hotuba yake siyo tu ameelezea mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Tano, bali pia ametoa dira na mstakabali wa taifa letu kwa kuainisha masuala muhimu ya kitaifa, kikanda na kimataifa ambayo yanagusa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge kwa ushirikiano inayotoa kwa Wizara. Nashukuru Kamati kwa miongozo na ushauri wake katika masuala mbalimbali ambayo imekuwa na mchango mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa na kuteuliwa katika kipindi cha mwaka huu wa fedha wa 2018/2019. Kuchaguliwa na kuteuliwa kwao ni kielelezo cha kuaminipa na wananchi na Serikali. Kwa namna ya pekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Damas Daniel Ndumbaro, Mbunge na Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Dkt. Faraji Kasidi Mnyepe, Katibu Mkuu;

Balozi Ramadhani Muombwa Mwinyi, Naibu Katibu Mkuu; Mabalozi wa Tanzania nje ya nchi, Wakuu wa Idara na Vitengo, Watumishi wa Wizara na Taasisi wa chini ya Wizara kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu. Nawashukuru kwa kujituma na kufanya kazi kwa weledi na kufanikisha kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na kuandaa bajeti ya Wizara ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila endapo sitamshukuru kwa dhati kabisa mke wangu mpendwa Dkt. Amina Mwaigwisya Kabudi na familia yangu kwa ujumla kwa kunivumilia, kuniunga mkono na zaidi kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niweze kutekeleza majukumu niliyopewa na Mheshimiwa Rais ya kujenga na kutetea maslahi ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2018/2019 Taifa letu lilikumbwa na maafa kutohana na ajali ya vyombo vya majini na nchi kavu. Itakumbukwa kuwa tarehe 20 Septemba, 2018 Taifa lilizizima kwa majonzi makubwa baada ya kupoteza takribani watu 200 katika ajali mbaya ya kuzama kwa kivuko cha MV Nyerere iliyotokea katika Ziwa Victoria. Naomba niungane na Mawaziri wenzangu walionitangulia kutoa salaam za pole kwa Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwa msiba huo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nifikishe salaam za rambirambi kwa Bunge lako tukufu kutoka Balozi za nchi za nje na mashirika mbalimbali ya kimataifa yaliyo hapa nchi nchini. Mwenyezi Mungu awajalie afya njema waliopata majeraha na azipumzishe roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa ndugu zetu wa Malawi, Msumbiji na Zimbabwe waliokumbwa na maafa ya kimbunga Idai na kimbunga Kenneth. Kwa namna ya pekee kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa

niaba ya Watanzania aliguswa na maafa hayo na kuchukua hatua za haraka kuzisaidia nchi hizo kwa kuzipatia misaada ya chakula, dawa, vifaa tiba, vyandarua na magodoro. Aidha, nachukua fursa hii kuwapa pole majirani zetu wa Comoro ambaao nao walikumbwa na kimbunga Keneth ambacho kilisababisha maafa makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali natoa pole kwa Serikali kwa nchi zilizokumbwa na mashambulizi ya kigaidi hivi karibuni, ikiwemo mashambulizi ya kigaidi liliotokea nchini Kenya mwezi Februari, 2019 katika Hoteli ya Dusit D2 Jijini Nairobi na kusababisha vifo vya watu 15. Shambulizi la kigaidi nchini New Zealand mwezi Machi, 2019 liliosababisha vifo vya watu takribani watu 50 na shambulizi la kigaidi liliotokea nchini Sri Lanka mwezi Aprili, 2019 katika maeneo ya ibada na hoteli na kusababisha vifo vya zaidi ya watu 300. Tanzania inaungana na mataifa mengine duniani kukemea na kulaani kwa vikali vitendo hivyo vya kikatili dhidi ya binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya hali ya dunia kwa mwaka 2018/2019; taarifa za hali ya uchumi duniani zilizotolewa na Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa zinaashiria kuwa katika miaka miwili mfululizo iliyopita uchumi wa dunia umeimarika na kuonesha matarajio ya kukua kwa zaidi ya mwaka 2019.

Aidha, uchumi wa nchi za Afrika Mashariki umekuwa kwa kasi zaidi ikilinganishwa na kanda nyininge ndani ya Afrika. Uchumi wa Tanzania umekuwa kwa wastani wa 7% na kufanya kuwa mionganoni mwa nchi tano ambazo uchumi wake unakuwa kwa kasi zaidi Barani Afrika. Pamoja na ukuaji huo wa uchumi, kuna dalili za kuwepo kwa vihatarishi vinavyoweza kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia na kuzorotesha kasi ya maendeleo hususan katika nchi zinazoendelea endapo hatua madhubuti za kisera hazitachukuliwa. Mionganoni mwa vihatarishi hivyo ni ongezeko la hali ya kutotabirika kwa sera za kibiashara za baadhi ya mataifa makubwa, mwenendo hafifu wa sekta ya fedha duniani na ukuaji wa madeni kwa nchi zinazoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya siasa, ulinzi na usalama kwa Bara la Afrika; naomba kutumia nafasi hii kuzipongeza nchi za Cameroon, Comoro, Guinea-Bissau, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Madagascar, Mali, Nigeria, Senegal, Zimbabwe, Afrika Kusini na Malawi kwa kufanya changuzi katika hali ya amani na utulivu. Hali hii inaashiria kuimarika kwa misingi ya demokrasia na utawala bora katika Bara letu la Afrika. Aidha, pamoja na hali ya kisiasa Barani Afrika kuwa ya kuridhisha, kumekuwepo na changamoto katika baadhi ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni Algeria ilikumbwa na maandamano ya kisiasa yaliyosababisha aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Mheshimiwa Abdelaziz Bouteflika kijiuzulu mnamo tarehe 2 Aprili, 2019. Kwa sasa nchi hiyo inaongozwa na Serikali ya Mpito itakayodumu kwa siku 90 kabla ya uchaguzi mkuu unaopangwa kufanyika mwezi Julai, 2019. Nitumie fursa hii kuwatachia ndugu zetu wa Algeria maandalizi mema ya uchaguzi ujao. Ni matumaini yetu kwamba uchaguzi huo utafanyika kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Burundi napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba hali ya siasa, ulinzi na usalama nchini Burundi inaimarika. Kuwepo kwa hali ya utulivu nchini humo kumewezesha raia wa nchi hiyo waliokuwa wakipata hifadhi hapa nchini kurejea nchini mwao kwa hiari. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu kati ya wakimbizi 239,164 waliokuwepo nchini wakimbizi 65,617 walirejea nchini Burundi kwa hiari. Jumuiya ya Afrika Mashariki inaendelea kuratibu mazungumzo kati ya Serikali ya Burundi na viongozi wa upinzani ili kupatikana kwa suluhisho la kudumu katika mgogoro huo. Kwa upande wetu Tanzania inaunga mkono juhudhi hizo ambazo tunaamini zinaweka mazingira mazuri kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika mwaka 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, baada ya uchaguzi mkuu uliofanyika tarehe 30 Desemba, 2018, hali ya kisiasa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo imeendelea kuwa tulivu. Rais wa nchi hiyo, Mheshimiwa Felix Antonie Tshisekedi anaendelea na

mchakato wa kuunda Serikali yake ambapo amemteua Mheshimiwa Profesa Sylvestre Ilunga Ilunkamba kuwa Waziri Mkuu. Pamoja na nchi hiyo inakabiliwa na changamoto za kiusalama katika maeneo ya mashariki, hivi karibuni kumeshuhudiwa kupungua kwa vitendo vya uvamizi vinavyofanywa na kikundi cha waasi cha *ADF* dhidi ya raia, askari wa jeshi la nchi hiyo na vikosi vya kulinda amani vya *MONUSCO*.

Aidha, baadhi ya wafuasi wa makundi yenye silaha katika Majimbo ya Kasai walijisalimisha na kuunga mkono Serikali mpya chini ya Rais Tshisekedi. Mbali na changamoto za kiusalama, nchi hiyo imekumbwa na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola katika maeneo ya Beni, Butembo na Ituri uliosababisha zoezi la uchaguzi kuahirishwa katika maeneo hayo. Uchaguzi katika maeneo hayo ulifanyika mwezi Machi, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Afrika ya Kati huko juhudzi za kuirejesha amani ya kudumu katika Jamhuri ya Afrika ya Kati zinaendelea chini ya usimamizi wa Umoja wa Afrika. Katika kufanikisha jitihada hizo, mwezi Februari, 2019 Serikali ya Jamhuri ya Afrika ya Kati na viongozi wa makundi 14 ya waasi nchini humo walifikia makubaliano ya amani. Miongoni mwa masuala muhimu yaliyokubaliwa ni pamoja na kuvunja makundi yenye silaha na kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kuanzisha mfuko wa kusaidla wananchi walioathirika na mapigano na kuunda Kamisheni ya Kitaifa ya Ukweli, Haki, Fidia na Maridhiano itakayotoa mapendekezo ya hatua za kuchukua ili kulinda haki za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya amani na usalama nchini Libya inaendelea kuwa ya wasiwasi tangu Kanali Muammar Gaddafi aliyekuwa kiongozi wa Libya alipoondolewa madarakani na kuuawa mwaka 2011. Hali hiyo imesababishwa na Serikali ya Mpito ya Libya kukosa udhibiti wa nchi, kuongezeka kwa makundi yanayokinanza, kuongezeka kwa vikundi vya wahalifu wanaojihusisha na biashara haramu za mafuta, binadamu na dawa za kulevyo

na kuchelewa kufanyika kwa mazungumzo ya amani. Hivi sasa mapigano yanaendelea nchini humo kati ya vikosi vya Serikali ya Mpito na vikosi vya Jenerali Khalifa Haftar.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa kwa kushirikiana na wadau wa ndani nchini Libya wanaendelea na uratibu wa majadiliano yatakayowezesha kufanyika uchaguzi wa kidemokrasia baadaye mwaka huu. Tanzania inaunga mkono juhudhi hizo ili kupata suluhisho la kudumu la mgogoro huo wa Libya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Sudan; mwezi Aprili, 2019 Jeshi la Sudan lilitangaza kumuondoa madarakani aliyekuwa Rais wa nchi hiyo, Jenerali Omar Al-Bashir kufuatia maandamano ya wananchi dhidi ya Serikali yaliyoanza mwezi Desemba, 2018. Jeshi lilitangaza kuundwa kwa Serikali ya Mpito ambayo itakuwa madarakani kwa kipindi cha miaka miwili. Tanzania itaendelea kuunga mkono jitihada za Jumuiya ya Kimataifa na wadau wengine wa amani ili kurejesha amani na utulivu nchini humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia makubaliano ya amani kati ya Serikali ya Sudan Kusini na wapinzani yaliyofikiwa Jijini Khartoum, Sudan mwezi Septemba, 2018 chini ya usuluhishi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Pembe ya Afrika (*IGAD*), pande zote mbili zinaendelea na utekelezaji wa makubaliano hayo ikiwemo kuunda Serikali ya Mpito itakayodumu kwa kipindi cha miaka mitatu. Tanzania inazisihi pande zinazokinzana kusimamia na kutekeleza makubaliano yaliyofikiwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya amani na usalama katika eneo la Mashariki ya Kati limeendelea kuimarika licha ya changamoto katika baadhi ya nchi ikiwemo masuala ya ugaidi na uhasama kati ya nchi na nchi. Hali ya kisiasa na kiusalama nchini Syria imeendelea kuwa ya wasiwasi licha ya Serikali ya nchi hiyo kuanza kudhibiti maeneo mengi ya nchi. Majeshi ya Syria yanaendelea na mapigano ya

kukomboa maeneo yanayoendelea kukaliwa na vikundi nya kigaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya usalama nchini Yemen imeendelea kuwa tete kutokana na mapigano yanayoendelea kati ya Majeshi ya Serikali na waasi wa Houthi. Mapigano hayo yamesababisha vifo nya raia wasio na hatia na kusababisha baa la njaa kutokana na kufungwa kwa bandari inayotumika kupidisha misaada ya kibinadamu. Juhudi za usuluhishi wa mgogoro huo kupidita Jumuiya ya Kimataifa zinaendelea na Tanzania inazisihi pande zinazopingana kutafuta suluhi ya kudumu kwa njia ya amani kupidita mazungumzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Amerika ya Kusini hivi karibuni Venezuela iliingia katika mgogoro wa kisiasa kufuatia maandamano ya wapinzani kumshinkiza Rais Nicolas Maduro Moros kuachia madaraka. Hii ilitokana na madai ya upinzani kuwa uchaguzi uliofanyika mwezi Mei, 2018 na matokeo yake yaliyompa ushindi Rais Nicolas Maduro haukuwa halali. Spika wa Bunge la nchi hiyo Bwana Juan Guaido alijitangaza kuwa Rais wa mpito wa nchi hiyo, akiungwa mkono na mataifa ya Magharibi. Tanzania inaamini kuwa mgogoro huu unaweza kupatiwa ufumbuzi kupidita njia ya majadiliano kati ya pande hizo mbili zinazokinzana. Hii itasaidia kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza nchini humo, hivyo tutaendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa kushawishi urejeshwaji wa amani na utulivu nchini humo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ulaya; Serikali ya Uingereza ilitangaza kujitoa katika Umoja wa Ulaya mwezi Juni, 2016. Hadi sasa kumekuwepo na majadiliano yanayoendelea kuhusu uamuzi huo wa Uingereza maarufu kama *BREXIT*. Wizara inaendelea kulifuatilia suala hili kwa ukaribu kutokana na Uingereza na Umoja wa Ulaya kuwa washirika wetu wakubwa wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafasi ya Tanzania Kimataifa; Tanzania inaheshimika kimataifa kutokana na mchango wake mkubwa katika masuala mbalimbali duniani

ikiwa ni pamoja na kudumisha ulinzi na usalama, kupambana na rushwa na mapambano dhidi ya biashara haramu, dawa za kulevyta, kukabiliana na tatizo la utakatishaji fedha, kutetea maslahi ya haki za binadamu na kuunga mkono misingi ya demokrasia na utawala bora. Tanzania inashiriki kikamilifu katika kulinda amani duniani ambapo kwa nyakati tofauti imekuwa ikichangia vikosi katika misheni mbalimbali za kulinda amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Tanzania inachangia walinda amani 2,687 katika misheni sita tofauti ambazo ni *MONUSCO* - Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, *MINUSCA* – Jamhuri ya Afrika ya Kati, *UNAMID* – Jamhuri ya Sudan, *UNIFIL* – Lebanon, *UNISFA* na *UNMISS* – Sudan Kusini. Napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa tarehe 16 Mei, 2019 kwa kutumia ndege ya Shirika la Ndege la Tanzania (*ATCL*), jumla ya wanajeshi 217 wallondoka nchini kwenda kushiriki ulinzi wa amani Darfur, Sudan. Ushiriki wa Tanzania katika kulinda amani duniani umetoa mchango mkubwa katika kuwalinda raia wa maeneo husika wanaokumbwa na madhila ya vita pamoja na kurejesha amani katika maeneo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza askari wetu na kuwapa moyo kuendelea na majukumu hayo ya kizalendo. Vilevile natoa pole kwa familia zillizopoteza wapendwa wao na Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kupoteza askari wake shupavu wakati wanatekeleza wajibu wao katika *operation* za kulinda amani kwenye Misheni ya Umoja wa Mataifa nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*MONUSCO*) na Misheni ya Kulinda Amani ya Umoja wa Mataifa Jamhuri ya Afrika ya Kati (*MINUSCA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kutoa salamu za pole, napenda kiliarifu Bunge lako tukufu kuwa Bwana Jean – Pierre Lacroix, Mjumbe Maalum wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika masuala ya kulinda amani, alifanya ziara mwezi Desemba, 2018 hapa nchini kwa ajili ya

kuwasilisha salaam za pole kwa Serikali na familia za askari waliouawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeandaa, imeshiriki na kuratibu ushiriki wa Serikali katika vikao mbalimbali nya kikanda na kimataifa. Ushiriki wa Serikali katika vikao hivi unalenga kuimarisha mahusiano yetu kimataifa, kulinda na kutetea maslahi na sifa nzuri ya Tanzania kwa kuieleza Jumuiya ya Kimataifa jitihada ambazo Serikali imefanya katika kuhakikisha maendeleo ya wananchi wake yanapatikana na masuala ya utawala bora na haki za binadamu yanalindwa kwa wananchi wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi, 2019 Tanzania ilishiriki kikamilifu katika Kikao cha 40 cha Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Mataifa huko Geneva, Uswis na kutumia fursa hiyo kutoa ufanuzi wa kina kuhusu tuhuma za upotoshaji unaofanywa mara kwa mara kuwa kuna ukiukwaji wa haki za binadamu nchini. Tanzania illiarifu Jumuiya ya Kimataifa jinsi Serikali inavyotimiza misingi ya haki za binadamu kama ilivyobainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Tanzania ni mwanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutaendelea kuhakikisha kuwa taswira ya nchi yetu inalindwa kila mahali na pale ambapo shutuma dhidi ya nchi yetu zinatolewa hatutasita kuzitolea ufanuzi. Niendelee kuzisihi jumuiya ya kimataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali kushauriana na Serikali pale ambapo wanahisi kuna tatizo kabla ya kutoa shutuma dhidi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgogoro wa Israel na Palestina, msimamo wa Tanzania ni kuendelea kuzingatia misingi tulioachiwa na waasisi wa taifa letu na hasa Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambayo ndiyo nguzo ya sera yetu ya mambo ya nje ya kupigania haki ya kujitawala wenyewe, kuheshimu mipaka ya nchi na kuunga mkono maazimio ya Jumuiya ya Kimataifa. Hivyo, Tanzania inaunga mkono maazimio ya Umoja wa Mataifa na Umoja

wa Afrika kuhusu mgogoro huu ambapo itaendelea kushauri pande husika kuheshimu makubaliano yaliyofikiwa. Tanzania inaamini kwamba suluhisho la kudumu katika mgogoro huu ni la kuwa na nchi mbili ambazo zitaishi pamoja ikiwa ni Palestina huru na Israel salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mgogoro kati ya Morocco na Sahrawi kwenye eneo la Sahara Magharibi; Tanzania inaunga mkono juhudzi za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika katika usuluhihi wa mgogoro wa eneo la Sahara Magharibi kati ya Morocco na Sahrawi kwa kushiriki katika mijadala na mazungumzo kuhusu namna bora ya kutatua mgogoro huo. Katika mijadala hiyo, tumeendelea kuzisihii pande zinazokinzana kukaa kwenye meza ya mazungumzo ili kupata suluhu ya kudumu ya suala hili kwa njia ya amani. Tunapongeza mazungumzo yaliyofanyika mwezi Desemba, 2018 Geneva, Uswis kati ya pande mbili, ni matumaini yetu kuwa suluhu ya mgogoro huo itapatikana mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2018/2019; katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2018/2019, Wizara ilitengewa kiasi cha shilingi 180,927,265,043.65 kati ya fedha hizo, shilingi 170,527,265,045.65 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 10,400,000,000 ni kwa ajili ya bajeti ya maendeleo. Katika fedha zilizotengwa kwa matumizi ya kawaida, shilingi 158,682,176,563.65 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 11,845,088,480 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2018/2019 Wizara ilitarajia kukusanya maduhuli kiasi cha shilingi 28,564,158,100. Hadi kufikia mwezi Aprili, mwaka huu 2019 Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 21,339,394,423.16 ikiwa ni sawa na asilimia 74.7 ya makisio ya makusanyo yote ya maduhuli kwa mwaka 2018/2019. Mwenendo huu unatoa matumaini kuwa Wizara itafikia malengo yake ya kukusanya maduhuli yaliyokadiriwa kwa mwaka 2018/2019 na kuingizwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali kama ilivyoelekezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019, Wizara ilipokea kutoka Hazina mgao wa fedha kiasi cha shilingi 116,334,246,179.70 sawa na asilimia 64.3 ya fedha za bajeti iliyoindhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo, shilingi 108,310,011,974.70 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 8,028,234,205 ni kwa ajili ya mishahara. Wizara inatarajia kupokea fedha za bajeti ya maendeleo kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo ya fedha za umma katika kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara pamoja na Balozi zake 40 kati 41 zilizokaguliwa zimepata hati safi za ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubalozi wa Tanzania Lusaka Zambia ndiyo pekee uliyopata hati yenyeye mashaka. Nachukua fursa hii kuwashukuru Watendaji wa Wizara na kuwashimiza waendelee kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya matumizi ya fedha za Umma na ununuzi wakati wote wanapotekeliza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2018/2019 naomba sasa nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi baadhi ya mafanikio ya Wizara katiak kipindi hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara unaongozwa na Sera ya Mambo ya Nje, Dira ya Taifa ya Maendeleo, Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miaka Mitano, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, Mpango wa Maendeleo Endelevu wa Mwaka 2030, Mkakati wa Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na itifaki zake, Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na itifaki zake pamoja na mikataba mingine ya kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Maendeleo wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, Mpango Mkakati wa pili wa Asasi ya Ushirikiano katika Siasa, Ulinzi na Usalama na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, maoni na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili mpango wa bajeti ya Wizara kwa kipindi cha mwaka 2018/2019, Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 hadi 2021/2022 na maagizo mbalimbali yaliyotolewa kwa nyakati tofauti na Wizara na viongozi wa Kitaifa, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia miongozo hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ilijiwekea malengo mbalimbali ambayo yametekelezwa. Moja ni kulinda na kutetea misingi ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inaongozwa na misingi ambayo lengo lake kuu ni kudumisha amani, ulinzi, usalama na mshikamano wa wananchi wake na Taifa kwa ujumla kama ilivyowekwa na waasisi wa Taifa letu mara baada ya uhuru. Katika kutekeleza hilo, Tanzania imeendelea kulinda uhuru wetu, kujamulia mambo yetu wenyewe bila kuingiliwa, kulinda mipaka ya nchi yetu, kulinda haki, kuimarisha ujjirani mwema na kuunga mkono sera ya kutofungamana na upande wowote kama dira na msimamo wetu katika mahusiano na nchi nyingine katika Jumuiya ya Kimataifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, misingi hiyo ndiyo inayotufanya tujivunie kuwa Taifa lenye amani, ulinzi imara na usalama duniani, kuwa mstari wa mbele kutetea wanyonge, haki na uhuru, kutafuta amani na kutatua migogoro ya nchi mbalimbali na kuwa nchi kimbilio kwa wananchi wa Mataifa mengine. Aidha, Tanzania inaheshimu misingi ya mahusiano na Mataifa mengine Duniani. Kwa muktadha huo, tunatarajia Mataifa mengine kuheshimu uhuru wa nchi yetu na kutotuingia katika mambo yetu ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo kuhusu namna Wizara ilivyolinda na kutetea misingi ya Taifa ndani na nje ya nchi yanapatikana katika ukurasa wa 17 na 18 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kudumisha ujirani mwema na nchi zote zinazopakana na nchi yetu katika kuratibu na kusimamia masuala ya uhusiano wa ushirikiano na nchi hizo. Wizara iliratibu na kushiriki mikutano wa ujirani mwema kati ya Mkoa wa Rukwa na Jimbo la Kaskazini mwa Zambia uliofanyika Mjini Sumbawanga mwezi Julai, 2018.

Aidha, Wizara iliratibu na kushiriki mikutano inayohusu biashara na utatuza wa changamoto mipakani kati ya Tanzania na nchi za Kenya na Uganda iliyofanyika katika miezi ya Novemba, 18 na Februari na Aprili, 2019 kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi changamoto za mipakani ili kuimarisha mwingiliano wa biashara, ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje na kuhakikisha tunakuza na kutekeleza kwa vitendo diplomasia ya uchumi, Wizara na Balozi za Tanzania nje ya nchi zinashirikiana na Wizara za Kisekta, Taasisi za Serikali na Sekta Binafsi pamoja na Asasi za kiraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufanikisha hilo, Wizara imevutia wawekezaji katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo viwanda, miundombinu, usafirishaji, nishati, afya na kilimo, kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi, kuvutia watalii kuja kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo nchini, kushiriki katika mazungumzo na mashirika ya Kimataifa na nchi marafiki ili pamoja na mambo mengine kupata mikopo yene masharti nafuu na ufadhilli wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kutafuta fursa za ajira na mafunzo kwa Watanzania nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza hilo, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kufanikisha uwekezaji wa kiwanda cha kuzalisha unga wa muhogo kinachoitwa *Cassava Starch of Tanzania Corporation (CSTC)*

kilichopo Mkoani Lindi chenye uwezo wa kuzalisha tani 6,000 kwa mwaka. Maelezo hayo yamo kwenye aya ya 52 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumefanikisha uwekaji sahihi wa mkataba kati ya Tanzania na Jamhuri ya Korea wa ujenzi wa daraja jipya la Selander Jijini Dar es Salaam lenye urefu wa kilometra 1.03 utakaogharimu dola za Kimarekani milioni 126.26, rejea aya ya 56 ya kitabu cha hotuba; kufanikisha uwekaji sahihi mkataba kati ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Korea wa ukarabati wa meli mbili za ujenzi wa meli mpya za kisasa katika Ziwa Victoria, aya ya 57 ya kitabu cha hotuba; kufanikisha uwekaji sahihi kati ya Tanzania na Japan ya ujenzi wa daraja la gerezani Jijini Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 20.4 na upanuzi wa barabara ya Morocco, Mwenge Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi billioni 74. Rejea aya ya 58 ya kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kufanikisha upatikanaji wa nafasi 100 za ufadhilli wa masomo kwa vijana wa Kitanzania kwenda kujifunza kilimo cha kisasa nchini Israel. Mafunzo hayo yatachukua miezi 11 kuanzia mwezi Septemba 2019 mpaka mwaka wa masomo wa 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kufanikisha uwekaji sahihi mkataba kati ya Tanzania kupitia Shirika la Ugavi la Umeme (*TANESCO*) na kampuni za Arab *Contractors* na *El Sewedy Electric* za Misri kuhusu ujenzi wa mradi wa uzalishaji umeme wa *Megawatt* 2115 katika Bonde la Rufiji. Uwekaji wa sahihi wa mkataba huo ulifanyika wakati wa ziara ya Mheshimiwa Dkt. Mostafa Madbouly Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri iliyo fanyika hapa nchini mwezi Desemba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Ubalozi wetu wa China iliratibu na kuwezesha Tanzania kusaini hati ya makubaliano (*MOU*) na kampuni ya *Touch Road International Holding Group (TIHG)* mwezi Novemba, 2018. Kufuatia makubaliano hayo, kampuni hiyo itasafirisha watalii takriban

10,000 kutoka Jiji la Shanghai nchini China kutembelea vivutio vya kitalii vilivyopo nchini kwa mwaka 2019, ambapo kundi la kwanza la watalii 330 liliwasili nchini tarehe 14 Mei, 2019 na kupokelewa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge) Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kuptitia Ubalozi wetu Israel ilifanikisha ziara ya kundi la watalii 1,000 kutoka nchini humo walikuja kutembelea vivutio vya utalii vilivyoko hapa nchini mwezi Aprili, 2019 na kupokelewa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imejizatiti kuhakikisha kuwa Balozi za Tanzania nje ya nchi zinashirikiana na wadau wote wa utalii ndani na nje ya nchi kuratibu na kushirikiana katika kuvutia watalii kutoka pande zote za dunia kuja na kutembelea vivutio vya utalii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ninapenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mabalozi wa Tanzania katika nchi za China, Malaysia na Israel kwa jitihada zao za kuratibu na kufanikisha ziara za watalii hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee naomba pia nimshukuru Mheshimiwa kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutenga muda wake kuwalaki watalii hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina ya namna Wizara inavyotekeleza diplomasia ya uchumi inapatikana kuanzia ukurasa wa 18 hadi wa 29 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuratibu na kushiriki Tume za Pamoja za Kudumu na za Ushirikiano. Tume za pamoja za kudumu (*JPC*) ni nyenzo muhimu za kuanzisha na kuendeleza ushirikiano kati ya nchi yetu na nchi nyingine katika nyanja mbalimbali. Tume hizi huainisha maeneo

mbalimbali tunayokubaliana, kushirikiana kulingana na uhitaji wa masuala ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa *JPC* ni msingi unaorahisisha nchi zilizokubaliana kuingia makubaliano katika nyanja husika. *JPC* inatoa mwongozo wa ushirikiano baina ya nchi ya nchi. Kwa kuzingatia umuhimu wa *JPC*, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Kudumu ya Ushirikiano kati ya Tanzania na Uganda uliofanyika mwezi Agosti 18 Jijini Kampala.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkutano huo, mambo yaliyokubaliwa kwa haraka ni pamoja na kuanza zoezi la kuhakiki mpaka, kuharakisha utekelezaji wa zoezi la kutoa fidia ya ardhii kwa wananchi ambaao maeneo yao yatapitiwa na mradi wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Holma nchini Uganda hadi Chongoleani Tanga nchini Tanzania, kuanza kufanya kazi kwa masaa 24 kwa kituo cha pamoja cha kutoa huduma mpakani cha Mutukula, kuchukua hatua za kuimarisha biashara na kutatua changamoto zinazojitokeza mpakani kupitia vikao vya mara kwa mara baina ya mamlaka zinazohusika na usimamizi wa maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mkutano huo nchi hizi zilisaini hati ya makubaliano ya kujenga bomba la kusafirisha gesi asilia kutoka Tanzania hadi Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Oktoba, 2018 Tanzania na India zilishiriki katika Mkutano wa Ttisa wa Tume ya Pamoja ya Kudumu uliofanyika Jijini New Delhi, India. Katika mkutano huo, Serikali ya Tanzania na India zilisaini hati ya makubaliano ya ushirikiano. Hizo ni: hati ya makubaliano kati ya Chuo cha Diplomasia cha Tanzania na Chuo cha Diplomasia cha India kuhusu kushirikiana, Hati ya Makubaliano kati ya Chuo cha Diplomasia nchini Tanzania na Taasisi ya Mafunzo ya Utafiti wa Habari ya India (*Research Information System of India*) na Hati ya Makubaliano kati ya Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda (*TIRDO*) na Shirika

la Taifa la Utafiti wa Maendeleo la India (*National Research Development Corporation of India*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kupertia mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano, Tanzania na nchi husika zilifanya tathmini ya ushirikiano katika sekta mbalimbali na kuainisha maeneo mapya ya ushirikiano. Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta katika kuhakikisha utekelezaji wa makubaliano hayo yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makubaliano ya kikanda na Kimataifa; Wizara iliratibu na kushiriki katika majukumu mbalimbali yanayohusiana na Umoja wa Mataifa Jumuiya za Kikanda, Mashirika na Taasisi za Kimataifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Umoja wa Mataifa. Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 73 wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa uliofanyika tarehe 28 Septemba, hadi 1 Oktoba, *New York*, Marekani. Katika mkutano huo Tanzania ilitoa ufanuzi kuhusu masuala mbalimbali ya ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na mapambano dhidi ya rushwa, kuimarisha ukusanyaji wa kodi, kusimamia haki za binadamu na misingi ya utawala bora, kuziba mianya ya ukwepajji kodi, kusimamia nidhamu kwenye Utumishi wa Umma, ushiriki wa Tanzania kwenye *mission* za ulinzi wa amani duniani na zoezi la kuwarudisha kwa hiari wakimbizi wa Burundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa mkutano huo, ujumbe wa Tanzania ulikutana na kufanya mazungumzo na Bwana Filippo Grandi Kamishna Mkuu wa Shirika la Wakimbizi Duniani. Kufuatia mazungumzo hayo, Bwana Grandi alifanya ziara hapa nchini mwezi Februari, 19 na kufanya mazungumzo na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo aliahidi kufuatilia upatikanaji wa fedha, kiasi cha dola za Marekani milioni 20 kutoka vyanzo mbalimbali ili kufadhili miradi ya utunzaji wa mazingira na nishati mbadala katika Mkoa wa Kigoma ulioathirika kutohana na kuwepo kwa Kambi za Wakimbizi kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, linguini ni masuala ya wakimbizi. Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Burundi, shirika la *UNHCR* pamoja na wadau wengine inaendelea na zoezi la kuwarejesha kwa hiari nchini mwao wakimbizi kutoka Burundi. Tangu kuanza kwa zoezi hilo mwezi Septemba, 2017 hadi Aprili, 2019 wakimbizi wapatao 65,617 walirejeshwa nchini kwao na wengine wapato 13,075 waliojiandikisha kwa hiari, wanasuburi kurejea.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kurudisha wakimbizi wa Burundi nchini kwao kwa hiari linafanyika kwa weledi mkubwa na kwa kuzingatia mikataba ya Kimataifa pamoja na sheria za nchi. Kwa hiyo, wanaodai kuwa ni Warundi waishio kwenye baadhi ya nchi za Ulaya, walioanzisha kampeni za kuibagaza nchi yetu kuwa inawalazimisha wakimbizi kureja nchini kwao; tuhuma hizo siyo za kweli na zina lengo la kulichafua Taifa letu Kimataifa. Hivyo, Wizara kwa kushirikiana na Balozi za Tanzania nje ilitumia majukwaa mbalimbali ya Kimataifa kutoa ufanuzi wa namna zoezi la kuwarudisha wakimbizi wa Burundi nchini mwao kwa hiari linavyofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wadau wa Kimataifa wanaotunga mkono, wamefanya ziara katika maeneo husika kukagua zoezi linaloendelea na wameridhika kuwa linafanywa kwa weledi mkubwa. Tanzania itaendelea kupokea na kuhifadhi wakimbizi pale inapokuwa ni lazima kwa kuzingatia sheria za nchi na mikataba ya kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wizara iliratibu na kushiriki kwenye ziara za viongozi mbalimbali wa Mashirika ya Kimataifa kuja hapa nchini kwa nyakati tofauti. Viongozi hao ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Mpango wa Chakula, Mkurugenzi wa Bodi ya Wakurugenzi Mkuu wa Mpango wa Chakula, Mkurugenzi wa Bodii ya Wakurugenzi wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, Mkurugenzi wa Shirika la Fedha la Kimataifa Idara ya Afrika, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia Kanda ya Afrika, Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika na Rais wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo. Kupitia

ziara hizo, nchi yetu imenufaika kwa kupata ufadhili wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla viongozi wote walisifia na kuipongeza juhudzi za Serikali ya Awamu ya Tano za kukuza uchumi na kuwaletea wananchi maendeleo. Aidha, waliahidi kuendelea kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu ushiriki wa Tanzania katika masuala ya Kimataifa yanapatikana kuanzia ukurasa wa 33 hadi 40 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ushirikiano wa kikanda, Wizara iliratibu na kushiriki katika majukumu mbalimbali yanayohusiana na Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Jumuiya ya Nchi Zinazopakana na Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishiriki mikutano mbalimbali ya Umoja wa Afrika ikiwa ni pamoja na Mkutano Maalum wa 11 wa Wakuu wa Nchi na Serikali za Umoja wa Afrika uliofanyika Addis Ababa Ethiopia mwezi Novemba, 2018. Mkutano huo ulipokea na kujadili taarifa kuhusu mapendekezo ya mabadiliko ya kitaasisi yenye lengo la kuleta ufanisi, uwajibikaji kuwezesha umoja huu kujitegemea kifedha na kuweka mgawanyo wa majukumu kati ya Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kikanda na taasisi zake. Tanzania inaunga mkono mchakato wa mabadiliko hayo ambayo tunaamini yatapunguza gharama za uendeshaji wa umoja huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Wizara iliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye Mkutano wa 32 wa Wakuu wa Nchi za Serikali wa Umoja wa Afrika uliofanyika mwezi Februari, 2019 Addis Ababa Ethiopia. Mkutano huo ulimchagua Mheshimiwa Abdel Fattah Al-Sisi Rais wa Jamhuri ya Kiarabu ya Misri kuwa Mwenyekiti wa AUkwa kipindi cha mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo furaha kualiarifu Bunge lako Tukufu kuwa wakati wa mkuatano huo, Tanzania ilipewa tuzo ya kuwa mliongoni mwa nchi za Afrika zilizopiga hatua katika mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, taarifa ya Kamati Maalum ya Umoja wa Afrika kuhusu mwenendo wa utoaji wa huduma za afya ilionesha kuwa nchi yetu imefanya vizuri katika utoaji wa huduma za afya kwa wananchi hususan katika kudhibiti magonjwa ya Malaria na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio haya yanatokana na juhudzi za Serikali ya Awamu ya Tano chini ya uongozi mdhubuti wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kupambana na rushwa na kuongeza bajeti kwenye Sekta ya Afya ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Afrika ujulikanao kama Ajenda 2063. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara imeratibu ushiriki wa Tanzania katika utekelezaji wa hatua za mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo ni Umoja wa Forodha, Soko la Pamoja, Umoja wa Fedha na Shirikisho la Afrika Mashariki. Katika hatua ya Umoja wa Forodha, Wizara imeratibu na kusimamia utekelezaji wa himaya moja ya forodha. Wizara vile vile umeratibu mapitio ya wigo wa pamoja wa ushuru wa forodha na kuratibu uondoaji wa vikwazo vyia biashara visivyo vyia kiforodha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya Soko la Pamoja, Tanzania imefanikiwa kutoa vyeti 5,953 vyia uasili wa bidhaa kwa wafanyabiashara wa Tanzania wanaofanya biashara katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2018. Vyeti hivyo vimewasaidia wafanyabiashara wetu kutotozwa ushuru wa forodha kama wanavyotozwa wafanyabiashara wengine ambaa nchi zao siyo wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwaomba Watanzania kuendelea kuchangamkia fursa zitokanazo na Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki katika maeneo ambayo tumefunguliana Milango. Kwa kufanya hivyo, kutaifanya nchi yetu kuendelea kufanikiwa ipasavyo na mtangamano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya Umoja wa Fedha, Wizara imeratibu uanzishwaji wa Taasisi za kusimamia Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo Muswada wa Sheria wa Kuanzisha Taasisi ya Fedha ya Afrika Mashariki ulisainiwa na Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Muswada wa Sheria ya kuanzisha Taasisi ya takwimu ya Afrika Mashariki ulipitishwa na Bunge la Afrika Mashariki na kuwasilishwa kwa nchi wanachama kwa ajili ya maandalizi ya kusainiwa kuwa sheria na maandalizi ya Muswada wa Sheria ya kuanzisha Tume ya Usimamizi na utekelezaji wa Umoja wa Fedha na Tume ya Huduma za Fedha ya Afrika Mashariki yanaendelea. Aidha, nchi wanachama zinaendelea kuainisha sheria, mifumo na taratibu za usimamizi wa Sekta ya Fedha ndani ya Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa miradi na programu za miundo ya kiuchumi na huduma za jamii ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wizara iliratibu utekelezaji wa miradi na programu za Jumuiya Afrika Mashariki za uendelezaji wa miundombinu ya kiuchumi na huduma za jamii katika Sekta za Afya, Barabara, Elimu, Sanaa na Utamaduni na vituo vya kutoa huduma kwa pamoja mpakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwa upande wa Sekta ya Elimu, Jumuiya iliendesha Mashindano ya Uandishi wa Insha kwa Vijana wa Shule za Sekondari ili kuimarisha uelewa wa vijana kuhusu mtangamano wa Afrika Mashariki. Kwa miaka miwili mfululizo, vijana wa Kitanzania wameibuka kuwa washindi katika Shindano la Uandishi wa Insha. Nachukua fursa hii kuwatambua na kuwapongeza

Michael Msafiri Nyarunga kutoka Shule ya Sekondari Kibaha na Innocent Shirima kutoka Shule ya Sekondari Moshi kwa kuibuka washindi wa kwanza katika Shindano la Uandishi wa Insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa mwaka 2018/2019 mtawalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile mwezi Novemba, 2018 Jumuiya iliendesha mdahalo wa wanafunzi wa vyuo uliofanyika katika Chuo cha Dar es Salaam. Katika mdahalo huo, Kombo Faki Juma kutoka Chuo cha Utumishi wa Umma Zanzibar na Juma Emmanuel Erassy kutoka Chuo cha Tumaini Makumira, Arusha waliibuka washindi. Nachukua fursa hii kuwapongeza kwa ushindi huo ambao umewawezesha kuwa mabalozi wa vijana kutoka Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Natoa wito kwa walimu, wahadiri, wazazi na walezi wa wanafunzi wetu kote nchini kuendelea kuhamasisha wanafunzi kushiriki katika mashindano hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirikisho la Kisiasa la Afrika Mashariki ndiyo hatua ya nne na ya mwisho ya mtangamano kwa mujibu wa Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kutekeleza hilo, nchi wanachama zimekubaliana kuanza na fungamano la kisiasa (*confederation*) la Afrika Mashariki kama hatua ya mpito kuelekea shirikisho la kisiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia makubaliano hayo, timu ya wataalam inayoundwa na wajumbe watatu kutoka kila nchi mwanachama imeanza mchakato wa kuanda rasimu ya katiba ya fungamano kama ilivyoagizwa kwenye mkutano wa 19 wa Wakuu wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Arusha mwezi Februari, 2019. Hatua hiyo itaanza kutekelezwa mara baada ya kuanzishwa kwa Umoja wa Fedha mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu namna Wizara ilivyoratibu na kusimamia masuala ya mtangamano wa Afrika Mashariki yanapatikana kuanzia ukurasa wa 42 hadi 51 katika kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu na kushiriki katika mikutano na majukumu mbalimbali ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ikiwa ni pamoja na Mkutano wa 38 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliofanyika mwezi Agosti, 2018 Windhoek, Namibia. Mkutano huo ulipitisha Jamhuri ya Namibia kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia mwezi Agosti, 2018 hadi Agosti, 2019 na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Makamu Mwenyekiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hatua hiyo, Tanzania itachukua nafasi ya Uenyekiti wa Jumuiya hiyo kuanzia mwezi Agosti, 2019 hadi Agosti, 2020. Kwa utaratibu wa SADC katika kipindi hicho, Tanzania itakuwa mwenyeji wa mikutano yote ya SADC ikiwemo Mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali, Vikao vya Baraza la Mawaziri na Mikutano ya Kisekta. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa SADC unatarajiwa kufanyika hapa nchini Tanzania mwezi Agosti, 2019. Kufanyika kwa mkutano huo mkubwa hapa nchini itakuwa ni neema kwa nchi yetu kwa kuwa utaongeza pato la wananchi na Taifa kwa ujumla kwa njia ya ushuru wa viwanja vya ndege, usafiri wa ndani, malazi, vyakula, vinywaji, mawasiliano na taasisi za fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kupitia Bunge lako Tukufu kutoa wito kwa wadau wote wakiwemo Waheshimiwa Wabunge, wafanyakishara na wananchi kwa ujumla kutumia fursa hii ili kunufaika na uenyeji wa mkutano huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kipindi hicho, Wizara iliratibu na kushiriki katika Mkutano wa 30 wa Kamati ya Mawaziri wa Biashara uliofanyika Pretoria, Afrika Kusini mwezi Julai, 2018, na Mkutano wa 19 wa Kikosi Kazi cha Mawaziri kuhusu Mtangamano wa Kiuchumi uliofanyika Pretoria, Afrika Kusini Julai, 2018. Wizara pia iliratibu ushiriki wa

Tanzania katika uangalizi wa chaguzi katika nchi wanachama za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Kufuatia dhamira na uamuzi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika Nyanja mbalimbali za kikanda na Kimataifa Wizara imeendelea na juhudi za kuhakikisha lugha hiyo inakuwa lugha rasmi kwenye Mikutano ya *SADC*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutimiza azma hiyo, Tanzania iliyasilisha pendekezo la kuingiza lugha ya Kiswahili kuwa moja ya lugha rasmi za *SADC* katika Mkutano wa Baraza la Mawaziri uliofanyika mwezi Machi 2019 *Windhoek*, Namibia. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tanzania itatumla vema nafasi ya Uenyekiti wa *SADC* kusukuma suala hili ili kuhakikisha lugha ya Kiswahili inakuwa moja ya lugha rasmi za Jumuiya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ziara ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nchini Afrika Kusini iliyofanyika tarehe 24 hadi 27 Mei mwaka huu, Serikali ya nchi hiyo imeahidi kuchukua Walimu wa Kiswahili nchini Tanzania ili watumike kufundisha somo la Kiswahili katika shule za msingi na sekondari nchini humo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kuwa, mwaka 2018, Bunge la Afrika Kusini lilipitisha azimio kuwa Somo la Kiswahili liingizwe kwenye mitaala ya kufundishia katika elimu ya msingi na sekondari nchini humo. Wizara inatoa wito kwa kwa Watanzania wenyе sifa kuchangamkia fursa hiyo adhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu namna Wizara ilivyoratibu na kusimamia masuala ya mtangamano wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

yanapatikana kuanzia ukurasa wa 51 hadi 55 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutafuta fursa mbalimbali zinazotokana na ushiriki wa Tanzania katika Mtangamano wa Kikanda na Mashirika ya Kimataifa. Wizara iliratibu na kufanikisha kuzishawishi Nchi Wanachama wa SADC kuipigia kura Bohari Kuu ya Dawa ya Tanzania kushinda zabuni ya kuwa mnunuzi na msambazaji mkuu wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vyta maabara kwa ajili ya Nchi Wanachama wa Jumuiya hiyo. Mwezi Oktoba, 2018 Tanzania kuititia Bohari Kuu ya Dawa ilisaini Mkataba na SADC wa kusambaza vifaa hivyo kwa Nchi Wanachama wa SADC kwa muda wa miaka mitano kuanzia mwezi Oktoba, 2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuhakikisha Watanzania wananzaika na fursa za ajira katika Mashirika ya Kimataifa, Tanzania imefanikiwa kuushawishi Umoja wa Afrika kumpitisha Dkt. Agnes Kijazi kuwa mgombea pekee wa Afrika katika nafasi ya Makamu wa Tatu wa Rais wa Shirika la Masuala ya Hali ya Hewa Duniani (WMO) katika uchaguzi unaotarajiwa kufanyika mwezi Juni, 2019 Geneva, Uswisi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu semina ya kuwajengea uwezo watanzania wa namna ya kupata ajira kwenye maeneo ya ulinzi wa amani ya Umoja wa Mataifa. Semina hiyo iliyotolewa na Umoja wa Mataifa ilifanyika mwezi Novemba, 2018 Jijini Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalihusisha washiriki kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania; Jeshi la Polisi; watumishi wa umma, sekta binafsi; na wanafunzi wa vyuo vikuu, Wizara inafanya jitihada kuhakikisha kuwa semina hii inakuwa endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kufuatilia na kutangaza fursa mbalimbali zinazopatikana kutokana na ushiriki wetu katika Jumuiya za Kikanda, Kimataifa na Mashirika ya Kimataifa. Maelezo ya kina kuhusu utafutaji wa fursa zinazotokana na ushiriki wa Tanzania kwenye Mtangamano wa Kikanda na Mashirika ya Kimataifa

yanapatikana katika ukurasa wa 56 na 57 wa kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kuongeza uwakilishi wa Tanzania nje ya nchi; katika kuhakikisha kuwa tunadumisha mahusiano na nchi mbalimbali duniani, Tanzania inaendelea kuainisha maeneo ambayo yatakuwa na manufaa kiuchumi ili kuweza kuongeza uwakilishi wetu katika maeneo hayo. Katika kufanikisha hayo, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu imefungua ubalozi mpya Jijini Havana, Cuba na Mheshimiwa Rais amemteua Mheshimiwa Valentino Mlowola kuwa Balozi wa Tanzania nchini humo ambaye amesharipoti katika kituo chake cha kazi. Aidha, Wizara inaendelea na taratibu za ufunguzi wa ubalozi mpya *Windhoek* nchini Namibia pamoja na Konseli Kuu katika Miji ya Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guangzhou, katika Jamhuri ya watu wa China. Kufunguliwa kwa ofisi hizi za uwakilishi kutaiwezesha nchi yetu kunufaika na fursa za uchumi zilizopo kwenye nchi hizo. Aidha, Wizara inaratibu ufunguzi wa Konseli Kuu ya Umoja wa Falme za Kiarabu hapa nchini ambayo ofisi yake itakuwa Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwakilishi wa Heshima; Wizara iliratibu maandalizi ya ufunguzi ofisi ya Uwakilishi wa Heshima wa Shirikisho la Jamhuri ya Brazil hapa nchini uliofunguliwa mwezi Oktoba, 2018, Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatilia utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa katika nchi yetu na nchi nyingine; katika kipindi cha mwaka 2018/2019, Wizara iliratibu na kushiriki majadiliano na uwekaji saini wa mikataba na makubaliano mbalimbali yenye manufaa kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu. Mikataba na hati hizo zinalenga kuimarishe ushirikiano uliopo katika Tanzania na nchi hizo. Aidha, Tanzania itanufaika na fursa hizo zilizopo katika maeneo yaliyoelezwa katika makubaliano hayo. Katika kuratibu hilo, Wizara imekuwa ikiwasiliana mara kwa mara na wadau wa sekta husika ili kupata mrejesho wa utekelezaji wa mikataba

na makubaliano mbalimbali. Orodha ya mikataba hiyo na hati za makubalino hayo ni kama inavyoonekana kwenye Kiambatisho Na.5 kilichopo kuanzia ukurasa wa 97 hadi 100 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuongeza mshikamano na Jumuiya za Watanzania Wanaoishi Nje ya Nchi na kuweka utaratibu madhubuti utakaowawezesha kuchangia kwenye maendeleo ya taifa. Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kutekeleza diplomasia ya uchumi kupitia uhamasishaji na ushirikishaji wa Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*Diaspora*) katika kuleta maendeleo nchini. Ushirikishwaji wa *Diaspora* unafanyika kupitia Balozi zetu nje ya nchi na kwa kushirikiana na wadau wengine ili kuhakikisha wanachangia uchumi wa Tanzania kwa kuwekeza katika sekta mbalimbali. Katika kutekeleza hilo, Wizara iliratibu na kushiriki katika makongamano ya *Diaspora* matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ushirikishwaji wa *Diaspora* katika kuchangia maendeleo ya nchi, baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na *Diaspora* kuchangamkia fursa za uwekezaji kwenye sekta ya nyumba nchini kupitia Shirika la Nyumba Tanzania (*NHC*) ambapo katika kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 *Diaspora* walinunua nyumba zenye thamani ya shilingi bilioni 2.53. Vilevile, *Diaspora* wameendelea kurudisha nchini sehemu ya kipato chao ambapo kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2018, Benki ya *CRDB* imepokea fedha zinazotumwa nyumbani na Watanzania wanaoishi nje ya nchi (*remittance*) kiasi cha Shillingi bilioni 2.8; Benki ya *Stanbic* imepokea Dola za Marekani mia tisa ishirini na moja elfu, mia sita ishirini na saba na senti kumi na sita, *Euro* elfu saba na hamsini, Paund za Uingereza 7,800 na Faranga za Usvisi elfu moja na hamsini. Kadhalika, Shirika la Hifadhi ya Jamii Tanzania limekusanya Dola za Marekani kumi na nane elfu kutoka kwa *Diaspora* 60 waliojiandikisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu namna Serikali inavyoshirikiana na Jumuiya za Watanzania

Wanaoishi Nje ya Nchi yanapatikana kuanzia ukurasa wa 59 hadi 61 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutafuta nafasi za masomo, misaada na kushawishi nchi na mashirika kutufutia madeni; Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa msaada kwa kiasi cha Shilingi bilioni 307.5 kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu, mapambano dhidi ya rushwa na uboreshaji wa huduma za afya katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2023 kutoka Serikali ya Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu uwekaji saini mkataba kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Jamhuri ya Korea wa mkopo wa Dola za Marekani milioni 50 kwa ajili ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliratibu na kufanikisha upatikanaji wa nafasi za ufadhilli wa masomo ya muda mfupi na mrefu kutoka nchi wahisani na marafiki za Algeria, Morocco, Misri, Sudan, Romania, Uingereza, Malta, China, Urusi, Jamhuri ya Korea, Thailand, Japan, Israel, Oman, Australia, India, Saudi Arabia, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ubelgiji, Uholanzi, Hungary, Ireland, Ujerumani, Pakistan, Sweden, Norway, Finland, Ufaransa, Poland, Indonesia, Singapore, Malaysia, Austria, Italia, New Zealand na Marekani katika fani mbalimbali. Nafasi hizi zimekuwa zikipelekwa katika Wizara na taasisi za kisekta hapa nchini pamoja na kutangazwa katika vyombo vya habari. Nichukue fursa hii kuwasihii Watanzania wenzangu kuchangamkia fursa hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya kina kuhusu utafutaji wa nafasi za masomo, misaada na ushawishi kwa nchi na mashirika ya kimataifa kutufutia madeni yanapatikana kuanzia ukurasa wa 61 hadi 63 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamia masuala yanayohusu kinga na haki za Wanadiplomasia waliopo nchini. Mkataba wa Vienna kuhusu Mahusiano ya Kidiplomasia wa mwaka 1961 na Mkataba wa Vienna kuhusu

Mahusiano ya Kikonseli wa mwaka 1963 unaipa nchi wajibu wa kuhakikisha Wanadiplomasia wanaowakilisha nchi zao na Mashirika ya Kimataifa hapa nchini, wanalindwa na kupata haki zao. Wizara kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali nchini inaendelea kutekeleza wajibu huo na kuhakikisha kuwa Wanadiplomasia wote hapa nchini wanaishi kwa usalama na amani ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Nichukue fursa hii kuwashukuru Wanadiplomasia wote nchini kwa ushirikiano wanaoendelea kuipa Wizara na mamlaka nyingine na niwaombe ushirikiano huu uendelee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamia na kuratibu masuala ya itifaki na uwakilishi; moja ya majukumu ya Wizara ni kuandaa na kuratibu ziara mbalimbali za kitaifa na kikazi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ndani na nje ya nchi kama ifuatavyo na hapa ningependa kuzitamka ziara za Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alifanya ziara ya kitaifa nchini Zimbabwe iliyofanyika tarehe 28 hadi leo tarehe 30 Mei, 2019; Ziara ya kitaifa ya nchini Namibia iliyofanyika tarehe 27 hadi 28 Mei, 2019; Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Rais nchini Afrika Kusini iliyofanyika tarehe 24 hadi 27 Mei, mwaka huu; Ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Malawi iliyofanyika mwezi Aprili 2019. Pia aya ya 166 mpaka 167 zinaonesha Ziara za Mheshimiwa Makamu wa Rais, ziara za Mheshimiwa Waziri Mkuu, Ziara za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na ziara za Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar. Pia Waheshimiwa Marais wastafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wametuwalishaa katika Mkutano mbalimbali kama ambavyo mmekuwa mnajulishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ziara hizo za viongozi wa kitaifa, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa nyakati tofauti walimwakilisha Mheshimiwa Rais katika mikutano, majukwaa ya kimataifa na ziara za kikazi katika mataifa mbalimbali. Pia tumekuwa

na ziara za Viongozi wa Kitaifa wa Nje na Mashirika ya Kikanda, tulikuwa na ziara za kikazi za Marais wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mikutano wa 20 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki uliofanyika Novemba, 2018 na Februari, 2019; lakini pia ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Rais Paul Kagame, Rais wa Jamhuri ya Rwanda mwezi Machi, 2019; Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Mustafa Madbouly, Waziri Mkuu wa Misri iliyofanyika Desemba, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Sheikh Saud Al Qasimi, Mtawala wa Ras Al Khaima, Umoja wa Falme za Kiarabu iliyofanyika Zanzibar mwezi Oktoba, 2018; Ziara ya kikazi ya Prince William, *the Duke of Cambridge*, iliyofanyika mwezi Septemba, 2018; Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Lee Nak-yon, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Korea iliyofanyika mwezi Julai, 2018; Ziara ya kikazi ya Bw. Gilbert Houngbo, Rais wa Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (*IFAD*) tarehe 19 hadi 22 Mei, 2019; Ziara ya kikazi ya Abebe Aemro Selassie, Mkurugenzi wa Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) Idara ya Afrika tarehe 5 hadi 6 Mei, 2019; Ziara ya Kikazi ya Mheshimiwa Dkt. Hafez Ghanem, Makamu wa Rais wa Benki ya Dunia Kanda ya Afrika iliyofanyika Novemba, 2018; Ziara za kikazi za Spika wa Mabunge ya Burundi, Cameroon na Misri zilizofanyika mwezi Aprili, 2019; Ziara ya kikazi ya Mheshimiwa Sheikh Mohammed bin Abdulrahman Al Thani, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Mambo ya Nje wa Qatar iliyofanyika mwezi Machi, 2019; na ziara za kikazi za Waheshimiwa Marais Wastaafu wa nchi za nje waliokuja hapa nchini katika vipindi tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ziara hizo nchi imeendelea kuimarisha mahusiano na ushirikiano na nchi na mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi zinazosimamiwa na Wizara; Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha; Kituo hiki kimeendelea kuwa kitovu cha diplomasia ya mikutano hapa nchini na kuchangia katika kukuza uchumi. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 Kituo hicho kimeingiza mapato ya jumla ya Shilingi bilioni

kumi na moja, milioni mia nne ishirini na nane, mia nane sitini na nane elfu na mia tisa tisini na nane. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni mbili, milioni sabini na sita, mia saba sabini na moja elfu na ishirini na saba zimetokana na huduma za mikutano 342 iliyofanyika katika kituo cha *AICC* ambapo 32 kati ya hiyo ni ya kimataifa na 310 ni ya kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shilingi bilioni mbili, milioni mia mbili arobaini na nne, mia tano thelathini na mbili elfu na mia siti na mbili zimetokana na huduma za Mikutano katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere; Shilingi bilioni tatu, milioni mia tano hamsini na sita, mia tano tisini na sita elfu na mia nane kumi na tisa ni kutokana na upangishaji wa nyumba na ofisi; na Shilingi bilioni tatu, milioni mia tano hamsini, mia tisa sitini na nane elfu na mia nne tisini ni kutokana na huduma za hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa *APRM*; katika mwaka wa fedha 2018/19 *APRM* Tanzania iliandaa ripoti ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango Kazi wake ilioangazia maeneo makuu manne ambayo ni Demokrasia na Siasa, Usimamizi wa Uchumi, Utendaji wa Mashirika ya Biashara na Utoaji wa Huduma za Jamii. Kwa ujumla ripoti hiyo imeonesha kuwa Tanzania imepiga hatua katika maeneo yote yaliyozingatiwa katika tathmini hiyo. Maelezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya *APRM* Tanzania yanapatikana kuanzia ukurasa wa 68 hadi 71 katika kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Diplomasia; Chuo hiki kimeendelea kutoa mafunzo na kufanya tafiti katika masuala ya diplomasia, Uhusiano wa Kimataifa na Usuluhishi wa Migogoro na Kulinda Amani. Chuo kinatoa mafunzo ya lugha saba (7) za kigeni ambazo ni Kiarabu, Kichina, Kifaransa, Kiingereza, Kireno, Kihispania na Kikorea. Aidha, hivi sasa Chuo kinafanya mazungumzo na Ubalozi wa Urusi hapa nchini kwa ajili ya kufadhili mafunzo ya lugha ya Kirusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Diplomasia kinaendelea kutekeleza Mpango wa Mafunzo kwa watumishi wake kitaaluma. Katika mwaka wa fedha 2018/2019

wafanyakazi wawili (2) wa ngazi ya shahada ya uzamivu na wawili (2) wa shahada ya umahiri wamehitimu masomo yao. Kadhalika, Chuo kimegharamia masomo kwa wafanyakazi kumi na tano (15). Nane (8) katika yao wanasoma shahada ya uzamivu, sita (6) wanasoma shahada ya umahiri na mmoja anasoma shahada ya kwanza, aidha, Chuo kimewasomesha wafanyakazi tisa mafunzo ya muda mfupi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuendelea kujenga uwezo wa watumishi Wizarani na Wizara kwa ujumla katika kutekeleza majukumu yake; Wizara inasimamia masuala ya utawala na maendeleo ya watumishi kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa sasa ina jumla ya watumishi 441 ambapo watumishi 280 wapo Makao Makuu ya Wizara, watumishi 17 wapo katika Ofisi ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Zanzibar na watumishi 144 wapo kwenye Balozi za Tanzania nje. Watumishi hawa wamegawanyika katika kada na fani tofauti zinazowezesha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kama yalivyoainishwa katika Muundo wa Wizara wa Julai, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo jumla ya watumishi 286 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani; kwa namna ya pekee naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru Mabalozi na baadhi yao wako hapa mmewaona, Wawakilishi wa Taasisi za Umoja wa Mataifa na Mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa kupitia nchi na mashirika yao kufanikisha mipango mbalimbali ya maendeleo inayotekelzwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kupata mafanikio makubwa kutokana na mchango wa wadau na Washirika wa Maendeleo kutoka nchi na Asasi mbalimbali za Kitaifa, Kikanda, Kimataifa

pamoja na sekta binafsi. Naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi za Afrika Kusini, Algeria, Ethiopia, Tunisia, Australia, Austria, Brazil, Canada, China, Cuba, Denmark, Finland, Hungary, India, Italia, Ireland, Israel, Iran, Japan, Jamhuri ya Korea, Kuwait, Malaysia, Marekani, Malta, Misri, Morocco, New Zealand, Norway, Oman, Pakistan, Palestina, Poland, Qatar, Saudi Arabia, Sweden, Singapore, Sri-Lanka, Thailand, Ubelgiji, Ufaransa, Uhispania, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Ureno, Urusi, Uswisi, Uturuki na Vietnam kwa kuchangia mafanikio hayo muhimu kwa Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani ziwaendee pia Umoja wa Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *African Capacity Building Foundation*, Benki ya Dunia, Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani, Shirika la Fedha Kimataifa, *Investment Climate Facility for Africa*, *UNDP* na Mashirika mengine yote ya Umoja wa Mataifa, *TradeMark East Africa*, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi ya Afrika (*BADEA*), *The Association of European Parliamentarians with Africa*, *WWF*, *WFP*, *The Belinda and Bill Gates Foundation*, *Global Fund*, *International Committee of the Red Cross*, *International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies*, *Medecins Sans Frontieres* pamoja na Mifuko na Mashirika mbalimbali ya Misaada, ni dhahiri kuwa mafanikio tuliyoyapata yamechangiwa kwa misaada na ushirikiano wetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na mambo mengine, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake ili kufikia malengo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kulinda na kutetea misingi ya Taifa ndani na nje ya nchi; kutekeleza Sera ya Mambo ya Nje inayoweka msisitizo katika Diplomasia ya Uchumi; kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa mikataba mbalimbali iliyosainiwa kati ya nchi yetu na nchi nyininge; kuratibu Mikutano ya Tume za Pamoja za Kudumu za Ushirikiano na kufuatilia utekelezaji wa makubaliano yaliyofikiwa;

kukamilisha Sera ya Taifa ya *Diaspora*; kushiriki katika shughuli za umoja wa Mataifa na Mashirika yake, Umoja wa Afrika na Jumuiya za Kikanda ambazo nchi yetu ni mwanachama; kutekeleza Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki zake; kusimamia majadiliano ya Rasimu ya Katiba ya Fungamano la Kisiasa la Afrika Mashariki; kutekeleza Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika na Itifaki zake; kuandaa Mkutano wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* na kutekeleza majukumu ya Uenyekiti wa *SADC* katika kipindi cha mwaka 2019/20; kutoa elimu kwa umma juu ya fursa zitokanazo na Mtangamano wa Jumuiya ya Afika Mashariki na Jumuiya nyingine za Kikanda; kutekeleza mpango wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na makazi Balozini pamoja na ujenzi wa jengo la ofisi ya Makao Makuu ya Wizara; kujenga uwezo wa watumishi wa Wizara; kuratibu ziara za viongozi wa juu wa nchi nje ya Tanzania; kuratibu ziara za Viongozi wa Mataifa mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa wanaokuja nchini; kufungua Ubalozi mpya *Windhoek* nchini Namibia; kufungua Konseli Kuu kwenye Miji ya Lubumbashi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Guangzhou nchini China; na kukamilisha Sera ya Taifa ya Mambo ya Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya taasisi ziilizo chini ya wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020; Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020, Kituo kinatarajia kukusanya mapato ya Shilingi bilioni kumi na sita, milioni mia tatu kumi na tatu, mia nane na tatu elfu na mia moja arobaini na tatu. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni kumi na tano, milioni mia sita na tatu, mia nne sitini na nane elfu na arobaini na nne ni kutoka vyanzo mbalimbali vya ndani; na Shilingi milioni mia saba na kumi, mia mbili arobaini na nane elfu na mia nane tisini na tatu zitatakana na mkopo.

Aidha, Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere kinatarajia kukusanya mapato ya Shilingi bilioni tatu, milioni mia moja na saba na mia saba elfu kutokana na huduma za mikutano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo kinatarajia kukopa shilingi milioni mia saba na kumi ...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri uombe fedha, muda umekwisha.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka 2019/2020, Wizara imepangiwa bajeti ya kiasi cha Shilingi bilioni mia moja sitini na sita, milioni mia tisa ishirini na sita, mia nane ishirini elfu. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni mia moja hamsini na mbili, milioni mia saba kumi na saba, mia saba ishirini na tatu elfu ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Shilingi bilioni kumi, milioni mia mbili na tisa na saba elfu ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi bilioni nne ni kwa ajili ya Bajeti ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha za bajeti ya Matumizi Mengineyo ya Wizara, Shilingi milioni mia tisa arobaini na nane, kumi na mbili elfu na mia nane sitini na sita ni kwa ajili ya Mpango wa APRM, Shilingi bilioni moja ni kwa ajili ya fedha za Matumizi Mengineyo ya Chuo cha Diplomasia, Shilingi bilioni moja, milioni mia mbili thelathini na tisa, mia sita thelathini na tatu elfu na mia saba hamsini na moja ni kwa ajili ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu na Shilingi milioni mia moja hamsini na nane, mia mbili sabini na tisa elfu na mia saba sitini ni kwa ajili ya Bodi ya Ushauri wa Masuala ya Rushwa ya Umoja wa Afrika. Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mishahara Shilingi bilioni mbili, milioni mia tano na saba na mia tisa themanini na sita ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Chuo cha Diplomasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa miradi itakayotekelezwa na fedha za bajeti ya fedha za maendeleo kiasi cha Shillingi bilioni nne zilizopangwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 ni kama inavyoonesha katika aya namba 195 ya kitabu cha Hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara kuititia Balozi zake inatarajia kukusanya kiasi cha Sh.2,550,879,070 ikiwa ni maduhuli ya Serikali. Ili kuweza kutekeleza kikamilifu majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Sh.166,926,820,000, kati ya fedha hizo Sh.162,926,820,195 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.4,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makof)

WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutamsikia Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba yake Mheshimiwa Cosato David Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba taarifa hii iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*), kama ilivyowasilishwa Mezani kwako.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Kwa kuwa leo ni siku ya kujadili bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanadiplomasia namba moja nchini Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa jinsi anavyoendelea kuiweka nchi yetu katika nafasi bora ya uhusiano na ushirikiano wa

kimataifa katika nyanja zote za kidiplomasia kiuchumi, kisasa na kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juhudhi hizo za kidiplomasia za Rais wetu zimepelekea nchi yetu kuwa na ushirikiano na uhusiano mzuri si tu kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile tunazopakana nazo, bali pia na nchi nyingine nyingi ndani na nje ya Bara la Afrika. Ushirikiano na uhusiano huu mzuri umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoja na kuanza kwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ya ujenzi wa Bwawa la Umeme la *Stiegler's Gorge* katika maporomoko ya maji ya Mto Rufiji; Ujenzi wa reli ya kisasa ya *Standard Gauge* na Ununuzi wa ndege kwa ajili ya ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL). Aidha, juhudhi hizo za Mheshimiwa Rais wetu zimeifanya Tanzania kujulikana zaidi katika Bara la Afrika na uso wa dunia kwa ujumla wake kuliko wakati mwingine wowote katika historia yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi hizo, kwa mujibu wa Kanuni ya 99, kifungu kidogo cha (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka wa fedha 2018/2019; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020, na kuliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 kifungu kidogo cha (3) (c) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara hii ni mionganini mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 kifungu kidogo cha (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Naomba kularifu Bunge lako Tukufu

kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 22 na 25 Machi, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika vikao hivyo, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019 kama ilivyoelekeza Kanuni ya 98 kifungu kidogo cha (2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu:-

(i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa Maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019; bajeti;

(ii) Uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo liliowekwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(iii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(iv) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu Changamoto za Utekelezaji wa bajeti katika mwaka wa fedha 2018/2019;

(v) Uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020;

(vi) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020; na

(vii) Mapitio ya Malengo ya bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la maelezo hayo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali halisi ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kulinganisha na Makadirio ya fedha za Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ili Bunge liweze kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nitajielekeza katika mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilihu maeneo makuu mawili. Maeneo hayo ni Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati na mapitio ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kama inavyoonekana katika ukurasa wa 4 hadi 9 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba upo ushauri uliozingatiwa, upo unaoendelea kuzingatiwa na upo ushauri unaohitaji kuzingatiwa zaidi katika utekelezaji wake hususani ushauri uliohusu masuala ya kibajeti. Kati ya ushauri uliopewa uzito kidogo katika utekelezaji wake ulihu Serikali kutoa fedha kiasi cha Sh.1,894,056,560 zilizokuwa zimetengwa katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ubalozi wa Tanzania Jijini Muscat, Oman. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilionesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 fedha hizo hazikutolewa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na ushauri huo, Kamati pia iliishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kuendeleza viwanja vya Balozi zake nje ya Nchi ikiwemo Viwanja vilivyopo London, Addis Ababa, Nairobi na Muscat. Kamati imebaini kuwa, katika kutekeleza ushauri huo, katika mwaka wa fedha 2018/2019 zilitengwa fedha Shilingi Bilioni 6.1 kwa ajili ya kuendeleza Kiwanja cha Muscat, hata hivyo, hadi kufikia mwezi Machi, 2019, fedha hizo hazikutolewa. Kamati ina maoni kuwa upo umuhimu kwa Serikali

kuviendeleza viwanja hivyo ili pamoja na mambo mengine, kuokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia Kodi ya Pango kwa majengo yaliyokodiwa kwa ajili ya makazi na Ofisi za Watumishi wa Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa bajeti, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato hadi Mwezi Februari 2019 pamoja na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019. Taarifa ya makusanyo hayo inaonekana katika ukurasa wa 6 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ulinganisho na hali ya ukusanyaji kwa mwaka wa fedha 2017/2018 hadi kufikia Februari, 2018. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari, 2018 makusanyo yalifika asilimia 72.4 tofauti na asilimia 64 ya lengo la makusanyo kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kuwa kiwango cha Makadirio ya Makusanyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kilongezeka kwa asilimia 9.7 ikilinganishwa na Makadirio ya Mwaka 2017/2018. Hali hii ilichangia asilimia ya makusanyo ya mapato kuonekana imepungua ikilinganishwa na makusanyo ya Mwaka 2017/2018 katika kipindi kama hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na asilimia ya makusanyo kuonekana imeshuka, tathmini iliyofanywa na Kamati ilionesha kuwa kiasi cha lengo kilichobaki kukusanywa ni Sh.10,229,995,763.66 sawa na asilimia 37 tu ambayo inaweza kukusanywa kwa kipindi cha Mwezi Machi hadi Juni, 2019. Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa ukusanyaji wa Maduhuli ni wa kuridhisha na lengo lililowekwa linaendana na hali halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Wizara ilipokea Sh.93,162,476,521

sawa na asilimia 52.6 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Hali hiyo ni tofauti na mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilipokea Sh.98,617,704,687.20 sawa na asilimia 65.38 ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijiridhisha kuhusu sababu ya kupungua kwa fedha zilizopelekwa Wizarani na kubaini kuwa hali hii imechangiwa na changamoto za kibajeti zilizosababisha kutokutolewa kwa fedha za maendeleo Sh.10,400,000,000 zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge tofauti na mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo Wizara, hadi kufikia mwezi Machi, ilipelekewa Sh.2,920,195,655.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kutokutolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kumeathiri utekelezaji wa miradi hiyo ambayo ina tija kwa Taifa hususan Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Jijini Muscat, Oman. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kutokutolewa kwa fedha hizo, kwa kutumia Kanuni ya 98 kifungu kidogo cha (3), Kamati iliwasilisha hoja ya Kibajeti ambayo ilishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha kwa ajili ya kuweseha utekelezaji wa Mradi wa Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Jijini Muscat, Oman. Kamati inapongeza Serikali kwa kuipokea Hoja hiyo ambapo imeahidi kuanza utekelezaji wake kabla ya mwaka wa fedha 2018/2019 haujakamilika. Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara ya Fedha kutoa kiasi cha Sh.322,333,563,000 kabla ya tarehe 15 Juni, 2019 kwa ajili ya kugharamia hatua za awali za ujenzi huo wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Balozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutohana na changamoto za kibajeti zilizosababisha kutokutolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo, Kamati ilitaka kujua Wizara ina mpango gani wa kuendeleza viwanja vyake vya Ubalozi nje ya nchi ikiwa fedha hizo hazitolewi. Maelezo ya Wizara yalibainisha kuwa Wizara imeandaa Mpango wa Ujenzi, Ununuzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi na Makazi Balozini utakaotekelzwa kwa kipindi cha miaka 15 (2018/2019 - 2031/32).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango huo, pamoja na Fedha za Maendeleo zitakazotengwa kila mwaka wa fedha, Wizara itatumia utaratibu wa karadha (*Mortgage Finance*) na kushirikisha Mifuko ya Jamii. Kamati inapongeza Mpango huu na inaamini utaratibu wa karadha utakuwa wa manufaa katika kupata majengo ya kutosha na yenyehadhi katika Balozi, lakini pia utaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipa kodi ya pango, kama ambavyo Kamati hii imekuwa ikishauri mara kwa mara. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/2019 pekee, Serikali ilitenga jumla ya Sh.21,667,174,191 kwa ajili ya kukodi Majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi zetu nje ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zilizojiteze wakati wa utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2018/2019. Kamati ilipopokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka 2018/2019, illibalini kuwa zipo changamoto mbalimbali ambazo ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2019. Changamoto hizo zimehainishwa katika ukurasa wa 9 - 10 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijadili kwa kina changamoto hizo na kuona kuwa, upo umuhimu kwa Serikali kuboresha utaratibu wa mtiririko wa fedha kwa Wizara hii hususan Fedha za Maendeleo. Aidha, juhudizaidi kwa ajili ya kutoa elimu kwa umma zifanyike ili wananchi wengi zaidi wapate uelewa kuhusu fursa zilizopo katika Mtangamano na Masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zilizopo kwenye masoko ya Kimataifa, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuendelea na msimamo wake wa kutokusaini Mkataba wa Ubia wa Uchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (EAC-EU EPA) hadi pale kasoro zilizobainika zitakaporekebishwa kama ambavyo Bunge lako Tukufu lilishauri Novemba, 2016. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kushawishi mapitio ya vipengele vya Mkataba huo

kwa kuzingatia Sera zetu za ndani ili uwe wenye manufaa kwa nchi na kuondoa taswira ya sasa ya Mkataba huo wa kuzifanya nchi za Afrika, Caribbean na Pasifikasi kuwa wasambazaji wa malighafi kwa Nchi za Ulaya na wakati huo huo kuwa soko la bidhaa za Umoja wa Ulaya jambo ambalo lisipopingwa linaweza kuuwa azma ya kuwa na viwanda vyetu wenyewe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najielekeza katika uchambuzi wa malengo ya bajeti. Kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020, napenda kutoa taarifa kuwa, pamoja na mambo mengine, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake ili kufikia malengo 13 ya kibajeti. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati kuhusu malengo yaliyoanishwa umebaini kuwa hakuna lengo mahsusini kuhusu uendelezaji wa viwanja vya Balozi zetu nje ya nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa jambo hili linapaswa kupewa uzito unaostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilipitia Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa Makadirio hayo yamepungua kwa asilimia 91 ikilinganishwa na Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato kwa mwaka wa fedha unaoishia. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya Sh.28,564,158,100 wakati kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara inalenga kukusanya kiasi cha Sh 2,550,879,072. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa upungufu huo unasababishwa na makusanyo ya Mapato ya Visa kuanza kufanyika kwa njia ya Visa Mtandao yaani (E-visa) ambapo fedha hizo zitakuwa zikilipwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali badala ya kukusanywa na Ofisi za Balozi kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi. Kamati ilielezwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh.166,926,820,000 ambapo Sh.152,717,723,195 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo yaani

(OC), na Sh.10,209,097, ni kwa ajili ya Mishahara na Sh.4,000,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa bajeti inayooombwa ni pungufu kwa asilimia 5.7 ikilinganshwa na bajeti iliyoidhishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019. Upungufu huu upo katika maeneo yote matatu ya matumizi ambayo ni Matumizi Mengineyo (OC), Mishahara na Fedha za Maendeleo. Bajeti ya Mishahara imepungua kwa asilimia 13.5, Matumizi Mengineyo yamepungua kwa asilimia 1.4 na Maendeleo yamepungua kwa asilimia 61.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na upungufu huo wa bajeti hususan katika Fedha za Maendeleo, Kamati ilitaka kujiridhisha kama miradi iliyopanga kutekelezwa ni ile ambayo hajatekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kamati ilibaini kuwa, Mradi wa Ujenzi wa Majengo ya Ubalozi Jijini Muscat, Oman haujawekwa katika makadirio ya mwaka wa fedha 2019/2020 licha ya umuhimu wake na badala yake miradi mingine mipyta sita imeongezwa katika maombi ya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza katika sehemu ya pili ya taarifa hii Mradi huo uliidihiishiwa fedha kwa miaka miwili mfululizo yaani 2017/2018 na 2018/2019 lakini fedha hizo hazijawahi kutolewa kutohana na changamoto za kibajeti. Kamati ina maoni kuwa ni vema Serikali ikatekeleza miradi yenye umuhimu kiuchumi ambayo bado hajatekelezwa kabla ya kuendelea na utekelezaji wa miradi mingine mipyta. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sura ya uwiano wa bajeti iliyotengwa kwa vipengele hivyo vitatu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na 2019/2020 ina tofauti hususan katika fedha za Maendeleo kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 1. Kutohana na uchambuzi wa uwiano wa bajeti kama inavyoonekana jedwali hilo, Kamati ina imani kuwa Serikali itaona umuhimu wa kuboresha mwenendo huu wa uwiano.

Aidha, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuona umuhimu wa kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo hususan ile inayohusu ukarabati na ujenzi wa Balozi mpya katika maeneo ya kimkakati kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajielekeza sasa katika maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kuwasilisha uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, naomba sasa niwasilishe maoni na ushauri wa Kamati, kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ihakikishe kuwa fedha zote kiasi cha Sh.10,400,000,000 zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kabla ya mwaka huu wa fedha 2018/2019 kuisha. Fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya kukarabati majengo ya Ubalozi wa Tanzania Khartoum, Sudan; ujenzi wa Ofisi wa Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, Kurasini Dar es Salaam.

(ii) Serikali ione umuhimu wa kuendelea kutenga Fedha na kutekeleza Miradi muhimu ambayo haijapelekewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoishia ili kufanikisha utekelezaji wa Miradi hiyo ya Kimkakati. Kwa mfano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Mradi wa ujenzi wa Ubalozi wa Muscat-Oman haujatengewa Fedha licha ya kuwa ilitengewa Fedha 2017/2018 na 2018/2019 na Fedha hizo hazikutolewa. Kamati inaanmini kuwa Serikali itapata fursa nydingi kiuchumi endapo itafanikiwa kujenga Ubalozi nchini Oman ikizangatiwa kuwa nchi hiyo ni miongoni mwa nchi zenyenye uchumi mzuri Duniani.

(iii) Pamoja na nia njema ya Serikali katika kutumia Wakala wa Serikali katika usimamizi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Balozi mbalimbali nje ya Nchi, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara kuhakikisha kuwa Wakala wetu wanatekeleza kwa ufanisi jukumu hilo.

(iv) Kwa kuwa Chuo cha Diplomasia kimeendelea kukabiliwa na changamoto ya upungufu na uchakavu wa miundombinu yake, Kamati inaishauri Serikali kutoa Shilingi bilioni 2.4 zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa ajili ya kupanua na kuboresha miundombinu hiyo. Upanuzi na ukarabati wa miundombinu utakisaidia Chuo kuongeza udahili utakaowezesha Chuo kujitanua na kujitegemea.

(v) Upo umuhimu wa Serikali kuhakikisha mchakato wa kupatikana kwa Sera ya Taifa ya *Diaspora*. Sera hiyo itawezesha Watanzania wanaishi nje ya nchi kuchangia zaidi katika Maendeleo ya Tanzania hususan kiuchumi, jambo ambalo kwa sasa halifanyiki kutohana na kukosekana kwa Mwongozo wa namna ya kuwashirikisha. (*Makofî*)

(vi) Kamati inaendelea kushauri kuwa Fedha zinazotengwa kwa ajili ya safari za kikazi za Viongozi wa Kitaifa nje ya nchi zitolewe moja kwa moja na Hazina bila kuitishwa katika Fungu la Wizara hii. Jambo hili litasaidia kuweka uhalisia katika Bajeti ya Wizara kwa kutenga Bajeti inayohusu majukumu yao moja kwa moja.

(vii) Kwa kuwa kituo cha Kimataifa cha mikutano cha Arusha hakujengwa mahsus kwa ajili ya shughuli za Mikutano jambo linaloathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa hakikidhi hadhi ya kimataifa. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuitia Wizara ya fedha kuupitisha haraka Mradi wa ujenzi wa kituo kipycha cha Mikutano cha *Mt. Kilimanjaro International Convention Centre* ambacho kinatarajiwa kukidhi viwango vya Kimataifa.

(viii) Kwa kuwa kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kinazidai baadhi ya Wizara na Taasisi takribani Shilingi Bilioni tatu kutohana na huduma za Mikutano, Kodi ya pango la Ofisi na nyumba, Kamati inaishauri *AICC* kutumia njia nyingine zaidi za kukusanya madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuhusisha Kampuni za kukusanya madeni yaani *auction mart* na vilevile kuwataja wadaiwa hao katika vyombo vya habari. Ulipwaji wa madeni hayo utakisaidia Kituo hicho

kuendelea kujidesha kwa ufanisi na kuendelea kutoa gawio la makusanyo yake kwa Serikali.

(ix) Kwa kuwa kumekuwa na kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na Masoko ya Kimataifa sambamba na uelewa mdogo wa Watanzania kuhusu masuala ya Mtangamano, Wizara iendelee kutoa elimu kwa umma kuhusu fursa zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na Masoko ya Kimataifa.

(x) Kwa kuwa Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora, Tanzania (APRM-Tanzania) bado haujapewa *legal entity* jambo linalosababisha Mpango huo kukosa Fungu yaani vote la Kibajeti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa Mpango huo kuwa na Fungu lake mahsusili ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa sasa matumizi ya Mpango huu yanapitia katika Fungu la Wizara chini ya Idara ya Afrika (*African Division*).

(xi) Kwa kuwa kiwango cha Fedha za Bajeti zinazotolewa kwa Wizara kimekuwa hakiendani na mtiririko wa Fedha uliopangwa jambo ambalo linasababisha Wizara na Balozi zake kutotekeleza ipasavyo majukumu yake ya msingi, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe kuwa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 zinatolewa kwa kuzingatia mtiririko uliopangwa.

(xii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza kasi ya kukamilisha upatikanaji wa Sera mpya ya Mambo ya Nje itakayojumuisha masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Sera hii, pamoja na kwamba itaendana na hali halisi ya sasa ya Diplomasia ya kiuchumi, itaiwezesha Serikali kuwa na Mwongozo wa kutekeleza masuala mbalimbali ya Kijumuiya.

(xiii) Pamoja na Kamati kuipongeza Serikali kwa kuandaa Mpango wa miaka 15 utakaoanza 2018/2019 mpaka 2031/2032 wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi zetu. Kamati

inaendelea kushauri kuwa, Mpango huu utoe kipaumbele katika kuendeleza viwanja vya Balozi ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu kwani visipoendelezwa vitakuwa katika hatari ya kuchukuliwa na Serikali za nchi hizo. Viwanja hivyo ni pamoja na vile vilivyopo London, Uingereza; Muscat-Oman, Adis Ababa-Ethiopia na Nairobi-Kenya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba yao kama yalivyo yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi, (Mbunge), Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro (Mbunge) Katibu Mkuu Ndugu Faraji Kasidi Mnyepe, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Ramadhan Muombwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali

kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mto Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha. (*Makoffi*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI (FUNGU 34) KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

SEHEMU YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leo ni siku ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mwanadiplomasia namba moja Nchini Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa jinsi anavyoendelea kuiweka nchi yetu katika nafasi bora ya Uhusiano na Ushirikiano wa Kimataifa katika Nyanja zote za Kidiplomasia ya Kiuchumi, Kisiasa na Kijamii.

Mheshimiwa Spika, juhudhi hizo za Rais wetu za Kidiplomasia zimeipelekea nchi yetu kuwa na Ushirikiano na Uhustiano mzuri si tu kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na zile tunazopakana nazo, bali pia na Nchi nyingine nyingi ndani na nje ya Bara la Afrika.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na uhustiano huu mzuri umechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha uchumi wa nchi yetu ikiwa ni pamoa na kuanza kwa utekelezaji wa Miradi Mikubwa ya Kimkakati ya Ujenzi wa Bwawa la Umeme la

Stiegler's Gorge katika Maporomoko ya Maji ya Mto Rufiji, Ujenzi wa Reli ya kisasa ya *Standard Gauge* na Ununuzi wa Ndege kwa ajili ya ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL).

Mheshimiwa Spika, juhudhi hizo za Rais wetu zimeifanya Tanzania kujulikana zaidi katika Bara la Afrika na uso wa Dunia kwa ujumla wake kuliko wakati mwenginee wowote katika historia yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, [Kanuni za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, na kuliomba Bunge lako Tukufu ilipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3) (c) cha Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Bunge, Wizara hii ni miongoni mwa Wizara zinazosimamiwa na Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama. Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge kimezipa jukumu Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kushughulikia Bajeti za Wizara inazosimamia.

Naomba kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki tarehe 22 na 25 Machi, 2019.

Mheshimiwa Spika, katika vikao hivyo, Kamati ilipokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama inavyoelekeza Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge kwa lengo la kulinganisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Taarifa ninayoiwasilisha inatoa maelezo kuhusu: -

- i) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu uzingatiaji wa Maoni yaliyotolewa na Kamati Bungeni wakati wa kujadili Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- ii) Uchambuzi wa ukusanyaji wa maduhuli ikilinganishwa na lengo lililowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- iii) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu upatikanaji wa Fedha zilizoidhinishwa na Bunge pamoja na utekelezaji wa majukumu na malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- iv) Mapitio ya Taarifa ya Wizara kuhusu Changamoto za Utekelezaji wa Bajeti katika Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- v) Uchambuzi wa majukumu na malengo yanayowekwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020;
- vi) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na
- vii) Mapitio ya Malengo ya Bajeti na Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, lengo la maelezo hayo ni kuliwezesha Bunge kupata taswira ya hali ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na kulinganisha na Makadirio ya Fedha za Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ili Bunge liweze kuamua kuhusu Maombi ya Wizara hii.

SEHEMU YA PILI

2.0 MAPITIO YA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilihusu maeneo Makuu mawili. Maeneo hayo ni Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati na Mapitio ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina maeneo yote mawili kama ifuatavyo: -

2.1 Uzingatiaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, Bunge lilipokuwa likijadili hoja ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilitoa ushauri katika masuala kumi na nane. Katika kufuatilia namna ambavyo Wizara imezingatia Ushauri huo, tarehe 22 Machi, 2019, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki alijulisha Kamati kuhusu utekelezaji wa masuala hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, upo ushauri uliozingatiwa, upo unaoendelea kuzingatiwa na upo ushauri unaohitaji kuzingatiwa zaidi katika utekelezaji wake hususan ushauri uliohusu masuala ya Kibajeti.

Mheshimiwa Spika, mionganini mwa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu Wizara kuendelea kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuvutia watalii wengi zaidi kutembelea Tanzania.

Kamati ilielezwa kuwa Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii katika kuratibu ushiriki wa nchi yetu katika maonesho na makongamano, kuandaa ziara maalum za waandishi wa habari wanaotangaza utalii duniani na kuratibu makubaliano mbalimbali yanayolenga kutangaza kwa pamoja vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Kamati inapongeza juhudzi za Serikali kwani ni ukweli ulio wazi

kuwa sekta ya utalii ni moja ya sekta muhimu nchini ambazo zinachangia katika kukuza pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, moja ya ushauri unaoendelea kufanyiwa kazi unahusu ukamilishaji wa Sera Mpya ya Mambo ya Nje itakayojumuisha Sera ya Mtangamano wa Afrika Mashariki.

Maelezo yaliyotolewa na Wizara yalibainisha kuwa, Wizara imekwishakamilisha Rasimu ya Sera hiyo ambapo hatua inayofuata ni kuiwasilisha kwa Wadau mbalimbali kwa lengo la kukusanya maoni kwa ajili ya kuiboresha zaidi.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa Rasimu hiyo itahusisha kwa kina masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki ili kupata ufumbuzi wa changamoto zinazojitokeza katika uratibu wa masuala ya Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa ni muhimu Serikali ikakamilisha haraka upatikanaji wa Sera hiyo muhimu ikizingatiwa kuwa Sera inayotumika sasa, pamoja na mambo mengine, hajajumuisha masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato huu katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa kuwa tangu Mwaka wa Fedha 2017/2018 Kamati imekuwa ikielezwa kuwa mchakato huo unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kati ya ushauri uliopewa uzito kidogo katika utekelezaji wake ulihusu Serikali kutoa fedha kiasi cha Shilingi **1,894,056,560.00** zilizokuwa zimetengwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ubalozi wa Tanzania Jijini Muscat, Oman. Taarifa iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilionesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 fedha hizo hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, Sambamba na ushauri huo, Kamati pia illiishauri Serikali kutoa kipaumbele katika kuendeleza viwanja vya Balozi zake nje ya Nchi ikiwemo Viwanja vilivyopo London, Addis Ababa, Nairobi na Muscat. Kamati imebaini kuwa, katika kutekeleza ushauri huo, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 zilitengwa Shilingi Bil. 6.1 kwa ajili ya kuendeleza Kiwanja

cha Muscat, hata hivyo, hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, fedha hizo hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kuwa upo umuhimu kwa Serikali kuviendoeleza viwanja hivyo ili pamoja na mambo mengine, kuokoa fedha nyingi zinazotumika kulipia Kodi ya Pango kwa majengo yaliyokodiwa kwa ajili ya makazi na Ofisi za Watumishi wa Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ushauri wa Kamati umefanyiwa kazi na utekelezaji upo katika hatua mbalimbali. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo katika Balozi za Tanzania nje ya nchi unapaswa kupewa uzito stahiki. Utekelezaji huo unahuksu ukarabati wa majengo na uendelezaji wa viwanja vya Balozi.

2.2 Uchambuzi wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa kuchambua hali ya Ukusanyaji wa Mapato hadi Mwezi Februari 2019 pamoja na upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019.

2.2.1 Ukusanyaji wa Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Wizara hii ilikuwa na lengo la kukusanya Maduhuli ya Serikali kiasi cha Shilingi **28,564,158,100.00**. Kamati ilijulishwa kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2019, Wizara kuititia Balozi zake ilikusanya Jumla ya Shilingi **18,334,162,336.34** sawa na **asilimia 64** ya lengo la ukusanyaji lililo kusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho na hali ya ukusanyaji kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 hadi kufikia Februari, 2018. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa katika kipindi cha Julai 2017 hadi Februari, 2018 makusanyo yalifika **asilimia 72.4** tofauti na **asilimia 64** ya lengo la makusanyo kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019.

Kamati ilijiridhisha kuwa Kiwango cha Makadirio ya Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kiliongezeka kwa **asilimia 9.7** ikilinganishwa na Makadirio ya Mwaka 2017/2018. Hali hii ilichangia asilimia ya makusanyo ya mapato kuonekana imepungua ikilinganishwa na makusanyo ya Mwaka 2017/2018 katika kipindi kama hicho.

Mheshimiwa Spika, pamoja na asilimia ya makusanyo kuonekana imeshuka, tathmini iliyo fanywa na Kamati ilionesa kuwa kiasi cha lengo kilichobaki kukusanywa ni Shilingi **10,229,995,763.66** sawa na asilimia 37 tu ambayo inaweza kukusanywa kwa kipindi cha Mwezi Machi hadi Juni, 2019. Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa ukusanyaji wa Maduhuli ni wa kuridhisha na lengo lili lowekwa linaendana na hali halisi.

2.2.2 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipochambua Taarifa ya upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilibaini kuwa hadi kufikia Mwezi Februari, 2019 Wizara ilipokea **Shilingi 93,162,476,521.00** sawa na **asilimia 52.6** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Hali hiyo ni tofauti na Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2018, Wizara ilipokea **Shilingi 98,617,704,687.20** sawa na **asilimia 65.38** ya Bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijiridhisha kuhusu sababu ya kupungua kwa Fedha zilizopelekwa Wizarani na kubaini kuwa hali hii imechangiwa na changamoto za kibajeti zilizosababisha kuto kuto lewa kwa fedha za maendeleo tofauti na Mwaka wa Fedha 2017/2018 ambapo Wizara, hadi kufikia Mwezi Machi, ilipelekewa Shilingi **2,920,195,655.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kati ya Fedha zilizopokelewa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Shilingi **86,702,025,696.00** sawa na **asilimia 56** ya Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya Matumizi

Mengineyo na Shilingi **6,460,460,825.00** sawa na **asilimia 55** ya Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya Mishahara.

Mheshimiwa Spika, Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, Shilingi **10,400,000,000/-** = zililenga kutekeleza Miradi ya Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman, Ukarabati wa majengo ya Ofisi na makazi yaliyopo Ubalozi wa Tanzania Khartoum, Sudan na Upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kutokutolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo kumeathiri utekelezaji wa miradi hiyo ambayo ina tija kwa Taifa hususan Mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Jijini Muscat, Oman.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Kanuni ya 98 (3), Kamati iliwasilisha hoja ya Kibajeti ambayo iliishauri Serikali kuona umuhimu wa kutoa fedha kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa Ofisi ya Ubalozi wa Tanzania Jijini Muscat, Oman.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipokea Hoja hiyo ambapo imeahidi kuanza utekelezaji wake kabla ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 haujakamilika. Kamati inaendelea kuisitiza Wizara ya Fedha kutoa fedha kiasi cha Shilingi **Milioni 322,333,563/=** kabla ya tarehe 15 Juni, 2019 kwa ajili ya kugharamia hatua za awali za ujenzi huo wa Jengo la Ofisi na Makazi ya Balozi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kutokana na changamoto za kibajeti zilizosababisha kutokutolewa kwa fedha za Miradi ya Maendeleo, Kamati illitaka kujua Wizara ina mpango gani wa kuendeleza viwanja vyake vya Ubalozi nje ya nchi ikiwa fedha hizo hazitolewi. Maeleo ya Wizara yalibainisha kuwa Wizara imeandaa mpango wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi na makazi Balozini utakaotekelzwa kwa kipindi cha Miaka 15 (2018/2019-2031/32).

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa Mpango huo, pamoja na Fedha za Maendeleo zitakazotengwa kila Mwaka wa Fedha, Wizara itatumia utaratibu wa karadha (Mortgage

Finance) na kushirikisha Mifuko ya Jamii. Kamati inapongeza Mpango huu na ina amini kabisa utaratibu wa karadha utakuwa wa manufaa katika kupata majengo ya kutosha na yenye hadhi katika Balozi, lakini pia utaokoa fedha nyingi zinazotumika kulipa kodi ya pango, kama ambavyo Kamati hii imekuwa ikishauri mara kwa mara. Kwa mfano, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali ilitenga Jumla ya Shilingi **Bilioni 21,667,174,191.00** kwa ajili ya kukodi Majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi zetu nje ya Nchi.

2.2.3 Changamoto zilizojitokeza wakati wa kutekeleza Bajeti ya Mwaka 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipopokea Taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2018/2019, ilibaini kuwa zipo changamoto mbalimbali ambazo ziliathiri utekelezaji wa majukumu ya Wizara katika kipindi cha Julai hadi Februari, 2019. Changamoto hizo ni pamoja na: -

- i) Kiwango cha Fedha za Bajeti zinazotolewa kwa Wizara kutoendana na Mtiririko wa Fedha uliowasilishwa Hazina. Jambo hili limesababisha Wizara na Balozi zake kutotekeliza ipasavyo majukumu yake ya msingi;
- ii) Kutokutolewa kwa Fedha za Bajeti ya Maendeleo ambazo zimeidhinishwa na Bunge kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo jambo ambalo limesababisha miradi ya ujenzi na ukarabati kutotekeliza kwa ratiba inayopangwa;
- iii) Balozi nyingi kuwa na magari ya uwakilishi na huduma yaliyochakaa. Hali inayosababisha Wizara kutumia ghamama kubwa kwa ajili ya matengenezo ya magari hayo pale ambapo fedha zinapatikana; na
- iv) Kasi ndogo ya Sekta Binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilijadili kwa kina changamoto hizo na kuona kuwa, upo umuhimu kwa Serikali kuboresha

utaratibu wa mtiririko wa fedha kwa Wizara hii hususan Fedha za Maendeleo. Aidha, juhudzi zaidi kwa ajili ya kutoa elimu kwa Umma zifanyike ili Wananchi wengi zaidi wapate ulewa kuhusu fursa zilizopo katika Mtangamano na Masoko ya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa zilizopo kwenye masoko ya Kimataifa, Kamati inaendelea kuipongeza Serikali kwa kuendelea na Msimamo wake wa kutokusaini Mkataba wa Ubia wa Uchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya (EAC-EU EPA) hadi pale kasoro zilizobainika zitakaporekebishwa kama ambavyo Bunge lako Tukufu lilishauri Mwezi Novemba, 2016.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kushawishi mapitio ya vipengele vya Mkataba huo kwa kuzingatia Sera zetu za ndani ili uwe wenyewe manufaa kwa Nchi na kuondoa taswira ya sasa ya Mkataba huo wa kuzifanya nchi za Afrika, Caribean na Pasifikasi (ACP) kuwa wasambazaji wa malighafi kwa Nchi za Ulaya na wakati huo huo kuwa soko kuu la bidhaa za Umoja wa Ulaya (EU) jambo ambalo lisipopingwa linaweza kuuwa azma ya kuwa na Viwanda vyetu wenyewe.

SEHEMU YA TATU

3.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA BAJETI YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

3.1 Uchambuzi wa Malengo ya Bajeti

Mheshimiwa Spika, kabla ya kueleza uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, napenda kutoa Taarifa kuwa, Kamati ilielezwa kuhusu maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 yamezingatia miongozo kumi na mbili inayolenga kutekeleza Sera na Mikakati mbalimbali ya Serikali.

Miongoni mwa miongozo hiyo, ni Sera ya Mambo ya Nje ya mwaka 2001, ambayo ina umri mrefu wa takribani miaka kumi na nane na inahitaji kurekebishwa, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na Maoni na Mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wakati wa kujadili Mpango na Bajeti ya Wizara kwa kipindi cha Mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati ilielezwa kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Wizara imepanga kutekeleza majukumu yake ili kufikia Malengo Kumi na Tatu ya Kibajeti. Mfano wa Malengo hayo ni kutekeleza Diplomasia ya Uchumi kwa kuvutia Wawekezaji na Wafanyabiashara kutoka nje, kuvutia Watilii na kushiriki katika Jumuiya za Kikanda kwa lengo la kuongeza ajira na Masoko ya bidhaa za Tanzania nje.

Vilevile, Wizara inalenga kuendelea kutekeleza Mkataba wa Uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Itifaki yake. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza lengo la kuratibu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kipaumbele iliyopitishwa na Wakuu wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki katika Mkutano wao Mwezi Februari, 2018.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu malengo yaliyoanishwa umebaini kuwa hakuna lengo mahsus kuhusu uendelezaji wa viwanja vya Balozi zetu nje ya nchi. Ni maoni ya Kamati kuwa Jambo hili linapaswa kupewa uzito unaostahili.

3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa bajeti ya Wizara hii, Kamati ilipitia Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato yanayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Katika uchambuzi huo, Kamati ilibaini kuwa Makadirio hayo yamepungua kwa **asilimia 91** ikilinganishwa na Makadirio ya ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha unaoishia. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilikuwa na lengo la kukusanya Shilingi **28,564,158,100/-** wakati kwa Mwaka wa

Fedha 2019/2020, Wizara inalenga kukusanya kiasi cha Shilingi **2,550,879,072/-**.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa upungufu huo unasababishwa na makusanyo ya Mapato ya Visa kuanza kufanyika kwa njia ya Visa Mtandao (e-visa) ambapo Fedha hizo zitakuwa zikilipwa moja kwa moja kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali badala ya kukusanywa na Ofisi za Balozi kama ilivyo sasa.


Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Shilingi **2,550,879,072/-**- zinalengwa kukusanywa kutoka katika vyanzo vingine kama vile pango la majengo kwa baadhi ya Balozi na uthibitishaji wa vyeti vya Taaluma. Kamati imejiridhisha kuwa lengo liliowekwa limeendana na hali halisi kutokana na sababu iliyoinishwa hapo juu.

3.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara hii inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Shilingi **166,926,820,000/=** ambapo Shilingi **152,717,723,195/=** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), Shilingi **10,209,097,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **4,000,000,000/=** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilichambua maombi hayo na kuona kuwa asilimia **91.5** ya fedha zinaoombwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, asilimia **6.1** ni kwa ajili ya Mishahara na asilimia **2.4** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama inavyoonekana katika Chati Na. 1 ya Taarifa hii.

Chati Na. 1: Uwiano wa Fedha zinazoombwa kwa Matumizi ya Wizara



Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020

Mheshimiwa Spika, vile vile, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa Bajeti inayoombwa ni pungufu kwa asilimia **5.7** ikilinganshwa na Bajeti iliyoidhishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Upungufu huu upo katika maeneo yote matatu ya matumizi ambayo ni Matumizi Mengineyo (OC), Mishahara na Fedha za Maendeleo. Bajeti ya Mishahara imepungua kwa asilimia **13.5**, Matumizi Mengineyo imepungua kwa asilimia **1.4** na Maendeleo imepungua kwa asilimia **61.5**.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo wa Bajeti hususan katika Fedha za Maendeleo, Kamati ilitaka kujiridhisha kama Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni ile ambayo haijatekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati ilibaini kuwa, Mradi wa ujenzi wa majengo ya ubalozi Jijini Muscat, Oman haujawekwa katika Makadirio ya Mwaka 2019/2020 licha ya umuhimu wake na badala yake miradi mingine mipya sita imeongezwa katika maombi ya Fedha.

Mradi huo umekuwa ukitengewa fedha kwa miaka miwili mfululizo yaani 2017/2018 na 2018/2019 lakini fedha hizo hazijawahi kutolewa kutokana na changamoto za kibajeti. Kamati ina maoni kuwa ni vema Serikali ikatekeleza miradi yenye umuhimu kiuchumi ambayo bado haijatekelezwa kabla ya kuendelea na utekelezaji wa Miradi mingine mipyä.

Mheshimiwa Spika, sura ya uwiano wa Bajeti iliyotengwa kwa vipengele hivyo vitatu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na 2019/2020 ina tofauti hususan katika Fedha za Maendeleo kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1.

Jedwali Na. 01: Uwiano wa aina za Bajeti ya Matumizi na ulinganisho wake kwa mwaka 2018/2019 na 2019/2020

MWAKA	2018/2019		2018/2019		% PUNGUFU	
	AINA YA MATUMIZI	KIASI	ASILIMA	KIASI	ASILIMA	
<i>MISHAHARA (PE)</i>	11,795,400,000.00	6.66		10,209,097,000.00	6.1	13.5
<i>MATUMIZI MENGINEYO (OC)</i>	154,810,812,000.00	87.46		152,717,723,195.00	91.5	1.4
<i>MIRADI YA MAENDELEO</i>	10,400,000,000.00	5.88		4,000,000,000.00	2.4	61.5
<i>JUMLA</i>	177,006,212,000.00	100		166,926,820,000.00	100	5.7

Chanzo: Randama ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchambuzi wa uwiano wa Bajeti kama inavyoonekana hapo juu, Kamati ina imani kuwa Serikali itaona umuhimu wa kuboresha mwenendo huu wa uwiano. Aidha, Kamati inatoa rai kwa Serikali kuona umuhimu wa kuendelea kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo hususan ile inayohusu ukarabati na ujenzi wa Balozi mpya katika maeneo ya kimkakati kiuchumi.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, naomba sasa niwasilishe Maoni na Ushauri wa Kamati: -

i) Serikali ihakikishe kuwa Fedha zote kiasi cha Shilingi **10,400,000,000/=** zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zitolewe kabla ya Mwaka huu wa Fedha 2018/2019 kuisha. Fedha hizo zilitengwa kwa ajili ya kukarabati majengo ya Ubalozi wa Tanzania Khartoum, Sudan, ujenzi wa Ofisi wa Ubalozi wa Tanzania Muscat, Oman na upanuzi na uboreshaji wa miundombinu ya Chuo cha Diplomasia, Kurasini Dar es Salaam.

ii) Serikali ione umuhimu wa kuendelea kutenga Fedha na kutekeleza Miradi muhimu ambayo haijapelekewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoishia ili kufanikisha utekelezaji wa Miradi hiyo ya Kimkakati. Kwa mfano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Mradi wa ujenzi wa Ubalozi wa Muscat, Oman haujatengewa Fedha licha ya kuwa ultengewa Fedha 2017/2018 na 2018/2019 na Fedha hizo kutokutolewa.

Kamati ina amini kuwa Serikali itapata fursa nyingi za kiuchumi endapo itafanikiwa kujenga Ubalozi nchini Oman ikizangatiwa kuwa Nchi hiyo ni miongoni mwa nchi zenye uchumi mzuri Duniani.

iii) Pamoja na nia njema ya Serikali katika kutumia Wakala wa Serikali katika usimamizi wa Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Makazi ya Balozi mbalimbali nje ya Nchi, Kamati inatoa angalizo kwa Wizara kuhakikisha kuwa Wakala wetu wanatekeleza kwa ufanisi jukumu hilo.

iv) Kwa kuwa Chuo cha Diplomasia kimeendelea kukabiliwa na changamoto ya upungufu na uchakavu wa miundombinu

yake, Kamati inaishauri Serikali kutoa Shilingi **2,400,000,000/-** zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa ajili ya kupanua na kuboresha miundombinu hiyo. Upanuzi na ukarabati wa Miundombinu utakisaidia Chuo kuongeza udahili utakaowezesha Chuo kujitanua na kujitegemea.

v) Upo umuhimu wa Serikali kuharakisha Mchakato wa kupatikana kwa Sera ya Taifa ya Diaspora. Sera hiyo itawezesha Watanzania wanaoishi nje ya nchi kuchangia zaidi katika Maendeleo ya Tanzania hususan kiuchumi, jambo ambalo kwa sasa halifanyiki kutokana na kukosekana kwa Mwongozo wa namna ya kuwashirikisha.

vi) Kamati inaendelea kushauri kuwa Fedha zinazotengwa kwa ajili ya safari za kikazi za Viongozi wa Kitaifa nje ya Nchi zitolewe moja kwa moja na Hazina bila kupitishwa katika Fungu la Wizara hili. Jambo hilli litasaidia kuweka uhalisia katika Bajeti ya Wizara kwa kutenga Bajeti inayohusu majukumu yao moja kwa moja.

vii) Kwa kuwa kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha hakujengwa mahsus kwa ajili ya shughuli za Mikutano jambo linaloathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi kwa kuwa hakikidhi hadhi ya Kimataifa, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupitia Wizara ya fedha kuupitisha haraka Mradi wa ujenzi wa kituo kipyaa cha Mikutano cha ***Mt. Kilimanjaro International Convention Centre*** ambacho kinatarajiwa kukidhi viwango nya Kimataifa.

viii) Kwa kuwa kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kinazidai baadhi ya Wizara na Taasisi takribani Shilingi **Bilioni tatu** kutokana na huduma za Mikutano, Kodi ya pango la Ofisi na nyumba, Kamati inaishauri AICC kutumia njia nyingine zaidi za kukusanya madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuhusisha Kampuni za kukusanya madeni (**auction mart**) na vilevile kuwataja wadaiwa hao katika vyombo nya habari. Ulipwaji wa madeni hayo utakisaidia Kituo hicho kuendelea kuijiendesha kwa ufanisi na kuendelea kutoa gawio la makusanyo yake kwa Serikali.

- ix) Kwa kuwa kumekuwa na kasi ndogo ya sekta binafsi kutumia fursa za biashara na uwekezaji zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na Masoko ya Kimataifa sambamba na uelewa mdogo wa Watanzania kuhusu masuala ya Mtangamano, Wizara iendelee kutoa elimu kwa Umma kuhusu fursa zitokanazo na Mtangamano wa Afrika Mashariki na Masoko ya Kimataifa.
- x) Kwa kuwa Mpango wa Kujitathmini kwa Utawala Bora, Tanzania (APRM- Tanzania) bado haujapewa *legal entity* jambo linalosababisha Mpango huo kukosa Fungu (vote) la Kibajeti, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuona umuhimu wa Mpango huu kuwa na Fungu lake mahsusili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Kwa sasa matumizi ya Mpango huu yanapitia katika Fungu la Wizara chini ya Idara ya Afrika (**Africa Division**).
- xi) Kwa kuwa kiwango cha Fedha za Bajeti zinazotolewa kwa Wizara kimekuwa hakiendani na mtiririko wa Fedha uliopangwa jambo ambalo linasababisha Wizara na Balozi zake kutoteketeza ipasavyo majukumu yake ya msingi, Kamati inashauri kuwa, Serikali ihakikishe kuwa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 zinatolewa kwa kuzingatia mtiririko uliopangwa.
- xii) Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza kasi ya kukamilisha upatikanaji wa Sera mpya ya Mambo ya Nje itakayojumuisha masuala ya Mtangamano wa Afrika Mashariki. Sera hii, pamoja na kwamba itaendana na hali halisi ya sasa ya Diplomasia ya kiuchumi, itaiwezesha Serikali kuwa na Mwongozo wa kutekeleza masuala mbalimbali ya Kijumuiya.
- xiii) Pamoja na Kamati kuipongeza Serikali kwa kuandaa Mpango wa miaka kumi na tano (2018/2019- 2031/2032) wa ujenzi, ununuzi na ukarabati wa majengo ya Ofisi na Makazi katika Balozi zetu. Kamati inaendelea kushauri kuwa, Mpango huu utoe kipaumbele katika kuendeleza viwanja vya Balozi ambavyo havijaendelezwa kwa muda mrefu kwani visipoendeleza vitakuwa katika hatari ya kuchukuliwa na

Serikali za nchi hizo. Viwanja hivyo ni pamoja na vile vilivyopo London, Uingereza; Muscat, Oman; Adis Ababa, Ethiopia; na Nairobi, Kenya.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambaao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba yao kama yalivyo yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard): -

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, **Mwenyekiti**
2. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
5. Mhe. Prosper J. Mbenya, Mb
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
7. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
8. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
9. Mhe. Bonnah Mosses Kaluwa, Mb
10. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb
11. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
12. Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
13. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
14. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
15. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
16. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
17. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
18. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
19. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
20. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
21. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
22. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
23. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
24. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
25. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
26. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Mhe. Prof. Palamagamba Kabudi, (Mb), Naibu Waziri, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) Katibu Mkuu Ndg. Faraji Kasidi Mnyepe, Naibu Katibu Mkuu Ndg. Ramadhan Muombwa pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano na mchango wao wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, **Mb**

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

Mei, 2019

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa tutamsikia Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani

Bungeni kuhusu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa niaba yake Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba hii iingie yote kwenye *Hansard* ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani katika Wizara ya Mambo ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili yake, kwa kuendelea kumlinda, kumtia nguvu na ujasiri wa kukabiliana na dhoruba mbalimbali za kisiasa zinazomkabili ikiwa ni pamoja na kuwekwa Gerezani kwa siku zaidi ya 100 bila kutiwa hatiani na hivi ninavyosoma leo hii Mheshimiwa Esther Matiko yuko Mahakamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakin pia niishukuru familia yangu ikongozwa na Mume wangu mpenzi, Bwana Nasibu Makaka nasema kila alipo Mwanamke aliyefanikiwa nyuma yake yuko Mwanaume.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia wasaa huu kuishukuru sana na kuipongeza Jumuiya ya Kimataifa na hususani Umoja wa Ulaya na Ubalozi wa Marekani hapa Nchini kwa kuendelea bila kuchoka kupaza sauti dhidi ya vitendo viovu vya ukandamizajji wa demokrasia na haki za binadamu na dhidi ya vitendo vyenye sura ya ugaidi, utekaji, utesaji, majaribio ya mauaji na mauaji ya viongozi wa kisiasa hasa wa vyama vya upinzani katika Mataifa mbalimbali Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajadili uhusiano wa kimataifa tukiwa katika zama mpya za utandawazi na soko huria ambapo nguvu ya soko ndiyo inayoendesha uchumi

na kuamua mustakabali wa nguvu za madola mbalimbali duniani...

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna utaratibu naomba ukae kidogo. Mheshimiwa *Chief Whip*, Mheshimiwa Jenista Mhagama.

KUHUSU UTARATIBU

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Naibu Spika, tunaendelea kupokea taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Aanze kifungu cha nne na atakapomaliza hapo ataingia kifungu cha tano na sita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie utaratibu wa Kanuni ya 64(1)(a) lakini nitatumia pia Kanuni ya 53(8) na hasa katika yale masuala ambayo Bunge lako tukufu ilikwisha kuyafanya maamuzi lakini pia nitataka uthibitisho wa maeneo mbalimbali na vinginevyo ningeomba kifungu cha tano na sita na hata kile cha saba viweze kuondolewa kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayasema hayo na kwa sababu Kanuni ya 63 inanitaka nithibitishe na *ku-prove wrong* katika yale ambayo yansemwa kwenye Kifungu cha 5 na cha 6, ninaomba niseme mambo yafuatayo:-

Katika kifungu cha 5 bado Kambi hiiya Upinzani imeendelea kuituhumu Serikali yetu kwamba inaendelea kuhangai ka kuficha ukweli wa report ya *IMF* ili kuufanya uchumi wetu utafsiriwe katika tafsiri ambayo kwa mtazamo wao nadhani wanaona siyo sawa kitu ambacho siyo kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapo ninaomba kulikumbusha Bunge hili kwamba Serikali kupitia Wizara ya

Fedha ilishatoa taarifa ndani ya Bunge hili kwamba Serikali yetu inaendelea na majadiliano na *IMF* na ninaomba kuku hakikishia hapa ninaposimama leo kama *Chief whip* wa Serikali ninafahamu kwamba timu ya *IMF* iko ndani ya Nchi ya Tanzania na tunaendelea na majadiliano kuhusu jambo hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienfdelea kuacha tu Msemaji wa Kambi ya Upinzani auchukue chukue tu maneno na kuyaweka hapa kwamba eti tunaendelea kuificha hiyo *report* siyo jambo la kweli na siyo jambo sahihi kwahiyo naomba jambo hili liondolewe. Lakini hata hivyo, kwa mujibu wa Kifungu cha 58(8) jambo hili lilihataloewa maamuzi ndani ya Bunge kwahiyo halikupaswa kabisa kuletwa tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kile Kifungu cha 6, tunaambiwa kwamba Serikali hii imetia fora kwa utawala usiozingatia Sheria, kukanyaga Katiba, Haki za binadamu na demokrasia na ndiyo hoi, iko *ICU*. Kwa kweli kwa heshima kubwa maneno haya ukiacha kwamba kuyachukulia ni maneno ya kiuchonganishi na ni maneno ambayo kwa kweli ya kuipaka Serikali yetu mambo ambayo kidhahiri shahiri siyo sawa sawa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mifano michache; kama Taifa hili lingeendelea kuwa ni Taifa ambalo liko *ICU* kwenye masuala ya Haki za Binadamu, Demokrasia na mambo mengine yaliyosemwa, *East African Court of Justice* isingekuwa bado iko katika Nchi ya Tanzania pale Arusha. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika isingeendelea kuwepo hapa Arusha ingeshaondolewa na ingeondoka, lakini vilevile *International Residual Mechanism for Criminal Tribunals* bado iko hapa kwa ajili ya Nchi ya Rwanda bado iko hapa Arusha-Afrika, lakini tunazo Mahakama zetu za mfumo wa Kimahakama ndani ya nchi kuanzia Mahakama za chini mpaka Mahakama Kuu mahali ambapo kila Mtanzania ana uwezo wa kudai haki na Demokrasia. Lakini ana-conclude kwa kusema kwamba hayo

yote yametupelekea sisi kunyimwa misaada na ame-*quote* hapo chini vijarida ambavyo ndiyo uthibitisho wa hicho anachokizungumza. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa mahusiano ya Kidiplomasia katika Sera za Fedha ni majadiliano kati ya Nchi na Nchi kwa kutumia Sheria na taratibu zilizowekwa. Sisi ndani ya Serikali tunafahamu, tunayaheshimu kabisa Mataifa haya makubwa yanayosaidia Taifa letu na tunajua, tuko tunaendelea na mazungumzo nao katika jambo moja na jingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa atuambie ametumwa na hivi vijarida kuja kuleta hizi habari ambazo sisi tunajua bado tuna mahusiano mazuri na haya Mataifa na bado tunaendelea na majadiliano nao katika mambo mbalimbali na hasa kwenye masuala ya Sera za fedha anazozisema. Kwa hiyo, haya mambo kwa kweli hayakubaliki ndani ya Bunge kwa kutumia kanuni nilizozisema, yaondolewe kwenye hotuba hii, yanachafua mahusiano yetu na utaratibu mwingine wa kimahusiano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Salome Makamba alikuwa anawasilisha taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani na katika kusoma kwake taarifa ambayo sote tunayo, Mheshimiwa Jenista Mhagama amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(a) inayosema kwamba "Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli". Ameenda mbali na kutupeleka kwenye Kanuni ya 63 inayozungumzia kutookusema uongo Bungeni na kwakuwa Kanuni ya 63 inamtaka anayemshutumu ama anayesema kwamba Mbunge mwingine anatoa taarifa za uongo ndiye anayepeswa kuonyesha uongo huo uko katika maeneo gani.

Ametoa maeleo kwa kirefu ambayo sikusudii kuyarudia lakini pia ametupeleka kwenye taarifa hii ya Mheshimiwa Salome Makamba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, ametupeleka pia kwenye Kanuni ya 53(8) inayozungumzia

Mbunge kutokufufua jambo lolote ambalo Bunge liliwishakuliamua ama katika Mkutano huo uliopo ama uliotangulia ama pia jambo ambalo linaweza kuja baadaye pia halitakiwi kuletwa na Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Jenista amesimama akieleza kuhusu taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye Kifungu cha 5,6 na 7 kabla hakijaanza kusomwa kwa sababu ya maelezo aliyojatoa na mimi kwa sababu taarifa hizi za *IMF* zilishatolewa humu na Mheshimiwa Waziri na Bunge lilihajulishwa kuhusu jambo hili na kwa mujibu wa kanuni hiyo ya 53(8), Kifungu cha 5 hakitaingia kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Lakini pia ametoa maelezo kuhusu kifungu cha 6 na kuonyesha kwamba taarifa zilizopo kwenye Kifungu hiki siyo za kweli kwa mifano allyoitoa yeye Mheshimiwa Jenista Mhagama na kwa kuwa kwenye eneo hili la 6 hakuna mahali ambapo taarifa hii inaonyesha uthibitisho wa kuonyesha demokrasia iko kwenye chumba cha wagonjwa mahututi basi hiyo sehemu ya sita pia itaondolewa.

Kuhusu sehemu ya saba, inazungumzia kuimbia Serikali kuhusu illichokifanya na ambacho kimeipandisha hadhi nchi yetu mifano imetolewa pia hapa na Mheshimiwa Jenista kuonyesha kwamba ziko taarifa mahususi zinazoonyesha Serikali na mambo inayoyafanya basi inafanya vizuri kwenye medali za Kimataifa. Kwa sababu hiyo, mwongozo wangu kwa kutumia hiyo Kanuni ya 53(8), Kanuni ya 63(5)(6) na (7) hakitaingia kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge. Mheshimiwa Salome Makamba!

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Sasa ukisema utaratibu maana yake unanipa mimi kwa sababu hakuna anayezungumza sasa, karibu usome.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni yetu ya 72 imetoa maamuzi kwamba uamuzi wa Spika ni wa mwisho. Spika alisimama hapo hapo kwenye Kiti ulichokalia akisema kwamba ni marufuku ku-*edit* hotuba za Upinzani.

Lakini kana hiyo haitoshi, shutuma ninazopewa kwa mujibu wa Kanuni ya 63 na nitaisoma, ni heri tupoteze muda lakini twende kwa kufuata taratibu na Kanuni tulizojiwekeea. Inasema "bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge ni marufuku kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge yoyote anapokuwa akisema Bungeni ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au kubahatisha" (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, paragraph yangu ya sita na ya saba nimeiweka kwenye *foot note*, ninayo *quotation*, nina *authority* inayothibitisha kweli kwamba...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome naomba unyamaze kidogo rudi pale ukae.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 5 inayozungumzia Mamlaka ya Spika, fasili ya 4 nitawasomea, inasema hivi; "Mbunge yoyote ambae hataridhika na uamuzi wa Spika anaweza kuwasilisha sababu za kutokuridhika kwake kwa Katibu wa Bunge ambaye atawasilisha malalamiko hayo kwa Spika". Kanuni hii inakusudia kwamba Bungeni, Kiti, Spika, Mwenyekiti au Naibu Spika anapotoa maamuzi hapa mbele hawezি kubishana na Mbunge. Kwa sababu hiyo, ndiyo maana Kanuni ya 5(4) imetoa fursa kwa Mbunge ambaye hakubaliani na maamuzi ya kiti ili kutoleta ubishani kati ya kiti na Mbunge inataka awasilishé hayo malalamiko yake kwa Spika na ukiisoma Kanuni hii inavyoendelea Spika ataitisha

Kamati ya Kanuni kwa ajili ya kuangalia hayo ambayo hayajaka sawa. (*Makofî*)

Kwa maana hiyo uamuzi uliotoka hapa mbele Mheshimiwa Salome Makamba huwezi kuanza kujitetea ama kubishana nao kwa mujibu wa Kanuni, kwa sababu hiyo Waheshimiwa Wabunge tutaendelea.

Mheshimiwa Salome Makamba. Umalizie namba nne uliyokuwa ukiiisoma halafu utaeleke namba nane. (*Makofî*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru naomba unitunzie muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajadili uhusiano wa Kimataifa tukiwa katika zama mpya za utandawazi na soko huria ambapo nguvu ya soko ndio inayoendesha uchumi na kuamua mustakabali wa nguvu za madola mbalimbali duniani. Kwa maneno mengine nguvu za kiuchumi ndizo zinazolipa Taifa nafasi ya kuheshimika na kuthaminiwa mionganî mwa mataifa mengine pamoja na uchumi wa soko huru, utawala wa sheria unaoheshimu haki za binadamu na demokrasia ya kweli ni nguzo muhimu na utandawazi ambako ndiko ulimwengu uliko sasa na ndiko unakoendelea kuwa na ndiko utakako kuwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia hiyo ndio umeifuta? Nashukuru niende wapi naomba unieleze.

NAIBU SPIKA: Nenda B.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania imekuwa na kigugumizi cha kuridhia mkataba wa makubaliano ya eneo huru la biashara Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali inajinasibu kutekeleza diplomasia ya uchumi na kwa kuwa mkataba huu ni fursa nyingine ya kuinua kiwango cha kibashara ndani ya Afrika hasa kwa mataifa yanayoipanga kimkakati, ni jambo lisiloelezeka kuona mpaka sasa Tanzania imekumbwa na kigugumizi kikubwa juu ya makubaliano haya na hivyo kutowasilisha Bungeni kuridhiwa na hatimaye kuwasilisha nyenzo za utekelezaji wake kwa Kamishna wa Umoja wa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Taifa makini, mkataba huu ni hitaji la muda mrefu ambao ni fursa kwa uchumi wa Taifa hili kukua kwa kasi na kusaidia kupunguza kiwango cha umaskini. Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kukuza uchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani kuititia CHADEMA imeeleza bayana katika Sera yake ya Mambo ya Nje Sura ya 12.1 kuhusu namna ambavyo uhusiano wa kimataifa utatumika kujenga diplomasia ya uchumi. Sera hiyo inasema kama ifuatavyo; "CHADEMA itaweka sera ya mambo ya nje ambayo itazingatia masuala ya uchumi, ulinzi, diplomasia na masuala mengine muhimu katika uhusiano wa kimataifa. Balozi za Tanzania zitakuwa na jukumu la kufanya diplomasia ya uchumi kwa kuwavutia wawekezaji na mitaji kutoka nje bila kuathiri ulinzi na maslahi ya nchi". (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba mkataba huu wa kibashara ni nyenzo muhimu ya kukuza mahusiano yetu na mataifa mengine Barani Afrika hasa yale ambayo sio ya *East African Community* na *SADC* ambamo sisi ni wanachama. Aidha, tunaona kwamba mkataba huu ni muhimu ya kukuza uchumi wa Watanzania na Taifa letu kwa ujumla kwani inatoa fursa kwa watu wetu kufanya biashara kwa urahisi zaidi na wenzao Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba kuendelea kuchelewa kwa Serikali kuleta mkataba huo ili uridhiwe na Bunge, ni kuendelea kuchelewa kuchangamkia fursa za biashara jambo ambalo halina afya kwa maendeleo kwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika Serikali Kuingia Mkataba na Kampuni Hewa kutoka Nje kununua Korosho na kuwasababishia wakulima wa korosho hasara kubwa.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha Serikali...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna utaratibu, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha. Mheshimiwa Salome Makamba naomba ukae.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 63(3) inayohusu utaratibu, lakini Kanuni iliyovunjwa ni Kanuni ya 53(8) naomba niisome; "Mbunge yoyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge liliwkishakuliamua ama katika mukutano huo uliopo au ule uliotangulia."

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kwenye hotuba hii ya Kambi ya Upinzani kuhusu jambo hili anachotaka kukizungumza namba 15,16,17 mpaka 21 jambo hili limekwhisha kuamuliwa kuititia Wizara zilizopita za Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo kulileta jambo hili tena Bunge liamue ni kuvunja Kanuni hii, kwa hiyo, naomba maeneo haya yote yaondolewe 15,16,17,18,19, 20 na 21. Ahsante. (*Makofii*)

MBUNGE FULANI: Kulipwa hatujalipwa.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha akisema anatumia

Kanuni ya 63(3) inayosema Kuhusu Utaratibu na wakatupeleka kwenye Kanuni ya 53(8).

Waheshimiwa Wabunge, kwanza Kanuni ya 63(3) inazungumzia mtu aseme Kuhusu Utaratibu jambo ambalo anaona linasemwa ni la uongo, lakini katika maeleo yake hajaonesha huo uongo kwa Mheshimiwa Salome Makamba uko wapi yaani kwenye hii taarifa yake isipokuwa ametupeleka kwenye Kanuni ya 53(8) kuonesha kwamba jambo hili lilikwishakuzungumzwa humu Bungeni kuitia maamuzi ambayo Bunge imeshalifanya kwenye taarifa za ama kwenye hoja za Wizara mbalimbali Wizara ya Kilimo na ya Viwanda na Biashara.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni hii nimetoka kuisoma wakati akizungumza Mheshimiwa Jenista hii Kanuni ya 53(8) na taarifa hii iliyoko hapa inazungumzia ununuzi wa korosho na huu mkataba ambao ulishajadiliwa hapa ndani na maamuzi yalishatoka. Kwa hiyo kwa mujibu wa hii Kanuni ya 53(8) taarifa hii haikupaswa kuwekwa kwenye hoja tena kwa sababu ilishatolewa maamuzi, lakini pia ilishatolewa ufanuzi na Wizara na hatuwezi kuwa kila siku tunazunguka hapo hapo.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa hiyo Kanuni ya 53(8) maeleo yaliyoko kwenye "C" yote yanaondoka ili tuweze kusonga mbele kwa mujibu wa Kanuni zetu tulizojiwekea wenyewe. Mheshimiwa Salome Makamba endelea na "D." (*Makofii*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, niongoze unapotaka nisome.

Mheshimiwa Naibu Spika, Siasa za Ndani na Taswira ya Nchi Kimataifa; tangu Serikali ya Awamu ya Tano kuingia madarakani mwaka 2015, kumekuwepo na ongezeko kubwa la ukiukwaji wa haki za binadamu, uminywaji wa demokrasia

na uvunjwaji wa sheria mbalimbali tulizojiwekea wenyewe kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matukio ya utekwaji wa watu mbalimbali hasa wanaonekana kuikosoa Serikali, kupotezwa watu pasi hatua madhubuti kuchuliwa na vyombo vy'a dola, majoribio ya kuuwawa kwa viongozi wa kisiasa na kuminywa kwa uhuru wa vyombo vy'a habari ni mambo ambayo yanaichafua Tanzania kwenye ulimwengu wa kimataifa. Kwa kipindi hiki, Serikali ya Tanzania imegonga vichwa vy'a habari vy'a kimataifa si kwa uzuri wala ukarimu wake kama ilivyokua imezoleka, bali kwa ukatili dhidi ya raia wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya haki za binadamu ya *State Department* ya Marekani kwa mwaka 2018 inaonesha hali ya hatari kwa Tanzania kwa kubainisha matukio ya mauaji, kutekwa na kupotezwa kwa watu, uvunjifu mkubwa wa Katiba ya nchi pamoja na ukandamizwaji mkubwa wa Vyama vy'a Upinzani. Hali hii pia inashajihishwa na ripoti ya *Freedom House* kwa Tanzania kwa mwaka 2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mambo haya sio tu yameichafua na yanaendelea kuichafua Tanzania bali yana athari za moja kwa moja Taifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi ni kudorora kwa shughuli za kiuchumi; ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa kiwango kikubwa unategemea na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi (*Foreign Direct Investment*). Taarifa ambazo ziko kwenye Ripoti ya *IMF* zinaashiria kuperomoka kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania kutoka 7.1% mwaka 2016 hadi asilimia sita mwaka 2018. Hii maana yake ni kwamba kumekuwepo na kuzorota kwa shughuli za uzalishaji nchini zinazotokana kwa kiasi kikubwa na uwekezaji wa makampuni ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huu, taarifa ya *UNCTAD* (*United Nations Conference on Trade and*

(Development) ya uwekezaji duniani ya mwaka 2018 inaonyesha kwamba kuna anguko la asilimia 14 la kiwango cha uwekezaji kwa Tanzania. Anguko hili ni kielelezo cha kwamba wawekezaji wanakimbia Tanzania kutokana na mambo ya hovyo, yasiyo ya kibinadamu yanatokea chini ya utawala huu pasi na hatua madhubuti kuchukuliwa na zikaonekana kweli zinachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatafsiri kuporomoka kwa kiwango cha mitaji ya uwekezaji (*Foreign Direct Investments*) nchini kama kielelezo cha Serikali hii ya CCM ya Awamu ya Tano kushindwa kutelekeza kwa vitendo diplomasia ya uchumi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kukimbia huku kwa wawekezaji kunatokana, pamoja na mambo mengine, vitendo viovu wanavyofanyiwa raia wa Tanzania na watu ambao mpaka leo Serikali ni ama inawajua na haitaki kuwachukulia hatua ama haina uwezo wa kuwabaini na kuwachukulia hatua na hivyo kutishia usalama mpana wa raia na mali zao. Aidha, maelezo ya kujichanganya yanayotolewa na vyombo vya dola dhidi ya matendo haya yanaongeza hofu zaidi kwa raia yoyote nchini kuishi kwa amani na kufanya kazi zake kwa utulivu. Kwa mazingira haya hakuna mwekezaji makini atakayetekeleza mitaji yake kuwekeza sehemu ambapo Serikali inashindwa kutoa uhakika wa usalama kwa raia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Shiriki la Bartelsmann ya Ukanda wa Afrika yenye kichwa cha habari "*A Divided Content*" ya mwaka 2018 inataja uchumi wa Tanzania kuanza kusinyaa kuanzia mwaka 2016. Ripoti hiyo inabainisha kwamba kusinyaa huku kunatokana na maamuzi juu ya uchumi yanayotokana na mihemko na sifa za kisiasa kuliko uhalisia (*Populism*). Ripoti hiyo inaweka bayana kuwa mambo haya yameshusha morali ya wawekezaji kutoka nje na uungwaji mkono wa jumuiya ya kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika,...

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba kuna utaratibu. Mheshimiwa Kingu.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. ELIBARIKI I. KINGU: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni 64(1)(g) na (f) sitasoma kwa ajili ya kuokoa muda.

Mheshimiwa Mbunge ametumia maneno ambayo kimsingi ninamheshimu dada yangu Salome Makamba lakini sio maneno ya Kibunge maneno kama mihemko, mimi nafikiri maneno haya yaondolewe hasa ukizingatia utekelezaji mkubwa unaofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi katika miradi mbalimbali ya kiuchumi, Serikali ya Chama cha Mapinduzi inatekeleza miradi ya muhimu ambayao *economic impact* yake itatokea na itaonekana katika vizazi vijavyo na itakuwa historia katika Taifa letu. Kwa hiyo naomba maneno mihemko yafutwe si maneno yenyе staha, si maneno ya Kibunge. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Kingu kwenye Kanuni ya 64 ametaja fasili ya (1)(f) na (g)akionesa kwamba wakati Mheshimiwa Salome Makamba akisoma taarifa yake kwenye kifungu cha 30 ametumia lugha ya kuudhi na inayodhalilisha watu wengine, kwa kuwa amesema maamuzi juu ya uchumi yanatokana na mihemko na sifa za kisiaza kuliko uhalisia, sasa Mheshimiwa Salome amesema maneno haya anayatoa kwenye hii taarifa ya huyu Mjerumani kwamba ye ye ndiye aliyeyasema haya maneno.

Sasa kama ye ye anachukua hayo maneno kwenye hiyo taarifa na ye ye ame amua kuyatumia hapa nadhani kwa kuwa hatuna hiyo taarifa ye ye ametuandikia hapa kwamba tukaisome hiyo taarifa.

Sasa maana yake si maneno yake ni maneno ya hiyo taarifa ambayo ye ye ameamua kuisoma. Kwa hiyo, kifungu namba 30 ambacho Mheshimiwa Salome Makamba anasema amesoma kwenye taarifa hiyo na ndicho ambacho kinasemwa kwenye hiyo taarifa pengine mtu atusaidie kutafuta hii taarifa halafu aseme kama ndicho kinasemwa mle au hapana, lakini kwa mujibu wa Kanuni zetu kwa sababu ametoa kwenye hiyo taarifa mahususi ambayo ameandika hapa hii sehemu ya 30 itabaki kama ilivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Salome Makamba. (*Makofi*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya ripoti hiyo inasema kwamba; naomba kunukuu "... *In a small but significant number of states including Tanzania and Zambia, this was compounded by the emergence of populist leaders who sought to intervene in the economy for political as much as economic goals, undermining investor confidence. One consequence of these changes has been the failure to effectively harness potential international support.*" (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuiarifu Serikali hii ya CCM, kama ilikuwa haijui ndio ijue sasa kwamba kufanikiwa au kutofanikiwa kwa sera ya nje ya nchi yoyote duniani kunatokana na jinsi nchi hiyo inavyoendesha siasa zake za ndani. Siasa za ndani zina athari ya moja kwa moja na mahusiano ya nchi na Jumuiya ya Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kudorora kwa mahusiano baina ya Tanzania na Jumuiya ya Kimataifa ni sababu ni madhara mengine ya utawala huu. Kuongezeka kwa matendo ya utekaji wa raia, kupotezwa kwa watu bila maelezo yanayoleweka ya Serikali, majaribio ya kuua bila wauaji kutiwa nguvuni, kuonewa na kukandamizwa kwa vyama vya upinzani nchini kumepelekea wadau mbalimbali

wa kimataifa kupaza sauti zao kukemea matendo haya. Hata hivyo Serikali imewaona wadau hawa kama maadui wa Taifa na hivyo kuweka mbinyo juu yao. Hili linadhihirishwa na mahusiano mabovu yaliyoko kati ya Tanzania na Jumuiya ya Ulaya ambayo imekiri kuwa ilimwita Balozi wake kurudi Ubelgiji kutokana na shinikizo la Serikali ya Tanzania juu yake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutikisika kwa mahusiano baina ya Tanzania na Umoja wa Ulaya hakuwaathiri viongozi wa CCM bali wananchi wanaonufaika na misaada ya jumuiya hii katika maeneo mbalimbali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuelewa kwamba hakuna Serikali duniani inayoweza kufanikiwa bila kuwa na mahusiano na mataifa mengine. Ni bahati mbaya sana kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inagombana mpaka na wahisani wanaoipatia misaada ya kibajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge na Taifa, ni kwa nini ilimuwekea shinikizo Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini hata kupelekeea kuondoka kwake? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa pia kujua ni kwa nini Serikali hii ya Awamu ya Tano imeanza kuwa na tabia ya kuziingilia na kiziwekea mashinikizo Balozi zinazoziwakilisha nchi zao katika utendaji wao wa kazi ikiwa haziendi kinyume na Mkataba wa Vienna? Hata kama Serikali inaona Balozi hizo zimekuwa zikikiuka Mkataba wa Vienna katika utendaji wao wa kazi, Bunge linapaswa kuelezwaa ni mambo gani hayo Balozi hizo zimekuwa zikifanya mpaka kustahili mashinikizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kanzidata ya Watanzania waishio nje ya nchi (*Diaspora Database*). Dunia sasa inatambua mchango mkubwa wa uchangiaji uchumi unaofanywa na watu mbalimbali wanaoishi nje ya nchi zao yaani *diaspora*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna takwimu za kitaifa zinazoonyesha idadi kamili ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi na taarifa za kile wanachokifanya huko. Umuhimu wa kuwa na taarifa ni kubaini kwa wepesi idadi na aina ya watu wenye ujuzi na uzoefu ambao Serikali inaweza kuutumia kwa maslahi ya nchi. Aidha, kujua idadi ya wananchi walio nje ya nchi kutapelekea kutengeneza milango ya kiuchumi kati yao na nchi yaani *economic gateway*, kutafungua fursa za kibashara ikiwa ni pamoja na soko la nje yaani *export market* kwa bidhaa zetu za Kitanzania na hivyo kutaachia fursa kwa soko la ndani kuboresha bidhaa zao ili ziweze kupata masoko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza uwepo wa kanzidata hiyo kwa kuwa *diaspora* ina mchango muhimu katika kukuza uchumi wetu, kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, Watanzania waishio nje waliochangia 0.8% ya *GDP* yetu kwa kutuma kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 430 kwa mwaka 2018. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kwamba ni muhimu kuwa na takwimu za Watanzania waishio nje sambamba na shughuli wanazofanya ili iwe rahisi kufanya makisio ya fedha zitakazopatikana yaani (*diaspora remittance*) na kuziingiza kwenye bajeti ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utengenezaji wa kanzidata hiyo uende sanjari na kutungwa sheria na sera mpya itakayoruhusu watanzania kuwa na haki ya uraia pacha ambao utamwezesha mtanzania aishiye nje kuwekeza kwa uhuru nje ya nchi na hapa nyumbani. Kumzuia Mtanzania anayeishi nje kuwa na uraia pacha ni kumwekea shinikizo la kutowekeza kikamilifu nje kwa kuwa anaishi kule kama mgeni na kwa sababu hiyo mchango wake wa fedha hapa nchini utakuwa pia wa mashaka kutoptana na kutokuwa na uhuru wa uwekezaji mkubwa nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la uraia pacha kwa dunia ya leo ni fursa. Kimkakati uraia pacha ni kichocheo cha maendeleo kwa Taifa. Mathalan kwa majirani zetu wa Kenya wenye uraia pacha diaspora yao imechangia kiasi

cha Dola za Kimarekani milioni 2,720 kwa mwaka 2018 sawa na 3% ya pato lao la Taifa. Hii ni kutokana na Wakenya wenye uraia wa nchi nyingine kuwa na confidence ya kuwekeza nyumbani bila ya bughudha ya aina yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa uraia pacha kwa Watanzania na wasio Watanzania hauko tu kwenye michango ya kifedha, bali upatikanaji wa ujuzi na maarifa (*skills*) mbalimbali kutoka kwenye Mataifa mengine ambapo ni vigumu kupatikana Tanzania na mazingira yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu huo wa uraia pacha, Sera ya CHADEMA inasema, nanukuu: "CHADEMA itaanzisha sera na kutunga sheria kuruhusu uraia pacha ikiwa ni pamoja na kuwahimiza Watanzania wanaoishi nchi za nje kuwekeza. Aidha, itaweka utaratibu wa hati fungani ambazo zitaongeza hifadhi ya fedha za kigeni nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Msimamo wa Tanzania Katika Kupinga Ubeberu, Ukoloni na Uonevu Duniani; nchi yetu imekuwa na historia iliyotukuka duniani ya kuwa mstari wa mbele kupinga aina zote za uonevu, unyonyaji na utumwa hususan ubeberu na ukoloni.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakumbuka kwamba Tanzania ndiyo ilikuwa muasisi wa nchi za Mstari wa Mbele chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere katika miaka ya 1960 kwa lengo la kupinga ubaguzi wa rangi na utawala wa wazungu wachache katika nchi za Kusini mwa Afrika. Tanzania ilienda mbele zaidi hadi kufikia hatua ya kuvunja mahusiano yake ya kidiplomasia na Mataifa mengine yaliyokuwa na tabia ya ubaguzi wa rangi, unyonyaji, ubeberu na ukoloni dhidi ya Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba Tanzania ilivunja ushirikiano wake wa kidiplomasia na Israeli kutokana na Israeli kuwa na tabia za kibeberu za kutaka kuikalia ardhi ya Palestina kwa nguvu. Aidha, Tanzania ilivunja

mahuiano yake na Morocco kutokana na nchi hiyo kuikalia Sahara ya Magharibi kwa nguvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ilipingga utawala wa ki-dikteta mionganini mwa nchi za Afrika kwa kuwa udikteta ulikuwa na tabia zote za unyonyaji, ubaguzi na uonevu, mambo ambayo Watanzania hawakuamini katika hayo. Ndiyo maana Tanzania kwa wakati huo haikumuunga mkono Mobutu Seseko wa iliyokuwa Zaire na sasa Kongo DRC, haikumuunga mkono Muammar Gaddafi wa Libya na pia ilimng'oa madarakani dikteta wa Uganda Idi Amin Dada. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, siku za hivi karibuni tumeshuhudia nchi yetu ikuhuisha mahusiano ya kidiplomasia na nchi nilizozitaja ambazo hapo awali tulikuwa hatuna mahusiano nazo kutokana na kukalia Mataifa mengine kimabavu au kufanya uonevu dhidi ya Mataifa mengine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza Bunge hili, ni sababu zipo zimesababisha Tanzania kubadili msimamo wake huo kuhusu ushirikano na mataifa hayo? Je, Morocco imeacha kuikalia kimabavu nchi ya Sahara Magharibi? Je, Israeli imeacha kuionea Palestina? Kama Serikali imebadili msimamo: Je, mabadiliko hayo ya msimamo yaliridhiwa na Bunge hili lini? (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Brexit na Athari Zake kwa Watanzania. Tanzania haijajiaandaa kukabiliana na Brexit. Inafahamika kuwa Tanzania ni mshirika wa kibashara na EU, lakini imekuwa na mahusiano na UK ambayo wananchi wake walipiga kura ya maoni kuamua kujitoa katika Umoja wa Ulaya.

Katika hali hiyo Tanzania haijaonesha kwa uwazi kuwa itakuwa upande upi, hasa ukizingatia kuwa hatujasaini mkataba wa kibashara na EU maarufu kama EPA na ambapo nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wameonesha wazi kuwa watasaini na kuiacha Tanzania na Burundi nje ya mkataba huo. Kambi Rasmi inataka kujua msimamo wa Serikali juu ya Brexit.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tishio la kusambaratika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Nchi ya Tanzania...

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: haijaonesha...

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba unitunzie muda wangu tafadhali. Nakuomba sana.

NAIBU SPIKA: Wanakutunzia bila shaka. Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. GOODLUCK A. MLINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kipengele ambacho anaenda kukisoma Mheshimiwa Salome Makamba kinavunja Kanuni ya 64(1)(a). Siyo tu kuvunja na hata kuharibu mahusiano yetu na Nchi za Afrika Mashariki na pia kuleta uchochezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, paragraph ya 57 kinasema: "Nchi ya Tanzania haijaonesha kwa vitendo wala kisera nia thabiti kuunga mkono kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki", kitendo ambacho ni uongo. Paragraph ya 58, "Jumuiya ya Afrika Mashariki ipo hatarini kusambaratika," kitu ambacho ni uongo na 59 hivyo hivyo, 60 na 61. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo kwa sababu, Kanuni inanitaka ya 63(4) kuthibitisha anayoyasema haya kuwa ni uongo; moja, katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kwanza hakuna Itifaki ya *Free Movement* bali kuna kipengele kimojawapo cha *protocol* katika Soko Huru. La pili, hakuna *visa* inayotozwa. *Visa* zinazotozwa ni kwa wale wanaofanya biashara au kufanya kazi. Badala ya kulipa *business pass* tunalipa *working permit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kwenye suala la biashara tumeshuhudia iko *Equity Bank* ina *branch* mpaka Dodoma, iko *Kenya Commercial Bank* mpaka Dodoma; pia kwenye siasa tulishuhudia Mheshimiwa Lowassa alienda kufanya kampeni ya Uchaguzi Mkuu kumfanya Mheshimiwa Uhuru Kenyatta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kijamii tumeshuhudiana Watanzania wakioa Wakenya. Kwa mfano, *Diamond Platinum* kaoa Mkenya na Ali Kiba ameoa Mkenya. Pia Mheshimiwa Kenyatta alitoa shilingi milioni 125 kusaidia majanga Tanzania meli ilipozama. Pia, walimu asilimia 70 wa *English Medium* hizi za *primary* ni Wakenya. Kwa hiyo, mahusiano siyo mabaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa muktadha huo, naomba *paragraph* ya 57, 58, 59, 60 na 61 viondolewe kwenye *Hansard*. Siyo kusema uongo tu, vinaleta uchochezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Goodluck Mlinga kwa mujibu wa Kanuni ya 64 fasili ya (1)(a) ambayo inazungumza kwamba, "Mbunge hatatoa ndani ya Bunge Taarifa ambazo hazina ukweli." Amejaribu pia kutumia Kanuni ya 63(4) kwamba, mifano aliyoitoa ambayo sikusudii kuirudia, inathibitisha kwamba hii taarifa iliyotolewa kuhusu tishio la kusambaratika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo ipo kwenye Taarifa ya Mheshimiwa Salome Makamba kwamba ni ya uongo.

Waheshimiwa Wabunge, nikiipitia hii taarifa, haioneshi pia taarifa hizi Mheshimiwa Salome Makamba amezitoa wapi kuonesha kwamba kuna kusambaratika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia ukiipitia vizuri anazitaja nchi mbalimbali ambazo kwa maelezo yake anasema zina mahusiano baridi ama hazina mahusiano mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu, taarifa kama hii inaingia kwenye Taarifa zetu Rasmi za Bunge na mahusiano yetu na nchi hizi ni yale ambayo Serikali inakuwa imeshaweka wazi; kwa kuwa taarifa hii ya Mheshimiwa Makamba haijasema yeye amezitoa wapi kujua kwamba kuna mahusiano baridi kati ya Rwanda na Uganda, kuna mahusiano baridi kati ya Rwanda na Burundi, taarifa hizi haziwezi kupokelewa na Bunge na kuwepo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofi*)

Kwa sababu hiyo, kwa kutumia kanuni hizo hizo mbili, Taarifa iliyoko kwenye (h) inayohusu Tishio la Kusambaratika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa, haijaonesha taarifa hizi zimetoka wapi inaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Mheshimiwa salome Makamba 63. (*Makofi*)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: *Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu unyanyapaa dhidi ya Uangalizi wa Kimataifa wa Uchaguzi Mkuu 2020. Ni utaratibu wa Kimataifa kuwa waangalizi wa Kimataifa wa Uchaguzi katika nchi nyiningine kwa lengo la kuhakikisha kuwa chaguzi zinakuwa huru na za haki. Pamoja na uhalisia huo na licha ya nchi yetu kufanya hivyo mara nydingi...[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA

MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
...safari hii kuna dalili za wazi kuwa Serikali ya CCM kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi kutowaalika waangalizi hao kuja kutazama mwenendo wa Uchaguzi Mkuu wa 2020. (Makof) [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, kuna utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi...

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara, Kanuni iliyovunjwa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waitara, Kanuni iliyovunjwa.

KUHUSU UTARATIBU

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 63(3) na niende kwenye (4) na (5). Taarifa ambayo Mheshimiwa Msemaji wa Upinzani

anaisoma, kipengele cha 63, 64, 65 na 66 kina mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza Bajeti ya TAMISEMI ambayo inahusiana na mambo ya Serikali za Mitaa, Bajeti ya Waziri Mkuu ambayo inahusika na Uchaguzi Mkuu ilishapita. Kwa hiyo, ukienda kwenye kanuni ya 53(8) mambo haya ya Uchaguzi Mkuu yalisha amuliwa na bajeti imeshapitishwa na Bunge hili tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ukisoma Kifungu kwa mfano cha 63 Msemaji anasema kuna dalili za wangalizi wa Kimataifa kuzuiliwa. Kitu ambacho tunajua, uchaguzi utakapofika, Tume ya Uchaguzi itawaalika nchi wahisani na nchi mbalimbali kuja kushuhudia uchaguzi. Uchaguzi haujafika. Hizo dalili hatuwezi kuzipima na hizi taarifa za kupotosha, hazina ukweli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipengele cha 64 anasema wangalizi hawa pia hawajapelekewa mialiko:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wenyewe kazi hii ya kupeleka mialiko kama nilivyosema ni Tume ya Uchaguzi na haijafanya hivyo, lakini sisi tutakapowaalika tutawaalika nchi nydingi zaidi ya hizi za Umoja wa Ulaya, Jumuiya ya Kimaendeleo, zimetajwa hapa; Israeli, watakuja Rwanda, watakuja *South Africa*, tutakuwa na Malawi na nchi kadha wa kadha ambazo zitaalikwa. Kwa ubaguzi huu wa kusema kuna watu wachache ambao wataalikwa, sisi kama Serikali hatusemi hivyo, hili jambo kimsingi shughuli inawahishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipengele cha tano anasema Serikali haitaki waangalizi hawa. Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi, hakuna ushahidi wowote; tumesema tupo tayari wakati ukifika wa uchaguzi waangalizi wa Kimataifa wataalikwa. Wao wanasema Serikali imesema haitaki, wamekutana wapi? Ana *document* gani? Ana barua gani? Ni ofisi gani? Afisa gani ambaye amesema kwamba Serikali haitawaalika Waangalizi wa Kimataifa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha saba anasema kwamba, hapa kuna mizengwe. Tumesema uchaguzi wa mwaka 2020 haujafika. Sasa hii mizengwe ambayo inazungumzwa leo kwenye bajeti ya mwaka 2019 mwezi wa Saba ni mizengwe ipi? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sababu hizo mbili, ni kwamba suala la uchaguzi bajeti tumeshatenga kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu, lakini pia hizi taarifa ambazo kwa kweli ni za uongo, ni za kughushi, haziwezi kuthibitika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa heshima kubwa Kiti chako kiondoe taarifa hii. Vinginevyo kama anaendelea kulazimisha, athibitishe Serikali imekataa kwa barua namba ngapi ya siku gani? Pia, aseme waangalizi ambaeo leo uchaguzi umefanyika hawajapewa mwaliko ni wa nchi gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilishe. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Waitara kwa mujibu wa Kanuni ya 63(3); ametaja pia fasili ya (5) akieleza kwamba taarifa inayosomwa kwenye sehemu ya (i) Kifungu cha 63, 64, 65 na 66 hazina ukweli. Ametoa maelezo kwamba pia, taarifa hii ya kuhusu mambo ya uchaguzi, Bunge hili lilishazungumza na kuamua wakati likijadili bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwa maana hiyo, matumizi ya Kanuni ya 53 fasili ya (8) yanaingia hapo tena.

Sasa nimeipitia pia taarifa hii katika kifungu hiki, katika vifungu hivi inayoonesha kwamba wako watu ama wako waangalizi wa uchaguzi ambaeo huwa wanakuja kwa kawaida; na kwa mujibu wa taarifa anayoitoa Mheshimiwa Salome Makamba hapa, ni kana kwamba, pengine yeye ana taarifa kutoka hao ambaeo huwa wanaalikwa kwamba safari hii hawajaalikwa, kwa hivyo, yeye anataka kuliaminisha Bunge kwamba Serikali ama chombo kinachosimamia uchaguzi hakina mpango wa kuwaalika watu hawa.

Sasa kwa sababu taarifa hii inakuja kwetu hapa sisi kama Bunge na tukiweka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge siyo taarifa ya ukweli, kwa sababu sisi kama Bunge hatuna taarifa hiyo. Pia, Serikali wakati ikzungmza wakati wa bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu haikuoneshwa kwamba Tume ya Uchaguzi ina mpango wa kukata watu wengine, kutokuwaalika hapa nchini.

Kwa hiyo, hoja ya unyanyapaa dhidi ya wasimamizi inakuwa haipo na kwa hiyo, kwa namna ilivyowekwa hapa inakuwa siyo ya ukweli. (*Makofii*)

Kwa sababu hiyo, kifungu hiki kinachozungumza kuhusu Unyanyapaa Dhidi ya Waangalizi wa Kimataifa Kuhusu Uchaguzi Mkuu wa 2020 kinaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Salome Makamba.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako, mimi ningombaa msome Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kabla hamjaanza kunipa Taarifa na Miongozo. Soma Kipengele Namba 64, *let us be fair*. Kipengele Namba 64 nimesema kuna dalili...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba dalili utaweza kuzithibitisha hapo? Ni dalili gani wewe ulizoziona na uchaguzi unakuwa mwakani?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome tafadhali, nimeshakusomea Kanuni ya 5(4) kuhusu maamuzi yanayotolewa na yejote anayekuwa amekalia Kiti hapa, wewe unapaswa kufanya nini. Huwezi kubishana nami nikiwa nimekaa hapa mbele. Kanuni ya tano inataka ikiwa huridhiki na yale niliyoyasema, upeleke malalamiko kwa Spika.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, uendelee kusoma taarifa yako.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MBUNGE FULANI: Endelea, endelea!

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee wapi? (*Kicheko*)

NAIBU SPIKA: 67.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dalili za ubaguzi wa itikadi za kisiasa katika Ubalozi mbalimbali, hususan Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza. Licha ya Mabalozi wetu nje ya nchi ni makada wa Chama cha Mapinduzi (sjui mtakataa na hiyo!) waliotunukiwa nafasi hizo kwa sababu mbalimbali, halondoi ukweli kwamba hao ni watumishi wa Umma na kwamba ofisi wanazofanyia kazi ni za Umma. Kwa kutambua uhalisia huo, Mabalozi hawa hawana budi kuwatumikia wananchi wote kwa usawa bila kujali itikadi zao za vyama vya siasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nime tangulia kusema hayo kwa kuwa imebainika kwamba yapo mawasiliano ya Chama cha Mapinduzi kwenye tovuti au website ya Ubalozi wa Tanzania nchini Uingereza...[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU
WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA
MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI):**
*...jambo linaloashiria kwamba Ubalozi huo unapokea
maelekezo kutoka juu ya utendaji...[Maneno Haya Siyo
Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Chumi, akiwa amesimama
hana mbele hawezi kupewa Taarifa. Wanaopewa Taarifa ni
wale ambao kuna kanuni imevunjwa. Kama hakuna kanuni
inavunjwa, huwezi kumpa taarifa akiwa hapa mbele.

Mheshimiwa...

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika,
kuhusu utaratibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU
WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA
MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:
Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mawasiliano hayo yanatoa
taswira kwamba Ubalozi huo unafanya kazi kwa kuegemea
itikadi zaidi jambo ambalo linaonyesha dhahiri...[Maneno
Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika,
Kuhusu Utaratibu.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, kuna
kuhusu utaratibu. Mheshimiwa Cosato Chumi?

KUHUSU UTARATIBU

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kuhusu Utaratibu na sitarejea Kanuni ya 64. Nami na Bunge hili linanifahamu, sina kawaida ya kusimama kuomba Miongozo au Utaratibu.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze katika kipengele ambacho anasoma.

MBUNGE FULANI: Kanuni ya ngapi?

MHE. COSATO D. CHUMI: Kanuni ya 63 nimesema Kuhusu Utaratibu na 64 kuhusu Mbunge kuzungumza mambo ambayo siyo ya ukweli. Sitazisoma zote kwa sababu tunazielewa na kila siku tunazitumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa *experience* na kwa *training*, robo tatu ya maisha yangu ya kazi nimefanya kazi Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa. Nimefanya kazi kama *Foreign Service Officer*. Vipengele anavyosoma Msemaji wa Kambi ya Upinzani; kwanza, Balozi zetu zinafanya kazi kwa mujibu wa mikataba mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo *Vienna Convention*, lakini kama haitoshi Balozi ni kiungo kati ya wananchi walioko nyumbani na kule ugenini. Ikiwa una shughuli yoyote, hauzuiliwi kuwasiliana na Ubalozi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama vile haitoshi, katika kipengele cha 69 na kipengele cha 70 ambacho kinasema kwamba kuna *link* katika *website* ya Ubalozi ya Chama cha Mapinduzi; ingia hata sasa hivi katika *website* ya Ubalozi wa Uingereza wa Tanzania nchini Uingereza uone kama kuna *link* hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu ambalo tunapaswa kufahamu kama Wabunge, tunapoishauri Serikali,

Ubalozi, kama taasisi yoyote hapa nchini ina shughuli katika ubalozi fulani haizuiwi kuwasiliana na Ubalozi wa nchi ile ili taarifa za *participants* mbalimbali ziweze kuwafikia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hebu tutumie Bunge lako Tukufu kueleza mambo ambayo yatalisaidia Taifa hili kuliko kupotosha taarifa kama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushauri wangu, maneno kama haya yanapoenda nje yanapotosha kwanza Bunge lako Tukufu na yanapotosha Taifa na yanapotosha Jumuiya ya Kimataifa. Naomba yafutwe na yaondolewe.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, Mheshimiwa Cosato Chumi amesimama kwa mujibu wa Kanuni 64, lakini pia Kanuni ya 63 akisema taarifa iliyopo katika kifungu cha 68, 69 na 70 kinazungumza taarifa ambazo si za kweli na kwamba taarifa hii kwamba ukifungua tovuti yetu ya Ubalozi wa Uingereza kuna taarifa zinaoonesha mawasiliano na Chama cha Mapinduzi na kwamba hawa makada wa chama wanaendeleza huko kazi ya Chama cha Mapinduzi na si kazi ya nchi. Mheshimiwa Cosato Chumi ameeleza kwa kirefu namna ambavyo taarifa hii inaleta upotoshaji na yeye anasema ameipitia tovuti hii na haina taarifa hii ambayo imezungumzwa hapa.

Sasa nimeipitia hii taarifa anayoisema Mheshimiwa Cosato Chumi na kama haya yanayosemwa hapa kwamba kuna huo uhusiano wa hiyo tovuti na Chama cha Mapinduzi hayapo, maana yake huu ni upotoshaji na hairuhusiwi kwa mujibu wa kanuni zetu; Kanuni ya 64(1)(a) na pia Kanuni ya 63 inazuia kusema uongo Bungeni. Kwa sababu hiyo, hii habari ya Ubalozi wa Tanzania Nchini Uingereza na taarifa iliyopo hapa kwa kuwa haina ukweli inaondolewa kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Salome Makamba...

**MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMAJI MKUU
WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA**

MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, hatuwezi kuja hapa kusema uongo na kuliongopea Taifa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: Mheshimiwa Naibu Spika, Joseph Sokoine...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Salome Makamba, taarifa inayosomwa ukiwa umesimama hapo mbele ni ile ambayo umeileta, eeh tafadhalii.

MHE. SALOME W. MAKAMBA - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA: *(Aliongea bila kutumia kipaza sauti).*

NAIBU SPIKA: Naomba Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Salome Makamba, Mheshimiwa Salome Makamba naomba urudi ukakae, naomba ukakae. *(Makofii)*

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA,
MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

A. UTANGULIZI

- Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Msemadi Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika Wizara ya Mambo

ya Nje, Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Kikanda na Kimataifa, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko (Mb) nina kila sababu ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili yake, kwa kuendelea kumlinda na kumtia nguvu na ujasiri wa kukabiliana na dhoruba mbalimbali za kisiasa zinazomkabili ikiwa ni pamoja na kuwekwa gerezani kwa zaidi ya siku mia moja bila kutiwa hatiani.

2. Mheshimiwa Spika, pili napenda kuwashukuru na kuwapongeza sana Wabunge wote wa upinzani na viongozi wote wa CHADEMA kwa ujasiri wao wa kuendelea kuchapa kazi bila woga licha ya mazingira magumu ya kufanya siasa hapa nchini. Aidha, nawatia moyo wale wote waliookamatwa na kuwekwa kizuizini magerezani; walioumizwa na kujeruhiwa kwa sababu tu ya kutumia haki yao ya kikatiba ya kushiriki shughuli za kisiasa. Napenda kuwaambia wasikate tamaa kwani mateso wanayoyapata ni kielelezo cha ukombozi wa watanzania walio wengi.

3. Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia wasaa huu kuishukuru sana na kuipongeza Jumuia ya Kimataifa na hususan Umoja wa Ulaya na Ubalozi wa Marekani hapa nchini kwa kuendelea bila kuchoka kupaza sauti dhidi ya vitendo viovu vya ukandamizaji wa demokrasia na haki za binadamu na dhidi ya vitendo vyenye sura ya ugaidi vya utekaji, utesaji, majaribio ya mauaji na mauaji ya viongozi wa kisiasa hasa wa vyama vya upinzani katika mataifa mbalimbali duniani. Mungu atawalipa kwa kazi kubwa mnayofanya ya kuhakikisha kwamba uhai na uhuru na utu wa mwanadamu vinalindwa na kuheshimiwa duniani kote.

4. Mheshimiwa Spika, leo tunajadili uhusiano wa kimataifa tukiwa katika zama mpya za utandawazi na soko huria ambapo nguvu ya soko ndiyo inayoendesha uchumi na kuamua mustakabali wa nguvu za madola mbalimbali duniani. Kwa maneno mengine, nguvu za kiuchumi ndizo zinazolipa taifa nafasi ya kuheshimiwa na kuthaminiwa mionganoni mwa mataifa mengine. Pamoja na uchumi wa soko huru; utawala wa sheria unaoheshimu haki za binadamu na demokrasia ya kweli ni nguzo muhimu za utandawazi ambako

ndiko ulimwengu ulipo sasa, ndiko unakoendelea kuwa na ndiko utakakokuwa.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

**B. TANZANIA IMEKUWA NA KIGUGUMIZI CHA KURIDHIA
MKATABA WA MAKUBALIANO YA ENEO HURU LA
BIASHARA BARANI AFRIKA**

8. Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 21/03/2019 Jijini Kigali Rwanda, viongozi wakuu wa nchi za Kiafrika na wale walioziwakilisha nchi zao walitia sahihi makubaliano ya kuanzishwa eneo huru la kibashara Barani Afrika. (African Continental Free Trade Area - AfCFTA). Lengo la makubaliano hayo ni kuondoa vikwazo vya biashara baina na miongoni mwa nchi za Afrika na hivyo kuongeza kiwango cha biashara ndani ya Bara hilli.

9. Mheshimiwa Spika, Eneo huru la kibashara Afrika linakuja wakati kiwango cha biashara miongoni mwa nchi za Afrika kikiwa ni cha chini kabisa cha asilimia 15.4 ukilinganisha na mabara mengine. Aidha, inatarajiwu kuwa ifikapo mwaka 2022, chini ya mkataba huu, biashara baina ya nchi za kiafrika zitaongezeka hadi kufikia asilimia 52 tofauti na asilimia 15.4 ya sasa.

10. Mheshimiwa Spika, Mpaka sasa nchi 23 ikiwemo Zimbabwe iliyordhia hivi majuzi tarehe 25 Mei, 2019; zimesaini mkataba huo na mabunge ya nchi hizo pia yameshapitisha azimio la kuridhia mkataba huo na kwa maana hiyo soko huru litaanza kufanya kazi mwezi Julai 2019. Kwa upande wa Afrika Mashariki, nchi za Kenya, Rwanda na Uganda tayari zimeshakamilisha hatua zote.

11. Mheshimiwa Spika, Kwa kuwa Serikali inajinasibu kutekeleza diplomasia ya uchumi na kwa kuwa AfCFTA ni fursa nyingine ya kuinua kiwango cha kibashara ndani ya Afrika hasa kwa mataifa yanayoipanga kimkakati, ni jambo lisiloelezeka kuona mpaka sasa Tanzania imekumbwa na kigugumizi kikubwa juu ya makubaliano haya na hivyo

kutowasilisha Bungeni kuridhiwa na hatimaye kuwasilisha nyezo za utekelezaji wake kwa Kamishna wa Umoja wa Afrika.

12. Mheshimiwa Spika, Kwa taifa makini, mkataba huu ni hitaji la muda mrefu ambalo ni fursa kwa uchumi wa taifa hili kukua kwa kasi na kusaidia kupunguza kiwango cha umasikini. Kwa kutambua umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa katika kukuza uchumi; Kambi Rasmi ya Upinzani kuititia CHADEMA imeeleza bayana katika Sera yake ya Mambo ya Nje Sura ya 12.1 kuhusu namna ambavyo uhusiano wa kimataifa utatumika kujenga diplomasia ya uchumi. Sera hiyo inatamka kama ifuatavyo; *"Chadema itaweka sera ya mambo ya nje ambayo itazingatia masuala ya uchumi, ulinzi, diplomasia na masuala mengine muhimu katika uhusiano wa kimataifa. Balozi za Tanzania zitakuwa na jukumu la kufanya diplomasia ya uchumi kwa kuwavutia wawekezaji na mitaji kutoka nje bila kuathiri ulinzi na maslahi ya nchi"*.

13. Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba, AfCTA ni nyenzo muhimu ya kukuza mahusiano yetu na mataifa mengine Barani Afrika hasa yale ambayo sio ya EAC na SADC ambamo sisi ni wanachama. Aidha, tunaona kwamba AfCFTA ni nyenzo muhimu ya kukuza uchumi wa watanzania na taifa letu kwa ujumla kwani inatoa fursa kwa watu wetu kufanya biashara kwa urahisi zaidi na wenzao Afrika.

14. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ina mtazamo kwamba kuendelea kuchelewa kwa Serikali kuleta mkataba huo ili uridhiwe na Bunge, ni kuendelea kuchelewa kuchangamkia fursa za biashara jambo ambalo halina afya kwa maendeleo ya uchumi wetu na kunakwenda kinyume na azma ya Serikali ya kukuza diplomasia ya uchumi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni lini italeta mkataba huo ili uridhiwe na Bunge.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

23. **Mheshimiwa Spika**, Matukio ya utekwaji wa watu mbali mbali hasa wanaonekana kuikosoa Serikali, kupotezwa kwa watu pasi na hatua madhubuti kuchuliwa na vyombo vya dola, majoribio ya kuuwawa kwa viongozi wa kisiasa na kuminywa kwa uhuru wa vyombo vya habari ni mambo ambayo yanaichafua Tanzania kwenye ulimwengu wa kimataifa. Kwa kipindi hiki, Serikali ya Tanzania imegonga vichwa vya habari kimataifa si kwa uzuri wala ukarimu wake kama ilivyokua imezoleka, bali kwa ukatili dhidi ya raia wake.
24. **Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya haki za binadamu ya State Department ya Marekani kwa mwaka 2018 inaonyesha hali ya hatari kwa Tanzania kwa kubainisha matukio ya mauaji, kutekwa na kupotezwa kwa watu, uvunjifu mkubwa wa sheria na katiba ya nchi pamoja na ukandamizwaji mkubwa wa vyama vya upinzani. Hali hii pia inashajihishwa na ripoti ya Freedom House kwa Tanzania kwa mwaka 2018.
25. **Mheshimiwa Spika**, Mambo haya sio tu yameichafua na yanaendelea kuichafua Tanzania bali yana athari za moja kwa moja taifa kama ifuatavyo:
- i. *Kudorora kwa Shughuli za Kiuchumi*
26. **Mheshimiwa Spika**, ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa kiwango kikubwa unategemea na uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje ya nchi (Foreign Direct Investment). Taarifa ambazo ziko kwenye ripoti ya IMF zinaashiria kuporomoka kwa ukuaji wa uchumi wa Tanzania kutoka 7.1% mwaka 2016 hadi asilimia 6 mwaka 2018/19. Hii maana yake ni kwamba kumekuwepo na kuzorota kwa shughuli za uzalishaji nchini zinazotokana kwa kiasi kikubwa na uwekezaji wa makampuni ya nje.
27. **Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha huohuo, taarifa ya UNCTAD (United Nations Conference on Trade and Development) ya Uwekezaji Duniani ya mwaka 2018 inaonyesha kwamba kuna anguko la asilimia 14 la kiwango cha uwekezaji kwa Tanzania. Anguko hili ni kielelezo cha

kwamba wawekezaji wanaikimbia Tanzania kutokana na mambo ya hovsky yasiyo ya kibinadamu yanatokea chini ya utawala huu pasi na hatua madhubuti kuchukuliwa na zikaonekana kweli zinachukuliwa.

28. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatafsiri kuperomoka kwa kiwango cha mitaji ya uwekezaji kutoka nje (Foreign Direct Investments) nchini kama kielelezo cha Serikali hii ya CCM ya awamu ya tano kushindwa kutelekeza kwa vitendo Diplomasia ya urchumi.

29. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba kukimbia huku kwa wawekezaji kunatokana, pamoja na mambo mengine, vitendo viovu wanavyofanyiwa raia wa Tanzania na watu ambao mpaka leo Serikali ni ama Serikali inawajua na haitaki kuwachukulia hatua ama haina uwezo wa kuwabaini na kuwachukulia hatua na hivyo kutishia usalama mpana wa raia na mali zao. Aidha, maelezo ya kujichanganya yanayotolewa na vyombo vyaa dola dhidi ya matendo haya yanaongeza hofu zaidi kwa raia yoyote nchini kuishi kwa amani na kufanya kazi zake kwa utilivu. Kwa mazingira haya hakuna mwekezaji makini atakayetekeleza mitaji yake kuwekeza sehemu ambapo Serikali inashindwa kutoa uhakika wa usalama kwa raia.

30. Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Shiriki la Bertelsmann² ya Ukanda wa Afrika yenyewe kichwa cha habari "A Divided Content" ya mwaka 2018 inataja urchumi wa Tanzania kuanza kusinyaa kuanzia mwaka 2016. Ripoti hiyo inabainisha kwamba kusinyaa huku kunatokana na maamuzi juu ya urchumi yanayotokana na mihemko na sifa za kisiasa kuliko uhalisia (Populism). Ripoti hiyo inaweka bayana kuwa mambo haya yameshusha morali ya wawekezaji kutoka nje na uungwaji mkono wa jumuia ya kimataifa.

²Bertelsmann is a German multinational corporation based in Gütersloh, North Rhine-Westphalia, Germany. It is one of the world's largest mass media companies and also active in the service sector and education

31. **Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya ripoti hiyo inasema kwamba; naomba kunukuu... *"in a small but significant number of states including Tanzania and Zambia, this was compounded by the emergence of populist leaders who sought to intervene in the economy for political as much as economic goals, undermining investor confidence. One consequence of these changes has been the failure to effectively harness potential international support"*

32. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kuiarifu Serikali hii ya CCM, kama ilikuwa hajui na ijue sasa kwamba kufanikiwa au kutokufanikiwa kwa sera ya nje ya nchi yoyote duniani kunatokana na jinsi nchi hiyo inavyoendesa siasa zake za ndani. Siasa za ndani zina athari ya moja kwa moja na mahusiano ya nchi na jumuiya ya kimataifa.

33. **Mheshimiwa Spika**, tunaikumbusha pia Serikali kuwa suala la usalama wa ndani kwa upana wake ni kichocheo kikuu cha kuvutia wawekezaji kutoka nje. Ni kwa maana hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza katika Diplomasia ya Uchumi na Usalama na si vinginevyo. Usalama unatokana pamoja na mambo mengine kuheshimu utawala wa sheria, haki za msingi za binadamu na misingi madhubuti ya demokrasiatofauti na ilivyo sasa.

ii. Kudorora kwa Mahusiano baina ya Tanzania na Jumuiya ya Kimataifa

34. **Mheshimiwa Spika**, kuongezeka kwa matendo ya utekaji wa raia, kupotezwa kwa watu bila maelezo yanayoeleweka ya Serikali, majaribio ya kuua bila wauaji kutiwa nguvuni, kuonewa na kukandamizwa kwa vyama vyia upinzani nchini kumepelekea wadau mbalimbali wa kimataifa kupaza sauti zao kukemea matendo haya. Hata hivyo Serikali imewaona wadau hawa kama maadui wa taifa na hivyo kuweka mbinyo juu yao. Hili linadhahirishwa na mahusiano mabovu yaliyoko kati ya Tanzania na Jumuiya ya Ulaya ambayo imekiri kuwa ilimwita Balozi wake kurudi Ubelgiji kutokana na shinikizo la Serikali ya Tanzania juu yake.

35. **Mheshimiwa Spika**, mpaka sasa Jumuiya ya Ulaya ambayo imekuwa mdau mkubwa wa maendeleo ya Tanzania katika sekta mbalimbali haina Balozi wake nchini na kwamba jumuiya hii inapitia upya mahusiano yake na Tanzania. Kutikisika kwa mahusiano baina ya Tanzania na Umoja wa Ulaya hakuwaathiri viongozi wa CCM bali wananchi wanaonufaika na misaada ya Jumuiya hii katika maeneo mbali mbali.

36. **Mheshimiwa Spika**, uthibitisho wa m dororo wa mahusiano kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya ni tamko liliilotolewa na Makamu wa Kamisheni ya EU anayeshughulikia mambo ya nje na masuala ya sera ya ulinzi, Federica Mogherini la tarehe 15/11/2018.

37. **Mheshimiwa Spika**, sehemu ya tamko hilo inasema hivi: *"In this context, the Tanzanian authorities have consistently increased their pressure on the EU Ambassador. This eventually led to his forced departure and recall for consultations. This unprecedented attitude is not in line with the long established tradition of bilateral dialogue and consultation between the two parties, which the EU deeply regrets. The EU calls on Tanzanian authorities to refrain from exerting undue pressure and limitations on diplomatic missions"*. Tamko hili linaonyesha sio tu EU waliokuwa na shinikizo la Serikali bali Balozi mbalimbali.

38. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuelewa kwamba hakuna Serikali duniani inayoweza kufanikiwa bila kuwa na mahusiano na mataifa mengine. Ni bahati mbaya sana kwamba, Serikali ya awamu ya tano inagombana mpaka na wahisani wanaoipatia misaada ya kibajeti.

39. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge na Taifa, ni kwa nini ilimuwekea shinikizo Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini hata kupelekeea kuondoka kwake? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ingependa pia kujua ni kwa nini Serikali hii ya awamu ya tano imeanza kuwa na tabia ya kuziingilia na kiziwekeea mashinikizo

Balozi zinazoziwakilisha nchi zao katika utendaji wao wa kazi ikiwa haziendi kinyume na Mkataba wa Vienna? Hata kama Serikali inaona Balozi hizo zimekua zikikiuka Mkataba wa Vienna katika utendaji wao wa kazi Bunge na Taifa linapaswa kuelezwu ni mambo gani hayo Balozi hizo zimekuwa zikifanya mpaka kustahili mashinikizo

E. KANZI DATA YA WATANZANIA WAISHIO NJE YA NCHI (DIASPORA DATABASE)

40. **Mheshimiwa Spika**, Dunia sasa inatambua mchango mkubwa wa uchangiaji uchumi unaofanywa na watu mbalimbali wanaoishi nje ya nchi zao yaani Diaspora. Hatuna budi kama Watanzania kuendelea kutambua na kuthamini mchango huu mkubwa unaofanywa na kaka na dada zetu wanaoishi nje ya nchi kwani uwepo wao huko unachangia kukuza jina la nchi yetu na kuboresha mahusiano na nchi hizo.

41. **Mheshimiwa Spika**, hakuna takwimu za kitaifa zinazoonyesha idadi kamili ya Watanzania wanaoishi nje ya nchi na taarifa za kile wanachokifanya huko. Umuhimu wa kuwa na taarifa ni kubaini kwa wepesi idadi na aina ya watu wenye ujuzi na uzoefu ambao Serikali inaweza kuutumia kwa maslahi ya nchi. Aidha, kujua idadi ya wananchi walio nje ya nchi kutapelekea kutengeneza milango ya kiuchumi kati yao na nchi (economic gateway), kutafungua fursa za kibashara ikiwa ni pamoja na soko la nje (export market) kwa bidhaa zetu za Kitanzania na hivyo kutaachia fursa kwa soko la ndani kuboresha bidhaa zao ili ziweze kupata masoko nje.

42. **Mheshimiwa Spika**, kuwepo kwa database hiyo pia yenye kila Mtanzania aliyepo nje ya nchi kutasaidia kupunguza idadi ya raia wa nchi nyingine wanaotumia jina la nchi yetu vibaya huko nje ya nchi kwa kujifanya ni wakimbizi kutokea Tanzania. Tutaweza kuwatambua na kuwabaini kwa kutumia Balozi zetu.

43. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa jambo hili la kutengeneza database

linazingatiwa kwa uzito wake kwa kuwa lina manufaa kwa wananchi wetu walio katika kila pembe ya dunia na pia manufaa kwa ya uchumi wa nchi yetu.

44. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasitiza uwepo wa kanzidata hiyo kwa kuwa Diaspora ina mchango muhimu katika kukuza uchumi wetu. Kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu za Benki ya Dunia, Watanzania waishio nje (Diaspora) waliochangia 0.8% ya GDP yetu kwa kutuma kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 430 kwa mwaka 2018. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kwamba ni muhimu kuwa na takwimu za watanzania waishio nje sambamba na shughuli wanazofanya ili iwe rahisi kufanya makisio ya fedha zitakazopatikana (diaspora remittance) na kuziingiza kwenye bajeti ya Serikali.

45. Mheshimiwa Spika, utengenezaji wa kanzidata hiyo uende sanjari na kutungwa kwa sera na sheria mpya itakayoruhusu watanzania kuwa na haki ya uraia pacha ambao utamwezesha mtanzania aishiye nje kuwekeza kwa uhuru nje ya nchi na hapa nyumbani Tanzania. Kumzuia mtanzania anayeishi nje kuwa na uraia pacha ni kumwekea shinikizo la kutowekeza kikamilifu nje kwa kuwa anaishi kule kama mgeni na kwa sababu hiyo mchango wake wa fedha (remittance) hapa nchini utakuwa pia wa mashaka kutokana na kutokuwa na uhuru wa uwekezaji mkubwa nje.

46. Mheshimiwa Spika, suala la uraia pacha kwa dunia ya leo ni fursa. Kimkakati, uraia pacha ni kichocheo cha maendeleo kwa taifa. Mathalani, kwa majirani zetu Kenya wenye uraia pacha, diaspora yao imechangia kiasi cha dola za kimarekani milioni 2,720 kwa mwaka 2018 sawa na asilimia 3 ya Pato lao la Taifa (GDP). Hii ni kutokana na Wakenya wenye uraia wa nchi nyingine kuwa na (confidence) ya kuwekeza nyumbani bila bugudha ya aina yoyote.

47. Mheshimiwa Spika, umuhimu wa uraia pacha kwa Watanzania na wasio Watanzaia hauko tu kwenye michango ya kifedha bali upatikanaji wa ujuzi na maarifa (skills) mbalimbali kutoka kwenye mataifa mengine ambazo ni vigumu kupatikana Tanzania kwa mazingira yake.

48. **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua umuhimu wa uraia pacha katika kukuza diplomasia ya uchumi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuititia CHADEMA, inakusudia kuanzisha sera na sheria ya kuruhusu uraia pacha pindi ikipewa ridhaa na wananchi ya kuendesha Serikali. Sera ya Chadema ya Mambo ya Nje, Sura ya 12.3 inasema hivi: *"Chadema itaanzisha sera na kutunga sheria ya kuruhusu uraia pacha ikiwa ni pamoja na kuwahimiza Watanzania wanaoishi nchi za nje kuwekeza Tanzania. Aidha, itaweka utaratibu wa hati fungani ambazo zitaongeza hifadhi ya fedha za kigeni nchini"*.

F. MSIMAMO WA TANZANIA KATIKA KUPINGA UBEBERU NA UKOLONI, NA UONEVU DUNIANI

49. **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu imekuwa na historia iliyotukuka duniani, ya kuwa mstari wa mbele kupinga aina zote za uonevu, unyonyaji na utumwa hususani ubeberu na ukoloni. Kutokana na tunu yake ya kujali utu na usawa mionganini mwa binadamu wote, Tanzania ya enzi za Mwalimu Nyerere, ilifikia hatua ya kujitoa kupigana vita vya ukombozi wa nchi za Kusini mwa Afrika, ili kuhakikisha kwamba ubeberu na ukoloni katika nchi hizo unatokomezwa na uhuru wa kweli unapatikana.

50. **Mheshimiwa Spika**, utakumbuka kwamba Tanzania ndio iliyokuwa mwasisi wa nchi za Mstari wa Mbele chini ya uongozi wa Mwalimu Nyerere katika miaka ya 1960 kwa lengo la kupinga ubaguzi wa rangi na utawala wa wazungu wachache katika nchi za Kusini mwa Afrika.

51. **Mheshimiwa Spika**, Tanzania illienda mbele zaidi hadi kufikia hatua ya kuvunja mahusiano yake ya kidiplomasia na mataifa mengine yaliyokuwa na tabia za ubaguzi wa rangi, unyonyaji, ubeberu na ukoloni dhidi ya mataifa mengine. Itakumbukwa kwamba Tanzania ilivunja ushirikiano wake wa kidiplomasia na Israeli kutokana na Israeli kuwa na tabia za kibeberu za kutaka kuikalia ardhi ya Palestina kwa nguvu. Aidha, Tanzania ilivunja mahusiano yake ya kidiplomasia na Morocco, kutokana na nchi hiyo kuikalia Sahara Magharibi kwa nguvu.

52. Mheshimiwa Spika, Tanzania ilipinga pia utawala wa ki-dikteta mionganoni mwa nchi za Afrika, kwa kuwa udikteta ulikuwa na tabia zote za unyonyaji, ubaguzi, uonevu na ukiukwaji wa haki za binadamu – mambo ambayo Watanzania hawakuamini katika hayo - na ndio maana Tanzania kwa wakati huo, haikumuunga mkono Mobutu Seseseko wa iliyokuwa Zaire – sasa Kongo DRC, haikumuunga mkono Muamar Gadafi wa Libya na pia ilimng'oa madarakani dikteta wa Uganda Idd Amin Dadah.

53. Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni tumeshuhudia nchi yetu ikuhuisha mahusiano ya kidiplomasia na nchi nilizotitaja, ambazo hapo awali tulikuwa hatuna mahusiano nazo kutokana na kukalia mataifa mengine kimabavu au kufanya uonevu dhidi ya mataifa mengine. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kulieleza Bunge hili, ni sababu zippi zimepelekea Tanzania kubadili msimamo wake, kuhusu ushirikano na mataifa hayo? Je, Morocco imeacha kuikalia kimabavu nchi ya Sahara Magharibi? Na je, Israeli imeacha kuionea Palestina? Na kama Serikali imebadili msimamo wa nchi kuhusu ushirikiano na mataifa hayo, je, mabadiliko hayo ya msimamo wa nchi, yaliridhiwa na Bunge hili?

54. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua pia ni nini msimamo wetu kama Taifa, juu ya tabia za kidikteta, ukiukwaji wa haki za binadamu, unyanyasaji na uonevu zinazoanza kuibuka na kujionyesha wazi mionganoni mwa baadhi viongozi wa mataifa mbalimbali duniani ?

G. BREXIT NA ATHARI ZAKE KWA TANZANIA

54. Mheshimiwa Spika, Tanzania hajajiaandaa kukabiliana na Brexit. Inafahamika kuwa Tanzania ni mshirika wa kibiashara na EU na pia imekuwa na mahusiano ya karibu na muda mrefu na UK ambayo wananchi wake walipopiga kura za maoni waliamua kuwa nchi yao ijiteo kwenye Umoja wa Ulaya. Hali hii imeifanya nchi ya Uingereza kuanza harakati za kutafuta nchi washirika na hasa zilizowahi kuwa makoloni yake ili kuwafanya washirika wake endapo watajitoa EU.

55. Mheshimiwa Spika, katika hilo Tanzania haijaonyesha kwa uwazi kuwa itakuwa upande upi hasa ikizingatiwa kuwa hatujasaini mkataba wa kibashara na EU maarufu kama (EPA) ambao nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wameonyesha wazi kuwa watasaini na kuiacha Tanzania na Burundi nje ya mkataba huo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge kuhusu msimamo wake wa wazi juu ya Brexit.

56. Mheshimiwa Spika, Sambamba na hilo kumekuwa na m dororo wa kidiplomasia baina ya Tanzania na nchi za Umoja wa Ulaya (EU) hasa kutokana na kitendo cha Serikali ya Tanzania ‘kumtimua’ nchini aliyekuwa Balozi wa Umoja huo mwaka 2018 na EU wakaamua kutokumteua mtu mwingine kuja kuwawakilisha nchini. Kitendo hiki ni dalili za wazi kuwa mvutano ni mkubwa na Serikali haikuwahi kutoa kauli hadharani jambo ambalo limepelekeea kuwepo kwa minong’ono mingi mitaani. Tunaitaka Serikali iweke wazi msimamo wake kuhusu mahusiano ya kidiplomasia baina yake na Umoja wa Ulaya na hasa sababu zilizopelekeea kuondolewa kwa Balozi wa Umoja huo nchini mwishoni mwa mwaka 2018.

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

62. Mheshimiwa Spika, lipo tatizo la msingi la mahusiano baina ya nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mfano, mahusiano baridi baina ya Uganda na Rwanda na Burundi na Rwanda, jambo ambalo ni tishio la kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, kama matatizo hayo hayatashughulikiwa mapema. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili na Taifa kwa jumla ni hatua gani za kidiplomasia zimechukuliwa hadi sasa kusuluhisha mvutano baina ya nchi wanachama zenye migogoro? Katika hatua hizo, Tanzania ambayo imekuwa nembo ya amani na msuluhihi wa migogoro katika ukanda wa maziwa makuu imefanya nini mpaka sasa ili kuhakikisha kwamba nchi wanachama zinashirikiana kwa upendo na amani ili kuiimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki?

[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

K. HITIMISHO

71. Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kusema kwamba duniani kote Wizara za Mambo ya Nje ni Wizara za kimkakati. Kwa nchi yotote ile, Wizara ya Mambo ya Nje ndiyo inayotekeleza mikakati ambayo nchi inataka kuifikia kutoka kwenye mataifa mengine. Kwa maneno mengine kutoichukulia kwa uzito Wizara ya Mambo ya Nje ni kutokuwa makini na malengo muhimu ambayo taifa linataka kuyafikia.

72. Mheshimiwa Spika, mikakati ya kimaendeleo ya ndani lazima ifungamanishwe kikamilifu na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuendana na hali ya dunia. Ndio maana mataifa yalioendelea huwa na mpango mkakati kwenye Wizara zao za nje. Kwa mfano nchini Uingereza wana mkakati wa maendeleo ya kimataifa kupitia Department for International Development - DFID na Marekani wana mkakati kama huo kupitia United States Agency for International Development – USAID.

73. Mheshimiwa Spika, ni kwa misingi hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuipa kipaumbele Wizara hii kwanza kwa kwa kuweka mpango mkakati wa kuandaa rasiliamali watu wenye maarifa na weledi wa kutosha kuendesha diplomasia ya kimataifa, lakini pili kwa kuitengea Wizara hii fedha za kutosha kwa ajili ya kuweza kutekeleza diplomasia hiyo.

74. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai hiyo, kwa sababu kumekuwa na viashiria vya kudharauliwa kwa Wizara hii na kuonekana kama haina umuhimu kwa nchi. Viashiria hivyo ni pamoja na kutenga bajeti ndogo jambo ambalo limepelekea Balozi zetu huko nje kuwa na mazingira duni na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, kiashiria kingine ni muda mdogo unaotengwa kujadili bajeti yenye. Kutenga siku moja au masaa kadhaa kujadili mustakabali wa nchi yetu

katika ulimwengu wa kimataifa kana kwamba ni idara au kitengo fulani ndani ya Wizara kinajadiliwa ni kutojitendea haki sisi wenyewe na maana yake ni kwamba tutaendelea kubaki nyuma kwa takribani kila sekta kutokana na kuachwa na dunia.

75. Mheshimiwa Spika, Wizara hii inabeba mambo mengi mtambuka muhimu, zaidi ulinzi na usalama pamoja na uchumi wetu kwenye uso wa dunia. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa kipaumbele stahili kwa Wizara hii.

76. Mwisho kabisa Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaisihi Serikali kupitia kwa Waziri mwenye dhamana kurejesha tena heshima ya Tanzania katika ulimwengu wa kimataifa ilioanza kutoweka. Sisi si kisiwa, tunaihitaji dunia kuliko dunia inavyotuhitaji sisi. Daima tukumbuke methali hii "tawi likijitenga na shina hunyauka" na huo ndio huwa mwisho wake.

77. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, namba kuwasilisha.

.....
Salome Wycliffe Makamba, (Mb)

**KNY. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA WIZARA YA MAMBO YA NJE, USHIRIKIANO
WA AFRIKA MASHARIKI, KIKANDA NA KIMATAIFA**

30 Mei, 2019

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tumemaliza uwasilishaji na kwa muda wetu uliosalia, wachangiaji wetu watakuwa wachache kuliko wale ambao walikuwa wamekusudiwa. Kwa hivyo, kwa kuwa tumebak kama na dakika 15 hivi, kila chama kitapata mchangiaji mmoja kwa dakika tano. Tutaanza na Mheshimiwa Susan Lyimo atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Stanslaus Mabula ajiandae.

MHE. SUSAN A. J. LYIMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na masikitiko yangu ni jinsi ambavyo hotuba yetu imekatwakatwa, lakini naamini kabisa watu wameelewa nini kinachoendelea na imekuwa bahati mbaya sana, mambo haya yanasemwaa Mabalozi wetu wapo hapa juu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee. Wizara hii ni muhimu sana na ndiyo kioo cha nchi kwenye dunia au kwenye ulimwengu wetu. Kwa hiyo chochote kinachofanyika ndani ya nchi, Wizara hii ipo *responsible* na ndiyo sababu umeona kwamba wameangalia Wizara zote kuanzia kilimo na nini na nini na ndiyo sababu hata Kambi ya Upinzani tumeongelea masuala hayo ya kilimo na mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba kuna tatizo kubwa sana katika Wizara hii. Nilzungumzie suala la watumishi, kumekuwa na tatizo kubwa sana la kupandishwa vyeo, pamoja na kwamba ni tatizo la kitaifa, lakini nilitegemea Wizara hii ingeweza kuwapandisha watumishi wake kwa takribani miaka 12 bado watumishi wa Wizara waliokuwa kwenye cheo fulani kwa mfano ile *Foreign Service* /mpaka leo kwa miaka 12 walitakiwa wawe *Principal Officers* lakini bado wako pale. kwa hiyo, naishauri Serikali wafanye kuwapandisha kwa mserereko ili waweze kupata hadhi yao na hivyo kuleta motisha katika kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia pia bajeti; bajeti na nashukuru hata Kamati imesema na Kambi. Ukiangalia mishahara, kwa mfano nimejaribu kuchukua, ukiangalia *recurrent budget* kwa mwaka jana na mwaka huu utaona kuna tofauti ya takribani shilingi bilioni 10, lakini kibaya zaidi angalia kwenye zile *multilateral missions*, unakuta kuna upungufu mkubwa sana wa mishahara. Kwa mfano, Balozi wetu wa London mwaka jana kwenye mishahara tu (*basic salary*) ilikuwa milioni 177, mwaka huu milioni 81. Ukija Lusaka ilikuwa milioni 93, mwaka huu milioni saba, ukienda Moscow ilikuwa milioni 116, mwaka huu milioni 77, ukienda Ottawa Canada ilikuwa milioni 107, mwaka huu milioni 49, ukija Rome ambako ni *Multilateral*tuna FAO na mambo mengine ilikuwa

milioni 166, mwaka huu ni milioni 100, ukija Riyadh ilikuwa 110, mwaka huu ni milioni 81, ukija New York ambapo tuna Mashirika makubwa ya Kimataifa ilikuwa milioni 88, mwaka huu milioni 64.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ina-cut across kwenye Balozi zetu zote na hili ni tatizo kwa sababu tunajua kwamba toka mwaka 2016 walivyordisha baadhi ya Maafisa wa Ubalozi, bado hawajafanya *replacement*. Nilikuwa Doha mwaka huu, pale wana watumishi wawili tu, Balozi na mtumishi mmoja au wawili, ukienda New York ni hivyo hivyo, nimetembea nchi nyingi kuna matatizo makubwa ya watumishi. Nataka kujua ni kwa sababu gani baada ya kurudisha baadhi ya watumishi, hawajawa-*replace* kwenye Balozi hizo kiasi kwamba hii inakuwa *reflected* kabisa kwenye hii mishahara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kumekuwa na tatizo kubwa sana la utendaji na ndio maana tunasema sasa ni lazima Waziri anapokuja ku-*wind up* atuambie baada ya kupunguza Maafisa wa Balozi, ni kazi gani wamefanya kuhakikisha kwamba wanawa-*replace* ili kazi ziweze kwenda. Tunajua kwa mfano pale New York wameondoa watu wengi sana, kwa hiyo Kamati mbalimbali hazipati watu wa kufanya hizo kazi au mtu mmoja anafanya kazi ya watu watatu. Kwa hiyo, tunaomba na hilo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Bunge tuna *passport* za Kibalozi, lakini na wengine wengi. Siku za nyuma tulikuwa tuna utaratibu mzuri, *Chief of Protocol* alikuwa anakuja kutoa mafunzo ya *etiquettes* na ni jinsi gani mtu anaweza ku-*appear*. Leo hivi tunaona hata Mabaloz wetu hawajui hizo *etiquettes*; inawezekanaje Balozi wa nchi anafuta miwani kwa kutumia ulimi. Kwa hiyo, haya ni mambo ambayo tunaona hayafai kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana... (*Makofi*)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

NAIBU SPIKA: Kengele imeshagonga Mheshimiwa Susan, ahsante sana. Mheshimiwa Riziki Lulida, tutamalizia na Mheshimiwa Timotheo Mzava.

MHE. RIZIKI S. LULIDA: Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru na niwatakie heri Waislam na wasiokuwa Waislam katika mwezi huu Mtukufu na kuwaombea amani na utulivu katika nchi yetu ya Tanzania ambayo itajengwa na Watanzania wenyewe. Hawezi kutoka mtu huko nje kuja kutuletea amani na utulivu, tushikamane Watanzania wote, tuijenge amani yetu na wenzetu wajifunze na iwe mfano katika nchi za wenzetu ambao wameonja vita ikiwemo Libya. Libya wameonja vita wakasema hakuna *democracy*, leo wenzetu wa Libya wapo katika uchumi mgumu, tujifunze kwa mapana yetu, tusiende kuhangai na maneno ya uchochezi wakaifanya nchi ikamwaga damu. Nawapenda Watanzania, naipenda amani ya Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nitazungumzia suala la mjesi ambaye yupo Ujerumani. Nilimwacha katika Wizara ya Maliasili kuileta kwa vile hapa ni sehemu pekee ambayo Ubalozi wa Ujerumani ni kama nchi ya Ujerumani iweze kutuambia sisi watu wa Mkao wa Lindi ambao lile jusi kubwa (*dinosaur*) na mifupa yake ipo Ujerumani, tunapata nini ndani ya yule mjesi? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimetaka kufunga ukurasa leo, Wizara ya Maliasili, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ishirikiane na nchi ya Ujerumani tuweze kujua katika Halmashauri ya Lindi inapata nini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji ambavyo vimezunguka pale palitoka yule mjesi wamesema *it's a lost science*, hapana *it's a life science*. Naomba Ubalozi wa Ujerumani wawatoe wawakilishi, nifuatane nao mimi nikiwa na kundi langu maalum twende mpaka Tendeguru lilipotoka lile jusi ili wakajionee kuwa jusi lile limetoka Tanzania katika Wilaya ya Lindi Vijijini, katika Kijiji cha Mipingo na Wanamipingo waweze kufaidika na mjesi yule. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili nalizungumza kwa mapana yake; utalii mkubwa utakaopatikana ndani ya Tendeguru utakuwa ni uchumi mkubwa katika uchumi wetu wa Tanzania. Tulikaa kwa muda mrefu toka mwaka 1905, mvumbuzi ambaye alikuwa mchimbaji wa madini akishirikiana na Wolf Henrick pamoja na Martin Abald, wao walikwenda Tendeguru kuchukua ile mifupa kwa ajili ya uchimbaji, wamepeleka Ujerumani, kunafanyika *exhibition*. Katika miaka yote mpaka leo katika vijiji vile hatujafaidika hata kwa kujengewa shule. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu Balozi na wawakilishi kutoka Ujerumani wanansikia, tukitoka hapa moja tu kuwa tunataka maendeleo katika Wilaya ya Lindi katika kupitia eneo lile lililotoka mjusi hata angalau wakatuoneshe kumbukumbu iko wapi. Tunataka ushirikiano kati ya Ujerumani na Lindi Vijiini illi angalau Lindi Vijiini wajue pato linalopatikana na wao wanafaidika. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu; naomba tupate shule katika eneo la Mipingo na vijiji vinavyozunguka, tunataka maji maana yake maeneo yale hayana maji, tupate maji katika maeneo yale, tupate vituo vya afya ili kujenga uhusiano bora uliokuwepo kati ya Tanzania na Ujerumani kwa kupitia *dinosaur*. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, wanazungumza halijulikani *It's a lost science, it's not a lost science, it's a life science come to Tanzania and visit Tendeguru na mtaona kila kitu kipo pale.* Ni matumaini yangu kuwa leo naitangaza Tendeguru ndani ya Bunge, naitangaza Tendeguru ndani ya Ujerumani, Wajerumani tukutane baada ya Bunge, Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje, Waziri wa Maliasili na Waziri wa Fedha tukutane kwa pamoja na mimi mwenyewe kama mdau mwanaharakati kwa muda wa miaka 15, naomba nami niwepo nitibitishe hili ili mapato yapatikane na nchi yangu iweze kutoka. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia fursa zilizopo ndani ya Balozi zetu. Nchi hii tuna Balozi ambayo inataka

kutupa uwakilishi, wale Mabalozi wasikae ubalozini kule wamekaa wanatumia pesa nyingi, matumizi makubwa. Je, wana-deliver nini katika nchi yangu ya Tanzania? Tunataka fursa tulizokuwa nazo Tanzania za kilimo, madini waje watuonyeshe tunafanya hivi. Tumekwama tunataka soko la *Euro*, wale wa *Europe* wanatupa soko gani sisi Watanzania ili angalau tutoke na mazao yetu, haiwezekani Tanzania soko letu mpaka twende Uganda, Rwanda; imekuwaje Mabalozi wetu wanafanya nini kutushirikisha kama nchi kuiingiza katika uchumi bora wenye maendeleo. Tanzania yenye maendeleo kwa kupitia Balozi zetu inawezekana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makof!*)

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kama kijana wa Kitanzania kiongozi nasimama kwa uchungu sana kwa yanayoendelea ndani ya Bunge letu. Tunapofanya siasa na kuchafua sura ya Taifa letu badala ya kulitetea na kuliweka vizuri Taifa letu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ni mchache, nizungumze mambo machache. Jambo la kwanza nizungumze nafasi ya haki za binadamu kwenye mahusiano ya Kimataifa. Nakubaliana kabisa kwamba haki za binadamu zina nafasi kubwa kutuweka kama Taifa kwenye sura nzuri kwenye ulimwengu huu, kwenye mahusiano yetu na nchi nyingine na Mataifa mengine. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho tunasahau, Tanzania ni miongoni mwa nchi chache sana ambazo zinatii na kufuata haki za binadamu. Ni miongoni mwa nchi chache sana ambazo haki za binadamu hazitajwi tu, tumeziweka kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya Kwanza, sehemu ya tatu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi ya hayo...

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Taarifa.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Kwenye nchi yetu tunazo sheria zilizotuwekea utaratibu, tunayo *institutional and legal framework* ya namna... (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, muda hautoshi.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Hakuna mtu ametoa taarifa, Mheshimiwa Salome naomba unyamaze. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa naomba ukae nimeshasimama, naomba ukae. Waheshimiwa Wabunge tujifunze kuheshimu mamlaka...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Nasema hivyo kwa sababu, nisikilizeni. Mheshimiwa Susan Lyimo amechangia dakika zake tano hakuna mtu nimemruhusu kusimama, Mheshimiwa Lulida amechangia hakuna mtu amesimama na huyu mchangiaji wa CCM atachangia bila mtu kusimama. Mheshimiwa Timotheo Mzava. (*Makofii*)

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa hoja yangu ni hii, kwamba kwenye nchi yetu tunayo Katiba na tunazo Sheria za Haki za Binadamu na namna ambavyo mtu atakuwa anahisi haki za binadamu zimevunjwa, aende kwenye vyombo vyaya sheria kwenda kufuata haki hizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kushauri vitu viwili; cha kwanza niishauri Serikali. Niiombe Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje semeniju ya haya mambo, tusiache watu wakachafua nchi yetu. Mheshimiwa Kabudi ameenda Geneva, ametoa taarifa nzuri na amesifiwa lakini huku ndani watu hawajui.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nataka kushauri, kwa kuwa tunayo *legal* na *institutional framework* ya namna ya ku-deal na mambo ya haki za binadamu, niwashauri wenzangu, Watanzania wote twende kwa namna hiyo, tuache kuzunguka kwenye maofisi huko mara kwenye Mabalozi, tunao utaratibu wa kisheria na kikatiba wa namna ya ku-deal na vitu vya namna hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze jambo la pili kwenye diplomasia ya uchumi. Diplomasia ya uchumi ni dhana pana na inawezekana tunapata shida sana kuilewa, niwapongeze sana Mabalozi wa nchi yetu ambao wanatuwakilisha kule nchi. Balozi wetu wa China, Balozi wa Urusi wanafanya kazi kubwa, matokeo tunayoyaona kwenye utalii sasa hivi ni matokeo ya kazi kubwa wanayoifanya kwenye diplomasia ya uchumi. Hata kitendo cha Zimbabwe kukubali tupeleke mahindi tani zaidi ya 700,000 kwenye ziara ya Mheshimiwa Rais ni matokeo ya diplomasia ya kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wasichoelewa ni kitu kimoja, Sera yetu ya Mambo ya Nje, Toleo la Mwaka 2001 imejisimika kwenye diplomasia ya uchumi, lakini haina maana kwamba kwa sababu ya diplomasia ya kiuchumi tumeacha vitu vingine na hata sera ile imesisitiza kwamba tunaendelea kuimarisha misingi na kanuni za sera yetu ya asili ile ya mwanzo ambayo ilitokana na Serikali ya Awamu ya Kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mionganoni mwa kanuni za kwenye Sera yetu ya asili ya Mambo ya Nchi za Nje pamoja na kwamba ilikuwa ni kwa ajili ya kuangalia ukombozi wa nchi nyingine, ilikuwa ni kulinda uhuru wa Taifa hili. Kuja kwa sheria za kwenye Sekta ya Madini, mabadiliko tuliyoyafanya

ni ishara ya kulinda uhuru wa Taifa kwenda kutafsiri diplomasia ya uchumi ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niishauri tu Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje iendelee kutoa ushirikiano mkubwa kwenye mikataba na Mataifa mengine, kwenye mikataba ya wawekezaji ili katika kufanya kazi mambo hayo, tujitahidi kuhakikisha kwamba na zile dhana zote zinazohusiana na mambo ya diplomasia na uhusiano wa mambo ya nje zinazingatiwa vizuri kwa kuondoa mikwaruzano na maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana Serikali, tangu 2015 mpaka sasa tumeanzisha Balozi zaidi ya saba, mpaka juzi tumeanzisha Balozi nyingine ya Cuba. Kukubaliwa kuanzisha balozi kwenye nchi nyingine, yenyeewe ni ishara kwamba tuna mahusiano mazuri na nchi nyingine. Hii dhana inayojengwa kwamba tuna mahusiano mabaya, watu wanatupotosha. (*Makofii/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe sana Serikali, waendelee kusimamia mahusiano na nchi nyingine, waendelee kusimamia diplomasia ya Tanzania kwenye Mataifa mengine. Sisi tunamwamini Mheshimiwa Profesa Kabudi, Mheshimiwa Dkt. Ndumbaro na tunamwamini Mheshimiwa Rais, wafanye kazi kwa niaba ya Watanzania, nchi yetu ipate sura nzuri mbele ya ulimwengu na dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika mwongozo wako.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

NAIBU SPIKA: Soma Kanuni ya 68(8) inasemaje.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, unasisimama haraka, unasisimama haraka haraka aah. Unatakiwa ukae kwanza, unasisimama haraka haraka mno.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Yaani inakuwa kama una...

NAIBU SPIKA: Naomba mkae, naomba mkae, naomba ukae Mheshimiwa Mbilinyi...

MBUNGE FULANI: *Poor timing.*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli za Bunge niwakumbushe jambo moja, Mwenyezi Mungu ametupa akili ili tuzitumie sawasawa. Mheshimiwa Cosato Chumi alisisimama hapa akisema ana taarifa na mimi nikamkataza Mheshimiwa Chumi, nikasema watu wanaoruhusiwa ni wale wanaozungumza kuhusu utaratibu. Mnapiga kelele hapa watu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kana kwamba kuna mtu aliruhusiwa kutoa taarifa halafu ninyi mmenyimwa, ninyi ni watu wa namna gani mnataka kiti kiendeshwe kwa kelele zenu? (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Bunge hili tunazo Kanuni hizi ndizo zinazotuongoza na hakuna mtu anakaa hapa mbele ambaye hatumii Kanuni kufanya maamuzi. Nikikataa taarifa nimezikataa kote hata kama ni wa upinzani anayetaka, nikikataa hata kuhusu utaratibu maana yake nitakuwa nimekataza watu wote. Kwa hiyo, msijenge taswira kana kwamba mnaonewa wakati mko hapa mnatumia akili na nyie mnazo, ndiyo maana mko humu ndani mnaitwa Waheshimiwa. Msipende kupotosha mambo ya wazi kabisa, mkafikiri kwamba hiyo inawasaidia kwa kupiga kelele, si sawasawa. Kwa hiyo, ni lazima mjiheshimu kama mnavyoitwa Waheshimiwa na muheshimu kiti kama Kanuni zinavyowataka. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, wapo wageni ambao hawakupata fursa ya kutangazwa asubuhi. Wageni watatu wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es salaam...

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: (*Aliongea bila kutumia kipaza sauti*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbilinyi tafadhali, nikiwa nimesimama usizungumze, ndiyo utaratibu wa Kikanuni.

Wapo pia wageni watatu wa Mheshimiwa Steven Kiruswa, sijui kama wamepata fursa ya kuingia, haya tutawatangaza mchana.

Waheshimiwa Wabunge, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 mchana leo.

(Saa 7.02 mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza mtoa hoja, Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, kwa kuwasilisha Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara yake kwa umahiri mkubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea masuala mawili mafupi tu ndani ya muda huu mdogo nilionao ambayo

yamegusiwa na Msemaji Mkoo wa Kambi Rasmi ya Upinzani, Mheshimiwa Salome Makamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine nianze kwa upande huo vilevile kwa kumpongeza Mheshimiwa Makamba kwa kukiri mbele yetu kwamba nyuma ya mwanamke yeote mwenye mafanikio yupo mwanaume. Hii ni dhahiri kabisa kwamba ana familia yenyе furaha katika nchi hii. Mimi naomba nimkumbushe tu kwamba pale ambapo kuna familia yenyе furaha basi nyuma yake kuna Serikali inayojali na Serikali hiyo ni ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Msemaji Mkoo wa Kambi ya Upinzani ametoa picha ukurasa ule wa saba wa nchi yetu kuwa yenyе ukandamizaji mkubwa na amenukuu tafiti mbalimbali alizozisoma yeye. Mimi naomba tu nimkumbushe vilevile tafiti ambazo zimefanywa na vyombo vyenye heshima kubwa sana duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi inayoheshimika duniani upande wa *Travel Advisory, Atlas and Boots*, inatoa orodha ya usalama wa nchi duniani kila mwaka inaitwa *Global Peace Index*. Inasema kwa mwaka 2018 nchi 100 zilikuwa na hali mbaya sana ya usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitangaze hapa na niko tayari kuweka juu ya Meza hapo, kwamba Tanzania haipo kati ya nchi 100 hatari duniani. Nilizoziona humu ni Syria, Afghanistan, Russia, Pakistan, Uturuki, Israeli, Colombia, na USA ni ya 43, sisi kwenye 100 hatumo. USA yenywewe ambayo wengi wanadhani ni paradiso ya usalama ni ya 43. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi zilizobaki salama zingine ziko kama 80; Ufaransa (103), Vietnam (104), Uingereza (107), Qatar (108), Tanzania (113) yaani tuko juu ya hata hao. Ndiyo shida ya kunukuu hivi vitu, basi nukuu vyote ili kupata picha *comprehensive*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma *worldpopulationreview.com* inatoa orodha ya nchi 55 za kidikteta duniani, tena 55 imefikia mwisho, Tanzania siyo mojawapo. Kwa hiyo, ukitaka kuleta *data* hapa uwe *comprehensive*, jaribu kusoma nyingi uweze kupata picha kamili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, amedai vilevile kuwa kuna ukosefu wa uhuru wa vyombo vyahabari Tanzania. Anasema hii ndio dosari kubwa kwelikweli hapa nchini. Mimi nataka tu niwahoji wenzangu amba wanakuja na hiyo hoja mara kwa mara, wanaposimama hapa Bungeni hebu wanitolee mfano wa nchi moja tu yenye uhuru wa vyombo vyahabari usio na mipaka, nitafurahi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pengine wanafikiri ni hao wakubwa, sasa kama ni wakubwa, hivi kama wakubwa hawana mipaka ni kitu gani kinawafanya mpaka leo huu mwaka wa saba wanahangaika na Assange? Ni kitu gani kinawafanya mpaka leo wanahangaika na Snowden? Yote ni kwamba wamekiuka ule uhuru wa habari uliopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwasilitizie Watanzania na Waheshimiwa Wabunge kuititia kwako kwamba nchi zote zenye heshima duniani zimesaini Mkataba wa *Civil and Political Rights*, ile *convention* ya mwaka 1966. *Convention* hiyo inatoa uhuru kwa vyombo vyahabari lakini kwa shartilaa kwamba usiingilie uhuru na haki ya mtu mwingine na usihatarishe usalama wa nchi yako. Sasa kama unahatarisha usalama wa nchi yako wewe utakaa kwenye nchi gani? Kwa hiyo, ndio maana nchi zote zinasema sisi tunafuata uhuru wa vyombo vyahabari lakini tunazingatia hiyo *International Convention* ya *Civil and Political Rights*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema tu kwamba Tanzania tunapewa *marks* kubwa kwa sababu ya utayari wetu na vilevile kuwa *champions* wa kuanzisha vyombo vyahabari ulinzi wa haki za binadamu. Nimefurahi sana leo *Chief Whip* hapa ameelezea kuhusu Mahakama zote za

Afrika na za kimataifa ziko Arusha kwa sababu ya *track record* ya *human rights* ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ndiyo tulikuwa waanzilishi wa hoja tuwe na *East African Court of Justice* hapa na Mahakama ya Afrika. Siyo hiyyo tu, Mahakama ya Afrika tukawa moja ya nchi tano tu tuliookubali wananchi wetu watupeleke kwenye hiyo Mahakama kama kuna ukiukwaji wa haki za binadamu, tano, kati ya nchi zote za Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Sasa ni zamu ya Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Usimame hapo hapo Mheshimiwa, una dakika 15.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi ya kipekee, kama wenzangu walionitangulia, kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake madhubuti na makini unaoendelea kugusa, siyo tu wananchi wa Tanzania, bali wa kuigwa katika nchi za Bara la Afrika na dunia kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wake ndani ya Bunge hili. Aidha, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa namna ambavyo mnaliongoza Bunge hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kumpongeza kwa kipekee, Mheshimiwa Prof. Palamagamba Aidan Mwaluko Kabudi, Mbunge, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa uongozi makini na kuhakikisha tunapata ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara anayoiongoza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu na Mheshimiwa Najma Martaza Giga kwa namna wanavyoonesha uwezo mkubwa wa kuongoza Bunge katika kipindi hiki. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya NUU kwa ushauri na maoni yao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Pia nawashukuru sana Wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano wao wanaoendelea kunipa. Nawaombea kila la heri katika utekelezaji wa majukumu yao hapa Bungeni na kwenye majimbo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee, napenda kuwashukuru wananchi wenzangu wa Jimbo la Songea Mjini kwa imani kubwa wanayonipa na wanayoendelea kuionesha. Nitaendelea kuwa nao karibu na kushirikiana nao katika kuleta maendeleo makubwa na naahidi kuwa sitawaangusha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru sana familia yangu, ikiongozwa na mke wangu mpandwa, Flora Ndumbaro, kwa uvumilivu kwangu na kwa namna wanavyonisaidia na kuniunga mkono katika majukumu yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, shukrani za dhati ziende kwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Mabalozi, Wakurugenzi, Watumishi na wasaidizi wangu katika Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa ushauri na msaada wao katika utekelezaji wa majukumu yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, nianze sasa kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Ni dhahiri kwamba michango yao itatusaidia sana katika kufanikisha shughuli za Wizara na kuimarisha ufanisi wa utendaji wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ambayo napenda kuiongelea ni suala la kuondoka kwa Balozi wa Jumuiya ya Ulaya hapa nchini. Mtoa hoja alisema Serikali ileze ni kwa nini iliweka shinikizo la kumwondoa Balozi huyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wizara na kama Serikali tulipokea tamko kutoka ka wenzetu wa Jumuiya ya Ulaya mnamo tarehe 5 Novemba, 2018 likisema kwamba limemuita Balozi huyo nyumbani kwa majadiliano. Suala la kuja Balozi yejote hapa nchini, kuishi kwake na kuondoka kwake kunaratibiwa na Mkataba wa Vienna unaohusu mahusiano ya kidiplomasia wa mwaka 1961. Katika mkataba huu, nchi ambayo imemleta Balozi huyo ina mamlaka ya kumwondoa pasipo kutoa sababu kwa nchi nyingine yoyote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tulipata taarifa ya kuondoka kwa Balozi huyu hatukupewa sababu yoyote ile. Hivyo, kututaka leo tutoe sababu wakati sisi siyo tuliomwondoa na sisi hatukuambiwa ni kwa nini ameondoka, siyo sahihi. Waliomwondoa ndiyo wako kwenye nafasi ya kutoa sababu ni kwa nini walimuondoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna hoja ya *Brexit*. Mtoa hoja amesema Serikali itoe msimamo wake kuhusiana na hoja ya *Brexit*. *Brexit* ni hatua ya Uingereza kujitoa katika Jumuiya ya Ulaya. Sisi tuna mahusiano mazuri na Jumuiya ya Ulaya na Uingereza lakini pamoja na mahusiano hayo mazuri hatuingili mambo yao ya ndani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu za Uingereza kujitoa zinamhusu yeye, kwa sababu sera yetu sisi hatuingilii mambo ya ndani, tunasubiri maamuzi ya mwisho ya *Brexit*. Endapo watajitoa ndipo tutaanza mchakato wa kuanzisha mahusiano binafsi na Uingereza au wataalam wanasesma *bilateral relations*. Kwa hivi sasa kwa kuwa mahusiano yetu na Jumuiya ya Ulaya ni mazuri tusingependa kuingia katika suala hili la Ulaya na *Brexit*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la *EPA* liliongelewa na kusema kwamba nchi nyininge zimeshasaini *EPA* ispokuwa sisi. Naomba nitoe taarifa kwamba zaidi ya asilimia 50 ya nchi za Afrika hazijasaini *EPA*. Katika Afrika Mashariki, kati ya nchi sita ni nchi mbili tu zimesaini *EPA*, nchi nne, ambazo ni nydingi, hazijasaini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hawajasaini siyo kwamba hawaipendi, nchi nydingi ikiwemo Tanzania tume-*raise concern*. Sisi Tanzania tumehoji vifungu nane vyta mkataba wa *EPA*. Katika vifungu nane hivyo tume-*raise issues* 12 ambazo tunasema zikiwa-*addressed* tutasaini mkataba wa *EPA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya *issues*, niwasaidie tu, ni kwamba mkataba huo unakwenda kupoka mamlaka ya Bunge hili hasa kwenye kutunga sheria zinazohusiana na fedha au kodi. Sasa hatuwezi kusaini mkatana ambao unapoka mamlaka ya Bunge pasipo Bunge lenyewe kuridhia. Kwa hiyo, suala hilo siyo la kwetu sisi tu, ni la Bunge hili na ni la Watanzania wote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, imeongelewa pia hoja kuhusiana na haki za binadamu. Naomba niseme, haki za binadamu ni suala mtambuka na zinaangaliwa sana kwa mujibu wa Kikanda. Sisi Afrika tuna Mkataba wa Afrika wa Watu na Haki za Binadamu, wenzetu wa Ulaya wana Mkataba wa Haki za Binadamu, neno watu halipo, hiyo ni tofauti kubwa sana ya mtazamo wa haki za binadamu kati ya Afrika na Ulaya. Ndiyo maana sisi kwa muktadha wetu tumeanzisha Mahakama yetu iliyoko pale Arusha ili masuala

ya haki za binadamu kwa muktadha wa Kiafrika tuyashughulikie kwenye Mahakama zetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokuja sasa kuanza kucheza ngoma ambazo siyo za kwetu tunakuwa tunapotoka. Kwenye hili, naomba nirejee ushauri mzuri aliyoutoa Mheshimiwa Mnzava kwamba katika kutatua changamoto za haki za binadamu Tanzania tuna mihimili ya kutosha; tuna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mahakama Kuu ambayo ina mamlaka kwenye haki za binadamu, Mahakama ya Afrika Mashariki ambayo pia inashughulikia haki za binadamu na Mahakama ya Afrika inayoshughulikia haki za binadamu ambayo iko Arusha. Kwa kuonesha umuhimu Mahakama hizi mbili, ya Afrika Mashariki na ile ya Afrika, ziko Tanzania, ziko Arusha, tumeziweka hapa kwa sababu tunapenda na tunalinda haki za binadamu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tu niseme katika haki za binadamu tuko vizuri pengine kuliko nchi ambazo watu wengi wanaziongelea. Niwape mfano tu, kuna nchi ambazo tunazisema sana humu ndani, hazijasaini Mkataba wa Haki za Mtoto Duniani lakini mnadhani kwamba hizo ndiyo zinatimiza haki za binadamu. Nchi hizo hazijasaini Mkataba wa *Rome Statutes* ambao unashughulikia masuala ya *ICC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwenye kipengele cha haki za binadamu tuko vizuri. Tufuate vyombo hivi ambavyo vipo, tuache kupeleka masuala ya haki za binadamu sehemu ambako hakuhusiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii, kwa namna ya kipekee, kumpongeza sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi. Najua wengi wangetamani Mheshimiwa Prof. Kabudi aweze kujibu mambo ambayo siyo mazuri. Mheshimiwa Prof. Kabudi anafanya kazi vizuri, tuna wazalendo wachache sana nchi hii kama yeye. (*Makof/Vigelegele*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, watu huwa tunasubiri mpaka mtu afe ndipo tumsifie.

Naomba mimi nimsifie Mheshimiwa Profesa Kabudi wakati bado anaishi na angalau na yeye mwenyewe apate pongezi hizi. (*Makof*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

NAIBU SPIKA: Kanuni inayovunjwa Mheshimiwa Mbilinyi?

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu, nikishaeleza ndiyo nitasema, naomba nafasi kwanza.

NAIBU SPIKA: Unasimama kwa mujibu wa Kanuni gani? Usiwe mbishi bila sababu na wewe ni Mbunge wa siku nyingi, kanuni inayovunjwa ni ipi. (*Makof*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, endelea.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbilinyi, naomba ukae, Mheshimiwa Naibu Waziri endelea.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, wazalendo kama Mheshimiwa Prof. Kabudi ni wachache. Hii ni tunu ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia, tunapaswa kuienzi na kuilinda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Prof. Kabudi ameifanyia mema nchi hii, mambo ya kihistoria, ametuletea sheria mbalimbali nzuri na anaongoza Wizara hii kwa ufanisi wa hali ya juu. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote tuchukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Prof. Kabudi, tumtakie maisha marefu ili aendelee kutumikia Tanzania kizazi na kizazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

WABUNGE FULANI: Unga mkono hoja.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. (*Makof*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite mtoa hoja aje ahitimishe hoja yake, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, karibu. (*Makof*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara muda wa asubuhi na sasa kuniruhusu kufanya majumuisho ya mjadala.

Nakushukuru kwa kuongoza mjadala wa bajeti yetu kwa umahiri na kwa msingi huo, maoni na michango iliyotolewa yameiwezesha Wizara kupata maoni na ushauri utakaotusaidia kwenye kutekeleza majukumu yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ulivyoendesha kikao leo mimi nimefurahi sana, kwamba leo Mabalozi ambaao kwao Bunge lao huwa ni zogo na fujo, wameona jinsi ambavyo Bunge hili ni la kistaarabu pamoja na kelele chache. Sisi ambaao tumepata bahati nadra sana kuishi huko,

tumeona Mabunge yao, viroja vyao, vituko vyao, wale waliodhani leo watafanya viroja ili Wazungu watuone hatufai, sasa tumewadhihirishia hao Wazungu kwamba sisi tuko mbali sana. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwaambie na natamani wawepo; Ujerumani Spika mwanamke alikuwa haruhusiwi na walipoamua kuwa na Spika mwanamke, anaitwa Clara Zetkin, ilibidi wamtungie sheria kumtangaza kuwa mwanaume ili aweze kuwa Spika. (*Makofi*)

WABUNGE FULANI: Ahaa.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu anavaa suruali ilibidi wapitishe sheria ya kumruhusu kuvali suruali. Sasa sisi tumeishi huko tumeyaona hayo tunayafahamu hayo sisi hapa hakuna suala la mwanamke kuwa Spika kule bado ni *issue* tena kubwa sana. Kwa hiyo, nimefurahi sana leo tumeonyesha umahiri wetu na uungwana wetu kwa kiasi kikubwa na kwa namna hiyo nakupongeza sana ulivyoendesha kikao cha leo, ulivyosimamia kanuni na ulivyozitafsiri. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee naishukuru kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nje ya Ulinzi na Usalama chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, na wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa waliotupatia wakati wa maandalizi ya bajeti na kwa hotuba nzuri waliyoitoa. Tunashukuru kwa maelekezo, maoni na ushauri ambao kamati hii imekuwa ikiupata na nataka niahidi yale yote ambayo leo wametushauri Wizara itayazingatia na itayatekeleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Salome Wickliffe Makamba nina mwendi labda nitoe siri leo. Salome Wickliffe Makamba marehemu baba yake Wickliffe Makamba na mama yangu Patricia Mwendi ni mabinamu na ndiyo maana mtoto wake anajina la babu yangu Mwendi, kwa hiyo mfahamu nafurahi sana mimi niko huku yeye yuko huko tumetoa hotuba leo na leo Gairo, Mamboya, Berega, Magubike wamefurahi sana kwa hiyo tumepokea maoni na ushauri ulioutoa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee namshukuru sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Phillip Mahiga, Waziri wa Katiba na Sheria ambaye hapo awali alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Mahiga aliweka msingi mzuri katika Wizara hii ambayo inaniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Mahiga kwa ushirikiano mkubwa alionipa mara mbili Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alinituma niende pamoja na Mheshimiwa Dkt. Mahiga nje na nilijifunza mengi sana kwake katika mikutano hiyo nje na leo hii namshukuru hakuwa mchoyo wakati huo kuniandaa leo kuchukua na kuvali viatu vyake ingawa dhahiri ni vikubwa lakini namshukuru sana pia anavyoendesha Wizara ya Katiba na Sheria nilikotoka. Mwalimu na mwanafunzi wanapopokezana vijiti ni jambo la fahari na ni nchi chache kitu kama hicho kinatokea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu naomba kumshukuru Dkt Damas Ndumbaro Naibu Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hii kwa kipindi cha miezi takriban miwili na toka niingie kwenye Wizara hii amekuwa na mchango mkubwa katika utendaji kazi wangu na ufanisi wa Wizara. Yeye amesafiri mara nyingi nje ya Nchi kuliko mimi na huko ametuwakilisha vizuri sana nichukue fursa hii kumpongeza sana alivyotuwakilisha vizuri Argentina, alivyotuwakilisha vizuri Brussels, Pretoria, Kigali, Uganda amefanya kazi nzuri na mimi najivunia sana kazi yake. (*Makof!*)

Mheshiiwa Naibu Spika, pia nimshukuru Katibu Mkuu Dkt. Faraji Mnyepe, Naibu Katibu Mkuu Mheshimiwa Balozi Muombwa Mwinyi, Mabalozi wote wote Wakurugenzi Wakuu wa vitengo na watumishi kwa kujituma ni imani yangu kuwa ushirikiano huu na kujituma kwenu kutaimarika wakati mnatekeleza bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mjadala wa bajeti yetu jumla ya Waheshimiwa Wabunge 13 wamechangia kwa maandishi na jumla ya Wabunge wanenamna wamechangia kwa kuongea kwa namna ya pekee nawashukuru Wabunge waliochangia kwa kuongea na maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yao mizuri waliyoitoa wakati wa majadiliano hapa Bungeni, tumepokea maoni mazuri ambayo yamelenga kuboresha utendaji wa kazi wa Wizara na Sera ya Kidiplomasia ya kiuchumi ni dhahiri Waheshimiwa Wabunge wote wanatamani kuona mchango wa Wizara hii katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwashakikisha kuwa chini ya uongozi wangu na viongozi wengine wa Wizara tutashakikisha kuwa mfumo wa utendaji kazi wa Wizara unabadijika na Wizara inatoa mchango stahiki na kwa ujumla maoni na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati wakichangia bajeti hii ni ushahidi kwamba Bunge hili linatambua umuhimu wa mapendekezo ya kujenga hoja. Kwa hiyo, ningependa niangalie nifafanue baadhi ya hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ningependa nieleze msingi wa sera yetu ya mambo ya Nje umewekwa bayana na Baba wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere katika waraka aliotoa kwa watumishi wote wa Wizara ya Mambo ya Nje unaitwa *argue don't shout* na inasema *an official guide on foreign policy by the President* na katika Waraka huu wa *argue but don't shout* mwalimu ameweka wazi baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, aliloliweka wazi ni kututaka tujuje dunia inabadilika lakini pamoja na dunia kubadilika mambo ya msingi tuyashikilie lakini tujuje kuna wakati itabidi tubadilishe mbinu na mikakati ya kufikia lengo tunalolitaka. Mwalimu hakutuambia tushikilie misingi tu na kuacha kuangalia hali halisi ya dunia alitutaka tuangalie hali halisi ya dunia bila kupoteza misingi. Na wengi siku hizi wanamzungumza Mwalimu bila kuwa na uhakika wa yale wanasesma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu hakuwa ni mtu ambaye alikuwa anakubali nchi hii iburuzwe. Kuna nyakati Mwalimu alichukua maamuzi katika sera ya Mambo ya Nchi za Nje ambao wengi hawakuyatazamia mwaka 1964 Tanganyika na Zanzibar zilipoungana. Tanganyika palikuwa na Ubalozi wa Ujerumani Magharibi, Zanzibar palikuwa na Ubalozi wa Ujerumani Mashariki, mara baada ya Muungano huo Ujerumani Magharibi ilitaka kumlazimisha Mwalimu kuiondoa Ujerumani Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu aliwaomba muda ili jambo hilo lishughulikiwe kwa utaratibu Wajerumani kwa sababu ndio waliokuwa wanaipa Tanzania misaada mingi kuliko nchi yoyote walidhani wanaweza kumburuza akubali maoni yao. Wale wote wenye umri mkubwa kuliko mimi wanajua, Mwalimu alichukua hatua ambayo hawakuitarajia. Moja aliwafokuza wataalam wote wa Kijerumani Isipokuwa Wamissionari, pili aliwarudishia Wajerumani fedha yao *doch mark* milioni 40 na Jengo la Nkurumah Hall Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambalo sasa halijamalizwa Mwalimu alisema limaliziwe.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Kuhusu Utaratibu.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Lakini pia Mwalimu alichukua hatua nyingine kubwa mwaka 1965 Wazungu wabaguzi...

NAIBU SPIKA: Naomba ukae Mheshimiwa ukiniona nakuongelesha hivyo ni kwa sababu sitaki kukukumbusha

kanuni zinasemaje huyu aliyesimama hapa ni Waziri mtoa hoja. Kanuni yako inasemaje? Naomba ukae Mheshimiwa Mwakajoka. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Na wakati huo wale Wazungu wachache wa Arodesia walipojitangazia uhuru Umoja wa Nchi za Afrika ulitoa maa zimio kwamba Uingereza iwaondoa Wazungu walowezi wachache Rodessia katika utawala na wasipofanya hivyo nchi za Afrika zivunje uhusiano wa Kibalozi na Uingereza.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nchi mbili tu zilifanya hivyo ni Ghana na Tanzania, na matokeo ya Ghana kuvunja uhusiano wa kibalozi na Uingereza marehemu Kwame Nkurumah alipinduliwa na wanajeshi wakiongozwa na Achlempong alliesoma *San Hast* nchi ya pili kufanya hivyo ilikuwa na Tanzania ilivunja uhusiano wa Kibalozi na Uingereza kuanzia mwaka 1965 mpaka mwaka 1972 Kerbado Mwalimu aliwarudishia Waingereza msaada waliokuwa wameuleta wa paundi milioni tano, huyo ndiyo Julius Kambarage Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hoja za leo ninazosikia watu watatamani tupate misaada hiyo na tuvunje misingi. Watu watatamani tupige magotii ili tupate misaada. Nasema hivi chini ya utawala huu wa Chama cha Mapinduzi nchi hii haitapiga magoti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kamwe nchi hii haitapiga magoti wamethhubutu wameshindwa hii ndiyo nchi pekee katika Bara la Afrika haijashindwa vita hatukushindwa Uganda, hatukushindwa Sychelles, hatukushindwa Comoro hii ndiyo nchi pekee imewapeleka wapigania uhuru kwao tumewapeleka Zimbabwe, tumewapeleka Msambiji, tumewapeleka Namibia hii ndiyo nchi ili yopokea watu wenye shida wengi kuliko wote na kwa kufanya hivyo Mwalimu alilipa ghamama kubwa ambayo Dkt. Magufuli atailipa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu kwa kusaidia nchi hizo aliiwa *M-communist* na mimi nilishangaa kwa mara ya kwanza tunamkatoliti *m-communist* na hila hizo hizo husuda hiyo hiyo wivu huo huo upo sasa kwa sababu nchi hii chini ya Dkt. Magufuli tumeamua kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na mara nchi ya Afrika inapoamua kujitegemea maadui wanatumia vibaraka ndani ya nchi, mabaraka ndani ya nchi...

WABUNGE FULANI: Wako humu, wako humu ndaniii!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni usaliti kwa nchi yetu tusikubali kuwa mabarakara wa mabeberu tusikubali kutumiwa hii nchi ni yetu. Niwakumbushe mara baada ya hali ngumu ya uchumi mwaka 1985 Benki ya Dunia na Benki ya IMF walipozilazimisha nchi zote kutuacha na nchi za mwisho kutuacha ilikuwa ni nchi za Nordic. Bado nchi hii ilisimama haikupiga magoti haiwezi kupiga leo magoti wakati tuna *foreign reserve* ya miezi mitano hatukupiga magoti wakati hatuna *foreign reserve* wakati mzee Mwinyi anaingia hatuvezi kupiga magoti leo tuna *foreign reserve* ya miezi mitano aslan kamwe halitatokea hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndio maana Mwalimu kwenye hii *argue don't shout anatutahadharisha* anasema wale wa nje ni *opponents* hawa wa ndani wanaokuchimba ndio *enemies* kwa hiyo, *we are facing enemies internally but we are facing opponent outside our enemies are eternal outside are opponents.* (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijibu hoija mbalimbali. Ya kwanza ni hoja kuhusu Tanzania kuwa na kigugumizi kuridhia mkataba wa makubaliano ya eneo huru la biashara Barani Afrika – AFTA. Serikali ieleze Bunge ni lini itatuletea mkataba huo Bungeni ili uridhiwe. Ningependa kusema hivi, mkataba huu tumekwisha usaini Tanzania imeusaini mkataba huu na saa hizi tuko katika mchakato wa kuupitia ili tuone faida zake na...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mbilinyi, Mheshimiwa Prof. Kabudi naomba unyamaze kidogo Mheshimiwa Mbilinyi na Mheshimiwa Salome na Mheshimiwa Mwakajoka tafadhalini sana. Mheshimiwa Mwakajoka tafadhalii, Mheshimiwa Mbilinyi tafadhalii na Mheshimiwa Makamba nimewataja hii ni mara ya mwisho hii ni mara ya mwisho Chief Whip wa *opposition* nimewataja Wabunge wako watatu mara ya mwisho. Mheshimiwa Prof. Kabudi.

Naomba ukae Mheshimiwa Selasini kwa sababu unaufahamu utaratibu nimekuambia nimewataja Wabunge wako kwa sababu we ndiyo kiongozi wako na uwambie watulie wamekaa hapo karibu na wewe. Mheshimiwa Kabudi naomba uendelee.

MHE JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa mimi ni *Chief Whip*.

NAIBU SPIKA: *Chief Whip* hausimami akiwa amesimama Waziri Chief Whip huwezi kusimama akiwa amesimama Waziri hata yeye angekuwa amesimama wakati Waziri amesimama hawezi kusimama naomba ukae, naomba ukae Mheshimiwa Selasini. Naomba uendelee Prof. Kabudi

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala kwamba hakuna takwimu za Kitaifa zinazoonyesha idadi kamili ya Watanzania wanaoishi Nje ya Nchi, na kile wanachokifanya huko. Na kwamba Serikali inapaswa kuhakikisha inaanizisha kanzi data ningependa kueleza kwamba hivi sasa Wizara inaendelea na maandalizi ya Sera ya Taifa ya Diaspora na yapo katika hatua nzuri. Mara baada ya kukamilisha sera hiyo tutaingia katika hatua ya kuwaandikisha Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Watanzania kuandikishwa ni la hiari kwa hiyo tunawaomba watananzia wote wanaoishi Nje ya Nchi wasikose kwenda kujiandikisha kwenye balozi zetu ili tuweze kuwatambua na kuwafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uraia wa Tanzania ningependa kueleza kwamba suala la uraia linasimamiwa na Sheria ya Uraia Namba 6 ya mwaka 1995 ambayo imebainisha kuwa uraia wa Tanzania upo katika makundi matatu uraia wa kuzaliwa, uraia wa kurithi na uraia wa tajinisi (kuandikishwa) kwa mujibu wa sheria hiyo, aina ya uraia wa kuandikishwa uraia wa pacha haupo katika sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kubadili msimamo kwamba Tanzania imebadili msimamo wake kuhusu ushirikiano na nchi za Morocco na Israel na je mabadiliko hayo ya msimamo wa nchi yanalindwa na yaliridhiwa na Bunge? Na nini msimamo wetu kama Taifa juu ya tabia za kidikteta, ukiukwaji wa haki za kibinadamu, unyanyasaji na uonevu zinazoanza kuibuka na kujionyesha wazi mionganoni mwa baadhi ya viongozi wa Mataifa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa nieleze kwamba Tanzania haikuvunja uhusiano na Israel mwaka 1973 kwa sababu ya suala la Palestina. Tanzania ilivunja uhusiano wa kibalozi na Israel mwaka 1973 kwa sababu baada ya Israel kuzishambulia nchi za Kiarabu na kuteka maeneo ya Sinai kwa upande wa Misri na kuteka maeneo ya Golan kwa upande wa Syria hiyo ndiyo ilikuwa sababu iliyofanya Tanzania wakati huo kuvunja ushirikiano wa Kibalozi na Israel.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nchi mbalimbali ikiwemo nchi ya Misri yenyeewe na nchi nyingi za Kiarabu zimeanzisha uhusiano wa kibalozi na Israel. Hatuoni sababu sisi kutokuanzisha uhusiano wa ubalozi na Israel. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuanzisha uhusiano wa kibalozi na Israel na kufungua ubalozi hakujatuondoa katika msimamo wetu wa kuunga mkono harakati za Wananchi wa Palestina. Na msimamo wetu uko wazi wala hauna kigugumizi, wala hauna tashwishwi tunasema tuwe na Israel iliyo salama na tuwe na Palestina

iliyohuru katika hilo hatubadilki na ndiyo maana mpaka leo tunavyozungumza mionganii mwa nchi ambazo zimeitambua Palestina na zina ubalozi wake hapa nchini ni Tanzania Palestina wana ubalozi wao Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo uhusiano wetu wa kibalozi na Israel hata kidogo hautatuondoa sisi kusimama kwa upande wa Palestina. Na ndiyo maana kama kuna nchi ambayo tumepeiga kura kuunga mkono maazimio yake katika Umoja wa Mataifa, ni Palestina. Nina orodha ya maazimio 23 ambayo Tanzania imepiga kura *in favour of Palestine*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningependa kuwahakikisha kwamba hatujatetereka lakini ni ukweli leo hii huwezi kuacha kuwa na mahusiano na Israel wakati nchi zote za Kiarabu zinamahusiano na Israel na yako mambo ambayo tunayahitaji kutoka Israel katika upande wa uchumi, upande wa kilimo, upande wa IT. Lakini hilo halitatuondoa katika kusema kwamba Palestina iwepo na iwe huru lakini pia Israel iwepo na iwe salama na maazimio hayo yapo mtu ambaye anapenda kuyapata atayapata jinsi ambavyo Tanzania imepiga kura kuunga mkono Palestina katika mambo yake mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Morocco na Saharawe na mgogoro wa Morocco Saharawi kwenye eneo la Sahara Magharibi. Tanzania inaunga mkono juhudzi za Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika katika usuluhisho wa mgogoro huo, Tanzania inaendelea kuzishi pande zote kukaa kwenye meza ya mazungumzo ili kupata suluhu ya kudumu ya mgogoro huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, na ndiyo maana kutokuegemea upande wowote tumekuwa tunahudhuria mikutano yote inayohusu Saharawi, tunahudhuria mikutano yote inayohusu Morocco. Na niseme hivi hata nchi hizo zenyewe ambazo zinawahisani watu wa Saharawi zinauhusiano wa kibalozi na Morocco mfano wa nchi hiyo ni Algeria na nchi ya Morocco kufungua ubalozi wake hapa

nchini haukuifanya sisi tuiambie Saharawi ifunge ubalozi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo leo Tanzania Saharawi ina ubalozi wake Morocco inaubalozi wake na sisi tunashirikiana na wote bila kuwabagua na tunawahimiza wamalize matatizo yao kwa kufuata maazimio ya Umoja wa Mataifa. Na tunaishukuru Algeria ambayo pamoja na mvutano wote haijavunja uhusiano wa kibalozi na Morocco hata wakati nchi nyininge zilipovunja uhusiano wa kibalozi na Morocco. Kwa hiyo hatuoni sababu ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa hoja alizozitoa Mheshimiwa Suzan Anselem Jerome Lyimo Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA ambaye ameishauri Serikali kufanyia kazi changamoto za kupandishwa vyeo watumishi wa Wizara ambao wamekaa kwenye cheo kimoja kwa muda mrefu. Na kutaka kujua Serikali inampango gani wa kupeleka mbadala wa watumishi waliorudi Makao Makuu kwenye Balozi zetu na kuishauri Wizara kutoa mafunzo ya Kideplomasia kwa mabalozi wetu wanaoenda kuhudumu kwenye Balozi zetu nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba tayari katika mwaka huu wa fedha tunaoumaliza jumla ya wafanyakazi 87 wamepandishwa vyeo, 66 wamepandishwa vyeo na 21 Wizara imependekeza wapandishwe vyeo vyta huo msereleko. Tunayo barua kuotoka Ofisi ya Rais, Manajimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye Kumb. Na. BC.46194/03D/44 ya tarehe 16 Aprili 2019 na barua yenye Kumb. Na. BC.46/97/03D/45 ya tarehe 30 Aprili, 2019. Barua hizi zimetoa kibali cha kuwapandisha vyeo jumla ya watumishi 66 na kuwababilisha kazi *recategorization* jumla ya watumishi watatu. Jitihada hiyo itaendelea kama ambavyo tumekuwa tunafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala kutoa mafunzo ya kidiplomasia kwa Mabalozi wetu wanaoenda kuhudumu kwenye Balozi zetu. Ningependa kulihakikishia Bunge lako

tukufu kwamba hicho ndicho kinachofanyika, hakuna Balozi anayepelekwa nje bila kufanyiwa mafunzo katika Chuo cha Diplomasia. Sio Mabalozi tu hata Watanzania ambao wanaochaguliwa kwenda kufanya kazi kwenye Mashirika ya Kimataifa ambao Serikali imeawaidhinisha waende, nao pia wanafanyiwa mafunzo haya na ninakubaliana na yeze kabisa kwamba kuna umuhimu wa sisi wote kujifunza *etiquette* za Kibalozi na Kidiplomasia ikiwa ni pamoja na Wabunge ili tuweze kuelewa hizi *etiquette* za kidiplomasia zinatakiwa ziwe namna gani.

Mheshimiwa *etiquette* Spika, kuhusu Mheshimiwa Riziki Said Lulida wa Lindi ambaye ameulizia suala la mjisiti toka Tendaguru, Lindi au kwa jina la kiingereza *Dinosaur*. Ningependa nieleze kwamba ni kweli ukienda kwenye Jumba la Makumbusho ya Elimu ya Viumbe yaani *Museum for Natural Historyya* ...yako masalia ya *Dinosaur* wa sita kutoka Tanzania ambayo wakati huo ilikuwa chini ya utawala wa Wajerumani na kwa kweli masalia hayo yalitolewa Tendaguru na ukifika pale wameeandika yametolewa Tendaguru, Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, masalia hayo ni mchanganyiko wa mifupa halisi mjisiti mkubwa *Dinosaur* na *cas, cas* ni maeneo ambayo mifupa haikupatikana walitengeneza ili kukamilisha umbo la wanyama hawa. Masalia yalichukuliwa kutoka kilima cha Tendaguru kuanzia mwaka 1909 mpaka mwaka 1913 wakati wa ukoloni wa Mjerumani.

Mheshimiwa Naibu Spika, takribani tani 250 za masalia pamoja na mimea silichukuliwa na kupeleka Ujerumani. Majina ya kitaalamu ya *Dinosaur* hao ni *Brachiosaurus, Branchai, Kentrosaurus, Diastosaurus, Digasaurus, Erliophosaurus*, Bambegi na Arosaurus na huyu *Brachiosaurus Branchai* ni mrefu na anachukua urefu wa ghorofa tatu. Na mimi kwa miaka tisana na siku nne nilizoishi pale Berlin hakuna Watanzania waliokuja kunitembelea sikuwapeleka kwenda kuyaona hayo masalia ya *Dinosaur* ni makubwa na bado ipo mifupa mingine ambao ipo kwenye sera ipo kwenye maghala ambayo bado hayajaunganishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo upo umuhimu wa Serikali ya Tanzania na Serikali ya Ujerumani kuzungumza kuhusu suala hilo. Kabla ya Ujerumani Mgharibi na Ujerumani Mashariki kuungana, Ujerumani Mashariki ambapo ndipo yalipokuwa hayo masalia kwenye Chuo Kikuu cha Berlin walikuwa wameanza utaratibu wa kujenga Makumbusho ya Elimu ya Viumbe hai Arusha ili waweze kuleta *leprechaun* mfano wa hao *Dinosaur*. Kuna umuhimu tena wa kufufua mazungumzo na Serikali ya Ujerumani ili tuchukue hiyo hatua ya kwanza kabla ya kuingia kwenye hiyo hatua ya pili ya kuomba masalia haya yarudi. Kwa sababu yanahitaji utaalamu wa hali ya juu kuyatunza na tunadhani hali ya hewa ya Arusha inafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ombi lake kwamba watu wa Tendaguru waweze kufaidika na mijusi hawa ambao wapo Berlin, wazo hilli tumelichukuka na sisi tutazungumza na Serikali ya Ujerumani kuona ni kwa kiasi gani Wajerumani na hasa wanaohusika na mambo ya utafiti wataikumbuka Tendaguru ambapo hao mijusi walichukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Timotheo Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijiini kwa maelezo aliyyoatao kuhusu hali ya haki za binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Machi tulipata nafasi ya kwenda kwenye Baraza la Haki za Binadamu la Umoja wa Kimataifa na tulipofika palikuwa tayari taarifa zimepelekwa nyingi sana kwamba Tanzania hali ya haki za binadamu haiko sawasawa. Tulitoa maelezo na maelezo yale yaliwaridhisha na kwa maana hiyo Kamishna wa Haki za Binadamu wa Umoja wa Mataifa aliiondoa Tanzania katika ripoti yake ya nchi zinazovunja haki za binadamu, aliiondoa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaeleza bayana wenzetu kwamba moja hakuna haki ambazo hazina mipaka, haki zote zina mipaka. Mipaka hiyo imewekwa ndani ya Katiba wazi kabisa, hakuna uhuru wa yoyote kuingilia uhuru wa mtu mwengine. Kwa hiyo, mpaka wa kwanza wa haki za

binadamu ni pale haki ya mtu mwagine inapoanza. Kwa hiyo, hakuna haki ambayo haina mpaka na Katiba yetu imeweka wazi kabisa katika Ibara ya 30 ni mipaka gani imewekwa kuhusu haki za bindamu nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, na kama iliyoelezwa sisi mahakama zetu na tatizo kubwa tulionalo sisi na hapo wa kulaumia ni mimi na Dkt. Mwakyembe. Kosa kubwa tulilolifanya mimi na Dkt. Mwakyembe ni kutokuandika *commentary* ya Katiba yetu. Kwa hiyo, watu wengi wanaposoma haki za binadamu wanazisoma silivyo ndani ya Katiba bila kuwa na *commentary* ya kuwaonesha ibara hii ya Katiba tayari Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa imetoa tafsiri hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishe sisi ndio nchi inayoongoza katika hukumu zetu za haki za bindamu kuwa *cited* na Mahakama za nchi nydingine za *Commonwealth*. Kesi ya kwanza ilioamuliwa na Mahakama Kuu iliyotupa umaarufu mkubwa kabisa na kunukuliwa na mahakama zaidi ya 56 ni kesi ya *Horaria vs Pastory*. Horaria binti wa Kihaya ambaye alizuiwa kurithi mali kwa sababu ni mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama Kuu ya Tanzania kuhumu ya Jaji Mwalusanya ilisema haki hiyo, sheria hiyo ya mila inavunja Katiba na baada ya hapo hiyo ndio imekuwa *reference* ya nchi nydingi kuhusu haki za wanawake zinapovunjwa na sheria za kimila. Kwa hiyo sisi Tanzania tumepiga hatua kwamba hata sheria za kimila zimebekewa mpaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hivi majuzi zimetoka kesi mbili maamuzi ya Mahakama ya Rufaa kwenye kesi ya Mheshimiwa Freeman Mboge na Mheshimiwa Esther Matiko, kabla ya hizo kesi kuamuliwa nilifuatwa na watu wa nje wengi sana wakati huo nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria wakinisihi niiambie mahakama hizo kesi zifutwe, jibu langu lilikuwa *we are not a banana republic allow the court to do their job.* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma leo hukumu hizo mbili zimeweka misingi mizuri sana tisa ya jinsi gani mahakama zishughulikie suala *bail* (suala la dhamana). Ningeshawishika ili kuwafurahisha na labda wanisifie na wanipambe hao watu wa nje ningeimbia mahakama bwana hii kesi iachen, tungekuwa tumekosa *judgement* nzuri kabisa ya Jaji Rumanyika ambaye ameweza sasa misingi mizuri tisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nina imani hukumu hiyo sasa itakuwa ni *precedent* ingawa sio *binding* katika nchi nyingine za Commonwealth. Kwa hiyo mahakama zetu zinafanya kazi kubwa sana na ndani ya ile hukumu kuna mstari watu wengi hawausemi. Sasa hivi hawa Wabunge wawili hawawezi kusafiri nje ya nchi bila *permission of the court* kwa sababu *wali-jump bail*, lakini kikubwa kwenye *judgement* hiyo ni ile misingi tisa ambao sasa mahakimu wote ni lazima waizingatie wanapotaka kumnyima mtu dhamana na ni misingi imewekwa vizuri na itawasaidia sana walio chini yake na sana itakuwa *binding to all subordinate courts*.

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi baada ya hukumu hiyo Mheshimiwa Naibu Spika niliwaita baadhi ya hao waliokuja kunisii nifanya hivyo, nikawambia hii misingi tungeipata wapi? Kwa sababu kuna tabia ya hawa wenzetu wa nchi za Magharibi na nchi za Magharibi hazina *moral authority* za kutufundisha haki za binadamu. Naawaambia na uzuri nimekaa nao miaka tisa, nimesoma nao wajinga pia kule wengi na nimefaulu nikawashinda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi nchi hizi za Afrika *we have never enslaved anybody, we have never colonized anybody, we have never plundered property of anyone, wao wametu-enslave, wametu- colonize na wame-plunder our resources, hawawezi kuwa na moral authority*. Nchi za Magharibi sisi hatujawahi kusababisha vita yoyote, wao wamesababisha vita kuu mbili, na vita zote kuu mbili zimekuwa na madhara kwa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Vita ya Kwanza ya Dunia ilipokwisha makoloni yote ya Wajerumanî yaliwekwa chini ya

league of nations yaligawanywa, Tanganyika huku, Rwanda na Urundi kule. Na nchi hii kwa miaka mitatu ilikuwa na haina jina, haina mwenyewe, Cameroon ikagawanywa, Togo ikagawanya, waliacha ... West Africa ambayo leo ni Nambia. Na matokeo yake we became the cinderella of West Africa, the British did nothing, the British did nothing for this country. The biggest university we have tumeijenga wenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waingereza hawajatuachia *University they did nothing*. Hata reli ile ile alioa cha Mjerumani na sasa tunajenga nyingine. Vita Kuu ya Pili ya Dunia wamechinjana Warusi peke yao walikufa milioni 20. Sisi hatukumkamata shoga kumtia kwenye *gas chamber* kama walivyofanya Wajerumani, sisi hatukumkamata chotara tukamtia kwenye *gas chamber*, sisi hatukumkamata Myahudi na kumtia kwenye *gas chamber*, sisi hatukukamata mashoga na kuwatia kwenye *gas chamber*. Wao wamefanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, so they have no moral authority of telling us anything, tutaendelea kuheshimu haki za binadamu kwa sababu ni muhimu kuziheshimu, tutaendelea kuheshimu Katiba yetu kwa sababu ni muhimu kuiheshimu. Lakini sio kwa sababu kuna mtu anayetuambia tuiheshimu na tuchukue jitihada zote kulinda haki za binadamu kwa sababu binadamu wote ni sawa, huo ndio msingi wa Katiba ya TANU, huyo ndio msingi wa Katiba ya CCM na huo ndio msingi wa Katiba yetu. Binadamu wote ni sawa na wanastahili heshima. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wao hawakutuheshimu na wao hawakutuchukulia kuwa sawa. Nchi hii imewahi kuingizwa katika ushauri wa ajabu kina Mzee Mkuchika wapo hapa mwaka 1958 tulilazimshwa kufanya uchaguzi na ninasema hivi kwa sababu wanafunzi wapo waelewe. Tukaambiwa ili mjiandae kupata uhuru lazima tuwafundishe kupiga kura, tukaambiwa kila jimbo la uchaguzi tuchangue Wabunge watatu Mzungu, Mhindi na Mwfrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachama wengi wa TANU walikataa ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu wa TANU wa wakati huo Zuberi Mtemvu ambaye alijitoa akaunda chama chake cha *African National Congress*. Tulivuka huo mtihani, tumevuka mitihani mingi na huu mtihani tutauvuka tena kwa ushindii mkubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1985 benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa lilitupigisha magoti kwa sababu tulikuwa hatuna uwezo wa kiuchumi. Sasa tunajenga *Stiegler's Gorge* itatupa umeme tunajenga *Standard Gauge Railway* tutasafirisha mizigo. Baada ya hapo huduma zetu za kijamii katika elimu, afya na maji haitategemea tena fedha kutoka nje. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tuwe ndio kizazi cha mwisho cha kutegemea misaada, wajukuu zetu na vitukuu vyetu wasiishi fedheha hii tena. Fedheha hii iishe na sisi, tunavuna haya kwa sababu bado hatujafikia mahali pa kujitegemea na mimi nashukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuchukua hii miradi ya kimkakati ambayo baadaye italicifanya Taifa hili lijitegemee liwe lenye nguvu, na mimi nimefarijika sana na ningependa kuwaambia Watanzania wote Mheshimiwa Rais leo amemaliza ziara ya Zimbabwe, tumekuwa Afrika ya Kusini siku nne, tumekuwa Namibia siku mbili. Zimbabwe ilikuwa tukae siku mbili lakini wakamuomba aongeze siku ya tatu. Ndugu zangu wanamuona ni Mwafrika mahiri, shupavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaambia Watanzania wote wenye umri wangu tumshukuru Magufuli kwa kufanya mambo haya makubwa ambayo Baba wa Taifa aliyajenga, Mzee Mwinyi akaichukua nchi hii kipindi kigumu, tumepepigishwa magoti tumekataa na waliofuata wamejenga msingi. Mkapa, Kikwete na sasa Magufuli na Magufuli ndio atakuwa Rais wa mwisho kwa maoni yangu aliyemuona Nyerere akiwa mtu mzima. Na ni vizuri Mungu atambariki kwa kukamilisha miradi yote ya Mwalimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie tulipifika Pretoria moja ya sababu kubwa ya kushangiliwa kwanza kuwaona Rais aliyestaa fu na Rais aliyemwachia wapo pamoja na wameshuka pamoja *is very rare*, lilikuwa ni jambo la fahari. Nchi nyine Rais Mstaafu na Rais aliye madarakani hata kusalimia hawasalimiani. Jambo kubwa, kwa hiyo Mheshimiwa nilikuwa kwenye uwanja nimeona aliyeshangiliwa zaidi kuliko wote ni Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumekwenda Nambia, tumekwenda Zimbabwe na kote watu wametupokea vizuri, na safari imekuwa ya mafanikio makubwa na manufaa makubwa kwa nchi yetu. Leo hawatanikasirisha leo sikasiriki ng'oo, ndio leo sikasiriki ng'oo, mtazoza mpaka mtachoka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maswali tuliyoyapata kwa maandishi na ambayo tumeyajibu na mengi yanafafan na yale ambayo yamekwishatolewa, kuna swali kutoka Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe, Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Rhoda Edward Kunchela, Mheshimiwa Christopher Chiza, Mheshimiwa Janet Mbene, Mheshimiwa Mwanne Mcchemba, Mheshimiwa Sonia Juma Magogo, Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Juma Othman Hija, Mheshimiwa Zainab Mndolwa Amir na Mheshimiwa Janeth Moris Masaburi.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango yote hii tumeipokea na tumeipa majibu na tutasambaza majibu yote ya maswali hayo ya maandishi tuliyoletewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa tena nichukue fursa hii kukushukuru sana Naibu Spika, kuwashukuru Wabunge wote kwa michango mikubwa waliyooita kwa Wizira yetu na imani yangu *Inshallah* katika mwaka huu wa fedha ambao tutauanza baada ya Bunge la hili la Bajeti kukamilika tutaendelea kutekeleza vipaumbele vyote vilivyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, hatutakaa kimya nchi yetu inapobezwa, hatukaa kimya nchi yetu inapotukanwa, hatutakaa kimya nchi yetu inapochokozwa. Tutajibu tutafafanua tutaeleza tulifanikiwa Geneva tutafanikwa New York na tutafanikiwa mahali popote, huu sio wakati wa kukaa kimya, huu sio wakati wa kupuuza, kila linalotolewa lijibewe tena lijibewe kwa stahili kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza, mimi sipendi sana kujieleza mimi ni nani, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri amesema na Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Ummy Mwalimu ni wanafunzi wangu wa *jurisprudence* mara baada ya kuwa nimerejea toka masomoni nje, nimewafundisha *jurisprudence*, lakini mara nyngi katika nchi hii sio mara ya kwanza kuombwa na nchi yangu kufanya kazi ngumu. Mheshimiwa January Makamba yupo hapa, Sheria ya Mazingira hiyo anayoitumia aliyelisimamia, allyeitunga na kuhakikisha inakuja Bungeni wakati Mheshimiwa Chenge kaka yangu akiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi na ninaomba niwasomee *Hansard* na nimsome wakati huo Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Arcado Ntagazwa anasema nini kuhusu Palamagamba Kabudi ndani ya Bunge hili mwaka 2004. (*Makof*)

Anasema; "Nimalize sehemu hii ndogo kwa kumshukuru na kumpongeza, ataniwia radhi kama nitatamka jina lake yabidi nifanye hivyo, Dkt. Palamagamba Kabudi, Mhadhiri wa Sheria katika Kitivo cha Sheria, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Dkt. Palamagamba Kabudi ndio Mshauri Mwelekezi (*Consultant*) kwa lugha ya Kiingereza wa Mradi wa Kubainisha Mfumo wa Kitaasisi na Kisheria katika jitihada za Taifa letu kuhifadhi na kusimamia mazingira, kujihakikishia maendeleo endelevu. Tunawashukuru Benki ya Dunia, waliohisani mradi huo na kupitia kwa Dkt. Palamagamba Kabudi Tanzania tuna mahali pa kujidai, kwani kwa yakini kuwa nchi yetu tunao wataalam wazalendo wanaokidhi sifa zitakiwazo Kimataifa. Maana Dkt. Palamagamba Kabudi sio peke yake, wako zaidi kama huyu." Hiyo ilikuwa tarehe 10 Novemba, 2004. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Sheria ya Kupambana na Rushwa inatungwa mwaka 2004, wakati upinzani chini ya Dkt. Wilbrod Slaa na Hamad Rashid na CCM wameshindwa kuelewana, mimi ndio niliyeitwa ku-*facilitate* maelewano hayo. Sasa naomba nimnukuu Dkt. Wilbrod Slaa, Kiongozi wa Upinzani wakati huo Bungeni, ambaye aliongea baada ya Halima Mdee kumaliza kuongea; anasema hivi: "Kwa bahati mbaya, Waziri ame-*quote* mifano ya mtu mmoja mmoja walioleta hisia zao, lakini taarifa ya mwisho iliyokuwa summed up na Profesa Kabudi ambaye alikuwa *rapporteur* wetu ambaye mimi ndiye nikaja kuwakilisha, haikusema hivyo." Mwaka 2007 brokered, compromise between the opposition and CCM, tena na Dkt. Slaa na Hamad Rashid. (Makofi)

Kwa hiyo, mtu yeoyote ambaye ana wasiwasi au anaishi kwa hofu ya Kabudi, aendeleee kuishi na hofu hiyo. Yeyote anayeishi na hofu ya Kabudi aendeleee kuishi na hofu hiyo. Kabudi hatatetereka, Kabudi hataacha kufanya kazi. Kwa hiyo hatatetereka, ishini na hofu ya Kabudi, Kabudi anaishi kwa neema ya Mungu. (Makofi/Kicheko/Vigelegele)

Mheshimiwa Naibu Spika, msisahau ndani ya Bunge hili, mimi kwenye timu hii nimeingia wakati wa dirisha dogo. Nimesajiliwa kwenye dirisha dogo, hilo mlifahamu. Kwa hiyo, endeleeni kuishi na hofu ya Kabudi, endeleeni kuishi na husuda ya Kabudi, endeleeni kuishi na wivu wa Kabudi, lakini yeeye atafanya kazi bila uoga wala bila kutetereka, kwa sababu nchi yangu ni muhimu kuliko mimi mwenyewe. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Mama yako!

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, nchi hii ni kubwa kuliko sisi wote, kwa hiyo, nitaitumikia nchi hii bila uoga, bila wasiwasi, bila chuki kwa sababu ni wajibu niliyoitiwa na mwezi huu ni Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, nawaomba wote muisome *Surat Yussuf* mtaelewa. (Makofi)

MBUNGE FULANI: Ipo.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wakristo mkasome kitabu cha Mwanzo Sura ya 42 mpaka 48 kisa cha Yusufu na nduguze, mtajua. Huyu ndio Yusufu, msimpeleke utumwani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Profesa Kabudi. (*Makofii*)

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wako.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wako.

NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 34 - Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Kif. 1001 – *Admin. and Human Resources Management*.....Sh. 11,117,507,447/=

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kama ulivyo utaratibu wetu, fungu hili ndilo lenye mshahara wa Waziri. Kwa hiyo, yako majina hapa yaliyoletwa na Vyama vyenye Wawakilishi Bungeni, tutaanza na Mheshimiwa Cosato David Chumi. (*Makofii*)

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi. Naiomba Serikali pamoja na maelezo yaliyoko katika hotuba ya Waziri, jambo ninalotaka kulizungumza limekuwa likizungumzwa sasa mwaka wa tatu. Mimi binafsi na Wabunge tumekuwa tukiishauri Serikali ione umuhimu wa kufungua Ubalozi mdogo katika Mji wa Lubumbashi na Mji wa Guangzhou China ili kuendana na diplomasia ya uchumi.

Kwa ufupi nitaelezea kwa nini tuna umuhimu wa kufungua Ubalozi mdogo katika Mji wa Lubumbashi? Kwa sababu sisi kama Taifa tunafanya sana biashara na Congo Mashariki na kutoka Lubumbashi mpaka ulipo Ubalozi Kinshasa, ni umbali zaidi kilometra 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa eneo hili kwa mfano, kwa mujibu ya *study* ya *World Bank on Cross Border Business* mwaka 2017 tu, mchele ulioingia Kalemie kutoka Tanzania thamani yake ilifikia dola milioni 1.5. Kwa hiyo, hili ni eneo ambalo lina fursa kubwa kiuchumi kama ambavyo tuna fursa kubwa kiuchumi kati ya Guangzhou na Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda Mheshimiwa Waziri pamoja na kueleza kwenye hotuba yake kwamba wako katika utaratibu jambo ambalo limekuwa kila mwaka linaleezwa hivyo, atueleze na alieleze Bunge hili, ni lini anadhani kwamba watafungua Ofisi za Balozi ndogo katika Miji *Guangzhou* na Lubumbashi? (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza tumshukuru Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge wa Mafinga kwa hoja yake hiyo nzuri ambayo amekuwa akiisimamia kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Chumi ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na jambo hili amekuwa akiliuliza sana hata toka kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imedhamiria kikweli kweli kuhakikisha kwamba tunatekeleza diplomasia ya uchumi kwa vitendo. Ni mpango wa Serikali kupitia Wizara hii, pale ambapo kuna manufaa ya kiuchumi, kama ambavyo ilivyo kwa Mji wa Lubumbashi na Mji wa Guangzhou, ni lazima tufungue Balozi ndogo au *consul* ili kuhakikisha kwamba siyo tu tunatoa huduma za Ki-*consul*/kwa wananchi mbalimbali lakini pia tunatumia uwepo wa *consul* hizo kuhakikisha tunakamata fursa za kiuchumi, hasa hivi sasa ambapo Shirika letu la Ndege la *Air Tanzania* limefufuka na tunahitaji kuwa na safari za Ndege kwenda Guangzhou na Lubumbashi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umbali wa kutoka Kinshasa mpaka Lubumbashi ni mkubwa mno na sehemu ya Mashariki ya Congo inategemea sana Lubumbashi na Lubumbashi inategemea sana upande wa Tanzania hasa mpaka Dar es Salaam. Hivyo naomba nimhakikishie Mheshimiwa Chumi katika mwaka huu wa fedha tumedhamiria, baada ya kufanikiwa kufungua Ubalozi wa Cuba ndani ya mwaka huu wa fedha na baada ya kufanikiwa kufungua Balozi saba ndani ya Awamu hii ya Tano ya Mheshimiwa Magufuli, sasa tunaelekea kukamilisha *consul* hizi mbili za Lubumbashi pamoja na Guangzhou.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, namwomba Mheshimiwa Chumi kama ambavyo amekuwa akituamini na anaendelea kutuamini, atuamini katika hili, tutasimama kwenye ahadi yetu, tutatekeleza na tutafungua hizi *consul* mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Cosato David Chumi.

MHE. COSATO D. CHUMI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba katika Awamu ya Tano walipoingia wameshafungua Balozi saba na kwa maelezo hayo, na mimi nikiwa Mjumbe wa Kamati,

ninaamini kwamba jambo hili linaenda kutekelezwa. Kwa hiyo, sina mpango wowote wa kushika shilingi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wafanyakazi kwenye Balozi zetu waweze kufanya kazi vizuri, lazima mazingira ya ofisi zetu yawe ni mazuri. Kuna umuhimu mkubwa sana wa sisi kama Taifa kuwa na majengo ya kwetu kwenye nchi ambazo tuna Balozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya sababu na faida, moja ni heshima kwa nchi yetu, lakini pia inatusaidia kupunguza gharama kwenye Ofisi za Ubalozi; tatu, inaweza kutumika kama chanzo pia cha mapato. Kwa mfano, Msumbiji, Tanzania tuna jengo la ghorofa karibu tisa na ninaambiwa Ubalozi wetu Msumbiji unatumia kama siyo ghorofa moja basi ni mbili na maeneo mengine ya jengo lile tunapangisha kwa ajili ya kupata fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa na Mheshimiwa Waziri kwenye kitabu kwa kifupi sana kwamba wana mpango wa kujenga majengo ya Ofisi za Ubalozi, lakini hata Kamati imeshauri kwenye kitabu chao hili jambo lifanyike. Nilipokuwa naangalia kitabu cha Mheshimiwa Waziri, lakini pia wakati anahitimisha hakupata nafasi ya kusema vizuri, sijauona mkakati madhubuti wa Wizara kuhakikisha kwamba wanaendelea kujenga majengo kwenye maeneo ya Ubalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Muscat, ninachofahamu tulipewa mpaka eneo, lakini mpaka leo hatujajenga. Kwenye Bajeti ya miaka miwili mfululizo iliyopita, tulitenga fedha lakini fedha hazikutoka na majengo yale mpaka sasa hivi hayajajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo madhubuti ya Serikali, tuna mkakati gani na mpango gani wa kujenga majengo ya Ubalozi kwenye nchi ambazo tuna wawakilishi ikiwemo Muscat? (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sitapata maelezo mazuri, nakusudia kutoa shilingi. (*Makof!*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, ufanuzi.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijiini kwa swali lake hilo zuri na kwa hoja yake hiyo ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tumesema kwenye kitabu Serikali imejitahidi sana kujenga mahusiano ya Kimataifa na Diplomasia kwa kuwa na Balozi nyingi. Hivi sasa tuna Balozi 42, lakini tuna Balozi ndogo tatu na huko kote kuna majengo pamoja na viwanja. Kwa upande wa majengo tunamiliki majengo 97. Kwa hiyo, inaonesha ni kwa kiasi gani Serikali kupitia Wizara hii imeweza kuwekeza kwenye suala la majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile viwanja ambavyo viko wazi, tuna mkakati wa makusudi kabisa kuhakikisha tunavijenga. Tumeshauriwa na Kamati inayoratibu Wizara hii, tuangalie uwezekano wa kutumia *mortgage financing*. Tumelipokea ombi hilo, tunalifanyia kazi ili kuona kwamba tutikumia mfumo huo kama unaweza kukubalika kiserikali, lakini pili ukishakubalika tuweze kuhakikisha kwamba viwanja ambavyo viko wazi vinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba njielekeze mahsus katika suala la Oman. Oman tuna kiwanja ambacho tumepewa na Serikali ya Oman. Kiwanja hiki kipo katika mkakati wa kujengwa. Tuliweka kwenye bajeti ya mwaka huu 2018/2019 na katika bajeti hiyo tuliweka shilingi za Kitanzania bilioni 6.1 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Oman.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi ni mchakato, tayari kwa kushirikiana na wadau mbalimbali Serikalini, tumeshaanza mchakato wa zabuni. Tumeshampata Mshauri Kiongozi (*Lead Consultant*) ambaye ni *Tanzania Building Agency*. Hivi sasa Mshauri Kiongozi huyu anapaswa kushughulikia masuala ya michoro na kupata vibali nya ujenzi. Pia tumeshaomba fedha kutoka Wizara ya fedha ili Mshauri Kiongozi huyu aweze kukamilisha hiyo hatua ya awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni wazi kabisa Mheshimiwa Mnzava, hatua zimeshaanza kuchukuliwa na tunatumaini kabisa katika mwaka huu wa fedha, shughuli hiyo awali itakuwa imeanza na katika mwaka ujao unaofuata wa fedha tutakuwa tumekamilisha zoezi hili ili Ubalozi wetu katika nchi ya Oman, nchi ambayo ina uchumi mzuri na mahusiano mazuri na Tanzania uweze kufanya kazi yake na uweze kusaldia katika diplomasia ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Timotheo Mnzava.

MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo na ahadi ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba wanaendelea na mchakato huo na ametuhakikishia kwamba kwenye mwaka huu wa fedha, fedha iliyokuwa imetengwa itatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo, basi namrudishia shilingi Mheshimiwa Waziri. Nashukuru sana kwa hayo maelezo, naomba waifanye hiyo kazi kwa sababu mwaka wa fedha wenyewe uko mwishoni. Ahsante sana.
(*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nitakwenda kwenye suala la *diaspora* na uraia pacha. Mheshimiwa Naibu Rais hapa, amewataka

Watanzania wa *diaspora* waende wakajisajili katika Balozi zetu nje ya nchi.

Sasa suala siyo kwenda kujitambulisha kwenye Ubalozi, kwa sababu mtu ambaye ana shughuli zake, anatokaje Texas, Marekani kwenda DC kwenye Ubalozi kwenda tu kuji-*register*? Hayo ni mambo ya kizamani kabisa hayo, enzi za ujima ambako Mheshimiwa Naibu anataka kutupeleka. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya... *sorry*.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: ...Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje anataka kutupeleka. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani, Kanuni iliyovunjwa.

MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni iliyovunjwa ya 64(1)(f) na (g). Mchangiaji anayechangia sasa hivi ameongea lugha ambayo haitakiwi kuongea hapa Bungeni. Amemwita Waziri, Naibu Rais. Sidhani kama kuna cheo cha Naibu Rais. Sasa nilikuwa nataka arekebishe hiyo kauli yake aliyoisema hapo.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, nadhani mmemsikia hapo mwisho amerekebisha. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi. (*Makofî*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Unajua hili jina linatumika sana na Wabunge wa CCM wanasema kwamba Kabudi anajifanya ye ye ni Naibu Rais kwa jinsi anavyoendesha mambo. Sasa ndiyo likawa limeniingia kidogo, kwa hiyo, nimeteleza mnisamehe sana. (*Makofî/Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, hilo jambo halipo. Kwa hiyo, liko lile ulilorekebisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi malizia hoja yako. (*Makofî/Kicheko*)

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa miaka mingi sana tumekuwa tunaitaka Serikali iruhusu uraia pacha (*dual citizenship*), lakini hamtaki. Sasa tunawauliza, *sisi enemies*, sisi maadui tunawauliza ninyi mnaoitakia mema nchi hii, mna tatizo gani? Mnawaogopea nini ndugu zetu hawa wa *diaspora*? Au mnaogopa *exposure* waliyokuwa nayo? Au hamjui umuhimu wa mchango wao katika Taifa letu? Eeh! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtaka Mheshimiwa Waziri, vinginevyo nitakamata mshahara, atuambie ni lini Serikali italeta sheria Bungeni ili tuwe na uraia pacha, wenzetu waweze kushirikia masuala ya Taifa, ikiwemo masuala ya uchumi, siasa na kijamii? Kwa sababu Watanzania wenzetu hawa wa nje wanapata taabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimekutana na Mtanzania hapo nje ameoa M-finn, anahangaika mwaka wa pili sasa kushughulikia kibali cha mke wake, *complications* zote hizi zinatokana na kutokuwa na *dual citizenship*. Tungekuwa na *dual citizenship* yule mtu asingelalamika. Sasa yule Mtanzania katika Finland kamuona Waziri, huu mwaka wa pili, mke wake na ye ye wame-*invest* zaidi ya dola 100,000 katika nchi hii kwenye masuala ya *sports*, lakini ananyimwa kitu ambacho kimsingi kipo kisheria. Mwaka 2016 ilipitishwa sheria hapa inaitwa *permit exemption*, yule mtu anaifukuzia hiyo miaka miwili hajapata. Sasa haya yote yanatokana na tatizo tulilokuwa nalo kwamba kwa nini hatuna sheria inayoruhusu *dual citizenship*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa naishia hapa lakini usiponipa maelezo mazru kuhusiana na hili nitakamata shilingi na nitakwenda mpaka mwisho na sitachoka. Kwa miaka tisa tumekuwa tunafuatilia hili na katika hili naomba Mheshimiwa Waziri alijibu kama mwanadiplomasia, kwa sababu Waziri wa Mambo ya Nje... (*Makofii*)

MWENYEKITI: Haya, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi subiri upate ufanuzi, kengele imegonga halafu utapewa fursa. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRICA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ambaye mimi ndiyo *best man* wake... (*Kicheko/Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRICA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivosema nimeomba kuwa *best man* wake, naamini atanikubalia kama ambavyo atanikubalia hoja hizi ambazo napenda kuzitoa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbilinyi ameongelea mambo mawili, moja suala la *diaspora* na pili suala la uraia pacha. Hivi ni vitu viwili tofauti ingawaje huwa vinakwenda kwa pamoja. *Diaspora* ni Watanzania ambao bado wana utanzania wao kwa maana ya uraia lakini kutokana na sababu mbalimbali wamejikuta wako katika nchi nyininge kwa sababu hizo mbalimbali. Sisi Tanzania tunawatambua *diaspora* hao, sasa hivi kama Wizara tumeanza kwa kuunda Idara ya *Diaspora* ndani ya Wizara. Idara ambayo inaongozwa na Mkurugenzi ambaye ni Mheshimiwa Balozi. Lengo letu kwa kutumia Idara hii tuweze kutambua na kusajili *diaspora* wote duniani. Tumeanza na kwa hao wachache ambao tumeanza mafanikio yameonekana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 61 wa kitabu chetu cha hotuba ya Wizara, tumeeleza baadhi ya mafanikio hayo ambayo kwa kuanzisha idara hii na juhudhi za kuwatambua *diaspora* zimeshaanza kuzaa matunda. Tumeona, jumla ya shilingi bilioni 2.5 zimekuja kwa kipengele kimoja tu kununua nyumba za *National Housing*, lakini kupita benki zetu hawa *diaspora* pia wameweza kusaidia kwa kiasi kikubwa. Mfumo huu ambao tumeuchukua sisi ni mfumo ambao unatumwiwa na Ethiopia, unatumwiwa na India. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni suala la uraia pacha. Ili mtu aweze kuwekeza hapa Tanzania siyo lazima awe raia, mgeni yejote ambaye siyo Mtanzania hana mpango wa kuwa Mtanzania anaweza akawekeza. Kwenda kuchukua uraia ni hatua nyingine, tunataka sasa huyu mtu ashughulike katika masuala ya kisiasa na masuala mengine, lakini kwa maana ya uwekezaji tu, mtu yejote anaweza akawekeza. Mfano mzuri ni Ethiopia, katika Afrika nchi inayoongoza, moja kati ya nchi ambayo inaongoza kwa *diaspora* wengi ni Ethiopia. Ethiopia pamoja na kwamba ina *diaspora* wengi sana na wanachangia sana katika uchumi na wanashiriki sana, lakini hawana uraia pacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingine duaniani ambayo ina *diaspora* wengi na wanachangia vizuri ni India. India ina *diaspora* wengi sana lakini hawana uraia pacha. Kwa hiyo na sisi Tanzania katika mfumo ambao tunao hivi sasa ni kwamba tutaeendelea kuwashirikisha, kuwasaidia na kuwapa fursa *diaspora* wetu.

Suala la uraia pacha siyo suala la kutolea maamuzi ya haraka haraka, ni suala ambalo tunatakiwa tukae chini tulifanyie utafiti, tujadiliane pande zote ikiwemo upande wa upinzani, ikiwemo na Watanzania walioko hapa, tutakapofikia hatua nzuri ya kufanya maamuzi hayo, tutayafanya maamuzi kupiditia chombo hiki kinachowakilisha wananchi na hatimaye maamuzi hayo ndiyo yatakuwa maamuzi ya mwisho. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo hayo na kwa kuwa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ni mtu msikivu na ameelewa na yeye anajua zaidi kuhusiana na *diaspora* tunaamini ametuelewa. Naamini atatuachia shilingi ili tuweze kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwemo kuwashudumia *diaspora*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri analipotosha Bunge na Taifa kwamba eti India hawana uraia pacha. India Mheshimiwa Waziri labda ni mgeni kwenye masuala ya *International Relations*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, India wana kitu kinaitwa *special status*, Mhindi ye yeyote duniani, popote alipo duniani akirudi India ana haki kama mzaliwa kwa maana ya kuwekeza na kadhalika kasoro vitu vichache tu ikiwemo labda kugombea masuala ya uongozi kwenye siasa na kadhalika.

MWENYEKITI: Sasa twende vizuri Mheshimiwa Joseph Mbilinyi ili kama unashika shilingi utoe hoja uungwe mkono, watu wajadili, halafu mwishoni utapewa fursa ya kufunga hoja yako. Kwa hiyo sasa hivi ni aidha unaachia kwa maana ya kwamba umeelewa maelezo au unatoa hoja ili watu wakuunge mkono.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipewa maelezo na nataka nimwambie Waziri mdogo kwamba kwa nini sikubaliani na maelezo yake kwa hiyo naomba nitoe hoja, niungwe mkono ili Bunge hili kwa niaba ya ndugu zetu labda kama huna ndugu nje ya nchi, mpo ambaio hamna ndugu, sasa waweze na...

MWENYEKITI: Haya, hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge, wengine wote make, wabaki wamesimama wanaotaka kuchangia hoja hii. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, Mheshimiwa Khatib, Mheshimiwa Edward Ngonyani, Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Suzan Kolimba na Mheshimiwa Kangi Lugola.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Kangi Mambo ya Nje na Mambo ya Ndani ni vitu viwilli tofauti, lazima ujue.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Khatib.

MHE. KHATIB SAID HAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mbilinyi kwamba umefika muda sasa wa Watanzania kupata haki ya kuwa na uraia pacha. Hili suala la uraia pacha kukataliwa ndani ya nchi yetu, nalifananisha na lile tendo la joka la mdimu, joka la mdimu hulinda matunda ambayo yeye hawezikula. Kwa sababu wakati wa utawala wa awamu iliyopita Mheshimiwa Kikwete aliwahi kufanya ziara nje ya nchi na kuzungumza na raia wa Tanzania wanaoishi nchi mbalimbali. Alitoa maelezo marefu kuonesha fursa walizonazo kuja kuwekeza ndani ya nchi yetu, ikiwemo kumiliki ardhi na kuweza kumiliki majumba. Aliwapa changamoto hiyo kubwa na aliwapa fursa kubwa ya kuwaambia njooni mjenge ndani ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walioko nje wengi sana wamefanikiwa kiuchumi na wanataka kuwekeza sana ndani ya nchi yetu, lakini awamu hii tumemsikia Waziri wa Ardhi akiwaambia hataruhusiwa Mtanzania ambaye hana uraia wa Tanzania kuweza kumiliki hata kipande cha robo mita cha ardhi ya Tanzania. Kwa hiyo Mheshimiwa jambo hili linakuwa linawapa mashaka watanzani waliko nje kuja kuwekeza mitaji yao kwa sababu bado pana vikwazo vingi. Hata hivyo, tujilize, nchi ambazo wamekuwa wakifuata jambo hili la uraia pacha ni athari gani walizopata nchi hizo kiasi ambacho unaweza kusema Tanzania tufuate kigezo hicho kwamba kuna athari za raia wa nchi moja kuwa raia wa nchi mbili. Hakuna nchi yoyote duniani ambao wamefuata mfumo wa uraia wa nchi mbili ambao uko ushahidi wowote ambao umeonesha kama kumetokea athari na badala yake zimepatikana faida nydingi sana za kiuchumi. Kwa hiyo naiomba Serikali, nawaomba wenzangu Wabunge wenzangu, tuache roho ya kwa nini. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naungana kabisa na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi juu ya kuwa na uraia pacha. Tulikuwa katika

nchi ya Kijamaa na mpaka sasa hatujitambui tuko katika maeneo gani. Tukumbuke sana kama Taifa tumejiunga katika jumuiya mbalimbali ikiwepo Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kama alivyotoka kuzungumza msemaji aliyejipa, ni kitu gani kibaya ambacho watoto wetu, kaka zetu, ndugu zetu walioko nje ya nchi hawawezi kurudi nyumbani na kuwekeza. Wakati huo huo wamefungua milango kwa wawekezaji wengine waje wakati watu wetu wanawazuia. Nafikiri uchumi walionao kule wakija wakawekeza hapa nyumbani ni kwa faida yetu sisi wenyewe. Tumesikia habari nyingine watu wanazungumza, unapokuwa umeolewa au umeoa ukiwa nje ya nchi unaporudi nyumbani kuna milolongo mirefu sana inaweza kukusaidia wewe uweze kurudi katika Taifa lako. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunganana na Mheshimiwa Mbilinyi, turuhusu watu wetu waweze kupata hilo nafasi ya kuweza kulitumikia Taifa lao na kusimamia maslahi ya Taifa letu bila ya kuwa na vikwazo. Wana haki ya kupiga kura, wana haki ya kuchagua viongozi wanaowataka. Tunaomba na wao waje wafanye hivyo na wala hakuna kitu chochote kibaya kinaweza kuharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga hoja ya Mheshimiwa Mbilinyi mkono na naomba Watanzania wote na mkiwemo Wabunge wa CCM muunge mkono..(Makof)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa kengele ilishagonga, Mheshimiwa *Engineer Edwin Ngonyani*.

MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa. Ni mara chache mimi kusimama katika ngazi hii, lakini suala hili kidogo limenigusa na naomba ndugu zangu tusichanganye. Hapa inaonekana hatuongelei diaspora badala yake tunaongelea Watanzania walio ukana uraia wa Tanzania huko nje.

Wameukana uraia wa Tanzania, wamekuwa raia wa nchi nyingine ndiyo tunaoongelea hapa. *Diaspora* ni kitu kingine, *diaspora* ni Watanzania wanaoishi nje ya nchi na bado ni Watanzania na tumeambiwa mchango wao humu, umeandikwa vizuri tu. Tuombe tu utaratibu uendelee kusukwa, mchango huo wa Watanzania wanaoishi nje uongezeke uwe mkubwa zaidi. Wakirudi Tanzania wana haki zao zote, wao ni Watanzania, kama tunaongelea mtu aliyeukana uraia wa Tanzania, huyu ni msaliti. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Mattar.

MHE. MATTAR ALI SALUM: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, lakini kwanza niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Maelezo yake mazuri na nimwombe sana kaka yangu Mheshimiwa Mbilinyi arejeshe shilingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameshazungumza vizuri. Hawa raia amba wako nje ya Tanzania wana haki ya kuwekeza ndani ya nchi yetu kwa kile wanachokitaka. Utaratibu amba tumezungumza, hili suala siyo bayu, Mheshimiwa Waziri amesema utaratibu unaweza ukafanya ili hili suala likakaa vizuri, haya mambo yakaenda vizuri. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Mbunge aweze kumrejeshea shilingi Mheshimiwa Waziri ili aweze kuchapa kazi haya mambo yaende kwa *speed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dkt. Susan Kolimba.

MHE. DKT. SUSAN A.KOLIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili kuchangia kwenye hoja hii. Naomba sana kaka yangu Mheshimiwa Joseph Mbilinyi mwenye hoja hii ya uraia pacha, nadhani pia wakati anaruhusu kwamba Naibu Waziri awe anasimamia harusi yake, nadhani amepokea yale maelezo vizuri kabisa. Niseme tu kwamba siwezi kurudia yake ambayo Mheshimiwa Naibu ameyasema kwamba, Katiba yetu kwanza hairuhusu suala hili, kwanza ni la kisheria. Hata tukiangalia katika *process* ya *ku-discuss* suala hili la uraia pacha, hata lilipopita kwenye

Bunge la Katiba ambalo bado *process* yake inaendelea lilikuwa limejadiliwa na hata wale waliokuwa wajumbe katika Bunge lille hawakufikia muafaka wa kusema kwamba tunatoa uraia pacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika mapendekezo yao wakati ule kama hata ile Katiba pendekezwa ingejadiliwa na kutolewa na maoni kwenye nchi yetu, bado tulisema kwamba hawa wapewe hadhi maalum, watapewa upendeleo, watapewa uwezekano wa kuwekeza. Vilevile nirudi kwenye suala ambalo limechanganywa kwamba kuna wale ambao wameukana uraia na wanataka uraia pacha. Kuna wale ambao ni *diaspora*. Naomba nirudie tena kusema kwamba diaspora bado wana haki nchi hii inawapa, wanawekeza, na wamewekeza katika shule, wamewekeza katika hospitali, wamekeza katika hoteli. Ndiyo maana hata Wizara hii ya Mambo ya Nje imefanya mambo makubwa sana. Mwaka jana imefanya makongamano na hata kwenye taarifa yamewekwa na mengine yalioneshwu kabisa mubashara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba suala la uraia pacha bado kwa maslahi ya nchi hii, bado wakati siyo muafaka na tunasema kwamba tunataka tulinde uhuru, uhuru wa nchi yetu. Nadhani kabisa mdogo wangu Mheshimiwa Mbilinyi namuona roho yake kabisa anakubaliana na Mheshimiwa Waziri na namuomba sana kwa heshima kwamba arudishe shilingi ili watu hawa wakafanye kazi ya kuhakikisha kwamba tunapata maslahi makubwa na mapana kwa ajili ya... (*Makofii*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mapema kabisa nimwombe rafiki yangu Mheshimiwa Mbilinyi almaarufu Sugu kuiachia shilingi

ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu *issue* ya *diaspora*, *diaspora* na Mheshimiwa Mbilinyi hawana tofauti yoyote wote ni Watanzania. Wote ni Watanzania, wote wana sifa ya kupiga kura, wana sifa ya kuomba uongozi, tofauti yao ni moja tu, kwamba Mheshimiwa Mbilinyi anaishi pale Mwanjelwa Mbeya na *diaspora* pengine anaishi Muscat au Marekani hiyo ndiyo tofauti, kwa hiyo wanazo haki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *issue* ya uraia pacha ni *issue* ya kiusalama, ni *issue* ambayo haiwezi ikazungumzwa kwa *pressure* ambayo Mheshimiwa Sugu anaihitaji hapa. Hatuwezi kuwa na *pressure* ya *diaspora* ambao wamekwisha kuwa na mahusiano na wananchi ambao wako Mataifa mengine kuleta *pressure* za haraka haraka ili tuweze kuwapa uraia pacha watu wanaoishi nchi nyngine au hao *diaspora* kwa sababu tu kwamba wanataka kuwekeza. Uwekezaji katika nchi yetu uko wazi kwa raia yelete na raia wa nchi nyngine ambaye akiona kwamba mazingira ya Tanzania yanamfaa kuishi na Tanzania nchi yetu ni mahali paliponoga, mimi Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa niaba ya Mheshimiwa Rais, aombe uraia hata leo tutampa uraia wa Tanzania na atakuwa kama Mtanzania na ku-*enjoy* kama Mtanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Sugu asikimbie sana, kama mataifa mengine kwa sababu yameruhusu uraia pacha, na sisi turuhusu. Kama mataifa mengine yameruhusu, ushoga na sisi turuhusu; kama mataifa mengine yameruhusu kila aina ya kitu na sisi turuhusu, haitawezekana. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lukuvi.

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hii hasa kwa kuunganisha na maneno ya Mheshimiwa Khatib. Najua iko *clip* moja huwa inachezwachezwa hivi, nataka nimfahamishe kwamba *diaspora* wana haki zote kama walivyosema Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge. *Diaspora* anaweza akamiliki ardhi akapewa na hati miliki, *diaspora*

bado ni raia wa Tanzania. Mtu mgeni ambaye siyo raia wa Tanzania anaweza akawekeza kwenye ardhi kupitia utaratibu wetu wa sheria akapewa *deliberative right*. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema mtu ambaye ni mgeni maana yake mtu ambaye ameukana uraia wa Tanzania hata kama ana asili, huyo ni mgeni. Kwa hiyo atafuata sheria za uwekezaji wa nchi hii na hatakuwa na fursa ya kupewa hati miliki, kwa hiyo ndiyo tofauti. Ardhi ileile anaweza kupata kama mtu raia lakini hati tofauti. Huyu atapewa hati miliki *diaspora*, lakini huyu ambaye ameukana uraia atapewa *deliberative right* kupitia *TIC* kama mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimwambie Mheshimiwa Khatib na hao wengine ambaao nafikiri wanauliza uliza maswali, wawekezaji wa kabile lolote, wa nchi yoyote wanaruhusiwa hapa, hata kwenye ardhi. Isipokuwa *diaspora* wana haki zaidi kwa sababu wana haki za Kitanzania, wanaweza kupewa hati miliki ambayo ni haki yetu sisi Watanzania, lakini kwa wawekezaji, mtu ye yote mkaribishe, aje na awekeze, Tanzania ni salama. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, hatimisha hoja yako.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivysikiliza michango ya wengi hapa nimeona tuna tatizo la *exposure*. Mfano kama Mheshimiwa Kangi yaani nimeona kabisa hana *exposure* kabisa. Ndiyo maana nilimuonya nikamwambia hii siyo Wizara ya Mambo ya Ndani kutumia nguvu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilivyoanza kutoa hoja yangu nimesema itajikita kwenye *diaspora* na uraia pacha, ni sentensi moja, siyo vitu viwili. Hii ni kwa sababu huwezi kuhitaji uraia pacha kama hauko *diaspora*. Huwezi kutaka uraia pacha wakati uko Mwanjelwa kama Sugu kama anavyosema Mheshimiwa Kangi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme tena, tunahitaji uraia pacha na leo ni lazima tupige kura ili tujue nani wanawatachia mema hawa Watanzania wenzetu na nani hawawatakii mema. Tunapata hasara sana kama Taifa kwa kuwaacha hawa Watanzania ambao wana uraia wa nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unasema wameukana uraia, je, wameukana kwa hiari? Hawajaukana kwa hiari, wameukana kwa sababu ndiyo matakwa ya sheria ya Tanzania kwenye masuala ya uraia. Kwa hiyo, siyo kama wamependa bali wamelazimika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu katoka hapa kaenda kusoma, kasoma na kaelimishwa vizuri kapata *reward*, nchi za wenzetu kama Marekani na nchi zingine zina *policy* nzuri, wakiona mtu huyu ni *potential* wanampa mazingira ya kubaki. Sasa mtu kasoma vizuri Marekani anapata kazi pale mshahara Dola 15,000 unataka arudi huku umpe mshahara Sh.800,000 kwa sababu tu eti utamlazimisha awe na uraia wa Tanzania? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira kama hayo mtu analazimika sasa kuacha uraia wa Tanzania bila hiari yake ili achukue huo mwengine. Ndiyo maana wanatutumia sisi Wabunge kudai mpaka kesho. Sasa Mheshimiwa Waziri...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Kengele imeshagonga, hakuna kengele mbili kwenye hatua hii Mheshimiwa Sugu.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbilinyi, kengele imeshagonga. Tunaendelea na Mheshimiwa Ally Saleh Ally.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Nimeomba tupige kura.
(*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge, nimekuambia muda wako umekwisha umeendelea kuzungumza, kwa hiyo, hujapata muda wa kutoa hoja ili tuweze sasa kuamua.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Hilo umelitaka wewe mwenyewe kwa sababu ulitakiwa ufunge hoja yako na Bunge lihojiwe.
(*Makof*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nitazungumzia *economic diplomacy* lakini zaidi kwenye suala la *stand alone policy* ya *economic diplomacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijazungumza, nataka niseme vitu viwili. Cha kwanza, leo tarehe 30 ni siku ambayo mkataba wa *Continental Free Trade Area* ambao utazungusha zaidi ya Dola trilioni 2.5 na una soko la karibu watu bilioni 1.2 unaanza rasmi baada ya nchi 22 kutia saini mkataba huo bila ya Tanzania kuwemo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimefurahi kwa siku ya leo kwamba Mwenyezi Mungu ametushushia...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh, kwenye hatua hii jambo huwa ni moja tu huwezi kuwa nayo mawili, jambo moja mahsus.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema moja tu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh, wewe mwenyewe hapo unasema jambo la pili. Kwa hiyo, rudi kwenye jambo lako la kwanza ulilozungumza malizia muda wako ili hoja yako ikae vizuri. Usiongeze la pili kwa sababu mwenyewe ndiye uliyesema la pili na mimi nimesikia pili.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu inasimama kwenye kuwa na *stand-alone policy* ya *economic policy* mpaka hivi sasa hatuna. Nilikuwa nasema kabla sijasema hoja hiyo, leo ni siku nzuri maana tumempata Mtume Yussuf humu ndani na Mtume Yussuf huyo ametuia sisi maadui, ametuita sisi mabarakala, majina yote ya duniani ametuita wananchi wenzake ambao tunachangia kwa kheri ya nchi hii. Mtume Yussuf hakuwa hivyo, ye ye alikuwa mstahimilivu, msikivu na alikuwa anapenda kupata ushauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nimpe shauri Mtume Yussuf a.k.a Profesa Kabudi mwalimu wangu kwamba mpaka hivi sasa hatuna *written document* ya *economic policy* na kwa hivyo tunapambaja pambaja huku na huku. Tunachofanya bado hatujui tunataka nini na tutakipata wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, juzi nchi hii tumetembelea Namibia, tunamwambia Namibia aje awekeze hapa, nchi ambayo *per capita* yake ni Dola 400. Tuna Ubalozi Brazil, sijaona cha maana kilichotoka Brazil kuja hapa wakati ni moja katika nchi kubwa ambayo ina uchumi mzuri. Tunao Ubalozi Uturuki, hatuutumii, tatizo letu ni kwamba hatujatengeza *stand-alone economic policy*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh, kengele imegonga, ngoja upewe ufanuzi, utapewa fursa tena. Mheshimiwa Naibu Waziri.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana

kwa kupata fursa hii ili niweze kujibu hoja iliyowekwa mezani na Mheshimiwa Ally Saleh (Alberto), Mbunge wa Malindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ally Saleh ameleta hoja kwamba hatuna *stand-alone economic policy*. Kwa ufahamu wangu na Waziri wa Fedha na Mipango yuko hapa anaweza akasaidia, Tanzania tuna Sera ya Uchumi ambayo ndiyo inaongoza na ndiyo dira ya uchumi wetu. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na Sera ya Uchumi peke yake kwa ajili ya diplomasia ya uchumi. Diplomasia ya uchumi ni kipengele ndani ya Sera ya Mambo ya Nje ya Nchi lakini kwa maana ya uchumi kiujumla wake, hiyo sera tunayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Ally Saleh ameongelea *African Continent Free Trade Area* ambayo anasema leo ndiyo inaanza rasmi na nchi 22 zimeshasaini. Nimwambie tu Tanzania ilishiriki Kigali na ilisaini. Kitu ambacho hakijafanyika kwa upande wa Tanzania ni kuridhia. Sasa kuridhia ni mchakato, huwezi ukasaini tu ukata kuridhia bila kufanya uchambuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tunafanya uchambuzi wa kina tuone faida na hasara ziko wapi. Tukishajua hilo ndipo tulete hapa mezani kwa Waheshimiwa Wabunge tuwaeleze kwamba mkataba ni huu hapa, vifungu vyake ni hivi, faida ni hizi na hasara ni hizi ili hata mkituuliza maswali tuweze kuyajibu. Kwa hiyo, tuko kwenye mchakato tunafanya huo uchambuzi sasa hivi lakini kusaini tulishasaini. Sisi ni moja kati ya watu ambao tunesaini mkataba huo ila bado hatujaridhia kama nilivosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuambie kwamba Sera ya Uchumi tunayo lakini hatuoni kama kuna umuhimu wa kuwa na *stand alone economic policy* kwa ajili tu ya *economic diplomacy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ally Saleh.

MHE. ALLY SALEH ALLY: Mheshimiwa Mwenyekiti, bado nashikilia na sijaridhika na jawabu la Mheshimiwa Waziri na nitaomba kutoa shilingi kwa sababu kuwa na *stand alone* ndiyo ushauri wangu mimi kwa sababu tumeshaonesha vitu vingi vimetupita. Tumepitwa na suala la Bagamoyo, Mchuchuma, *Continental Free Trade Area*, ni lazima tufike wakati tuwe na *stand alone policy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa shilingi jambo hili lijadiliwe na Wabunge. Naomba kuungwa mkono. (*Makofii*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono isipokuwa sasa muda wetu umebakizile dakika zinazotaka tuingie kwenye kuitisha mafungu kwa pamoja. (*Makofii*)

Katibu, tuendelee.

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Kif. 1001 - *Administration and HR*

Management.....Sh.11,117,507,447/=

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh.728,964,099/=

Kif. 1003 – *Foreign Affairs Office Zanzibar*.....Sh.693,561,824/=

Kif. 1004 – *Policy and Planning*.....Sh.726,109,149/=

Kif. 1005 – *International Cooperation*.....Sh.875,665,935/=

Kif. 1006 – *Europe and America*Sh.428,368,664/=

Kif. 1007 – *Asia and Australia*.....Sh.451,080,691/=

Kif. 1008 - *Africa*.....Sh.1,481,348,698/=

Kif. 1009 – *Regional Cooperation*.....Sh.3,539,101,590/=

Kif. 1010 - *Protocol*.....Sh.8,416,210,934/=

Kif. 1011 – *Legal Service*.....Sh.1,899,939,512/=

Kif. 1012 – *Government Communication*

Unit.....Sh. 276,557,044/=

Kif. 1013 – *Middle East Division*.....Sh.419,345,501/=

Kif. 1014 – <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.276,621,955/=
Kif. 1015 – <i>Procurement Unit</i>	Sh.447,338,407/=
Kif. 1016 – <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh.322,451,726/=
Kif. 1017 – <i>Diaspora Engagement and Opportunity</i>	Sh. 298,657,781/=
Kif. 1018 – <i>Economic Infrastructure and Social Support Services Division</i>	Sh.477,742,722/=
Kif. 1019 – <i>Political, Defence and Security Affairs</i>	Sh.439,779,134/=
Kif. 1020 – <i>Trade, Investment and Productive Sector Division</i>	Sh.499,988,540/=
Kif. 2001 – <i>Embassy of Tanzania – Addis Ababa</i>	Sh.2,769,359,990/=
Kif. 2002 – <i>Embassy of Tanzania – Berlin</i>	Sh.4,108,829,347/=
Kif. 2003 – <i>Embassy of Tanzania – Cairo</i>	Sh.2,000,363,357/=
Kif. 2004 – <i>Embassy of Tanzania – Kinshasa</i>	Sh.3,996,154,449/=
Kif. 2005 – <i>High Commission of Tanzania – Abuja</i>	Sh.3,799,486,781/=
Kif. 2006 – <i>High Commission of Tanzania – London</i>	Sh.3,296,983,161/=
Kif. 2007 – <i>High Commission of Tanzania – Lusaka</i>	Sh.1,318,426,628/=
Kif. 2008 – <i>High Commission of Tanzania – Maputo</i>	Sh.1,737,694,491/=
Kif. 2009 – <i>Embassy of Tanzania – Moscow</i>	Sh.3,288,506,455/=
Kif. 2010 – <i>High Commission of Tanzania – New Delhi</i>	Sh.2,989,582,158/=
Kif. 2011 – <i>Permanent Mission to the UN – New York</i>	Sh.5,499,492,812/=
Kif. 2012 – <i>High Commission of Tanzania – Ottawa</i>	Sh.2,737,635,522/=
Kif. 2013 – <i>Embassy of Tanzania – Paris</i>	Sh.3,310,867,940/=
Kif. 2014 – <i>Embassy of Tanzania – Beijing</i>	Sh.5,655,822,474/=
Kif. 2015 – <i>Embassy of Tanzania – Rome</i>	Sh.4,079,352,343/=
Kif. 2016 – <i>Embassy of Tanzania – Stockholm</i>	Sh.3,573,812,673/=

Kif. 2017 – *Embassy of Tanzania – Tokyo*.....Sh.2,497,592,000/=
Kif. 2018 – *Embassy of Tanzania – Washington*.....Sh.4,093,459,121/=
Kif. 2019 – *Embassy of Tanzania – Brussels*....Sh.3,392,079,158/=
Kif. 2020 – *Permanent Mission to the UN – Geneva*.....Sh.5,919,665,792/=
Kif. 2021 – *High Commission of Tanzania – Kampala*.....Sh.2,318,420,691/=
Kif. 2022 – *High Commission of Tanzania – Harare*.....Sh.1,808,391,899/=
Kif. 2023 – *High Commission of Tanzania – Nairobi*.....Sh.4,905,014,530/=
Kif. 2024 – *Embassy of Tanzania – Riyadh*....Sh.2,775,153,726/=
Kif. 2025 – *High Commission of Tanzania – Pretoria*.....Sh.3,311,866,578/=
Kif. 2026 – *Embassy of Tanzania – Kigali*.....Sh.1,453,459,860/=
Kif. 2027 – *Embassy of Tanzania – Abu Dhabi*.....Sh.3,503,721,820/=
Kif. 2028 – *Embassy of Tanzania – Bujumbura*.....Sh.1,855,234,193/=
Kif. 2029 – *Embassy of Tanzania – Muscat*..Sh.2,366,812,439/=
Kif. 2030 – *High Commission of Tanzania – Lilongwe*.....Sh.1,369,250,757/=
Kif. 2031 – *Embassy of Tanzania – Brasilia*.....Sh.2,999,468,612/=
Kif. 2032 – *High Commission of Tanzania – Kuala Lumpur*.....Sh.2,135,862,313/=
Kif. 2033 – *Embassy of Tanzania – The Hague*.....Sh.2,883,737,000/=
Kif. 2034 – *Embassy of Tanzania – Moroni*....Sh.2,346,581,228/=
Kif. 2035 – *Embassy of Tanzania – Kuwait*....Sh.1,568,600,820/=
Kif. 2036 – *High Commission of Tanzania – Algiers*.....Sh.2,581,969,790/=
Kif. 2037 – *High Commission of Tanzania – Ankara*.....Sh.2,960,516,667/=
Kif. 2038 – *Embassy of Tanzania – Khartoum*.....Sh.2,089,795,224/=
Kif. 2039 – *Embassy of Tanzania – Seoul*.....Sh.5,263,905,657/=
Kif. 2040 – *Embassy of Tanzania- Tel Aviv*....Sh.3,128,061,048/=

Kif. 2041 – *Embassy of Tanzania - Doha*.....Sh.2,211,442,933/=
Kif. 2042 – *Embassy of Tanzania - Havana*...Sh.3,208,044,190/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 34 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

Kif. 1004 – *Policy and Planning Unit*.....Sh.4,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya
Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI: Mheshimiwa
Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge lilitrudia)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Mtoa
hoja, taarifa.

T A A R I F A

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA
AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako
lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake.
Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.
(Makof)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA
MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, kwa utaratibu wetu, nitawahoji kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa mwaka 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

(Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 – Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki yalipitishwa na Bunge)

MHE. ALLY K. MOHAMED: Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, leo Bunge limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki. Nichukue fursa hii kuwapongeza sana Waziri na Naibu wake na watendaji walioko chini yao. *(Makoff)*

Kwa kuwa Bunge limeshafanya maamuzi juu ya haya mliyokuwa mmeyaleta, tunaamini michango ya Waheshimiwa Wabunge miliyopata inaenda kuwasaidia kuboresha utendaji kazi wenu. Tunawatakia kila la kheri katika yote yaliyo mbele yenu na tunaamini kwamba yale ambayo yamesemwa na Kamati na Wabunge pia mtayafanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, ninalo tangazo hapa la wageni ambao wako jioni ya leo humu ndani. Kwanza ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni wa Mheshimiwa Joseph Haule, ambao ni wanafunzi 100 na walimu 12 kutoka Shule ya Sekondari ya St. Peter Clavery ya Mikumi, Mkoani Morogoro. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wageni ambao wako Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Kundu la kwanza ni wanafunzi 115 na walimu watatu kutoka Shule ya Msingi Fransalian ya Morogoro Mjiini

wakiongozwa na Mwalimu Mkuu wao Sister Threzer Thomas. Karibuni sana Bungeni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao pia wanafunzi 187 pamoja na viongozi wao kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana tunaamini mmeweza kujifunza mawili matatu katika yale ambayo mmeshuhudia Bunge likifanya kazi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninayo miwani hapa, kuna Mheshimiwa Mbunge aliisahau kwenye mashine zetu za ukaguzi. Miwani imeandikwa *Farschad optic*. Naamini Mheshimiwa Mbunge mwenye miwani yake atawea kuwoana Makatibu ili aipate.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge na kwa sababu humu ndani tunao vijana wetu ambaao wanakuja kujifunza shughuli hizi, niwakumbushe Kanuni ya 52 na Kanuni ya 99(13). Kanuni hizi zinazungumza kuhusu Waziri ama shughuli za Serikali zikishaanza, Spika akishaita Waziri hakuna mtu anatakiwa kuzungumza hapo. Kwa hiyo, isitafsirike kwa namna yoyote ile kwamba Waziri Kivuli naye ni Serikali, Waziri Kivuli si Serikali kwa mujibu wa Kanuni zetu. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, tuyafahamu mambo haya na ni vizuri kuendelea kujifunza kwa sababu hata sisi wengine tunaendelea kujifunza kila siku. Tusome vitabu, tusome kanuni zetu tujifunze na kwinge wanafanyaje kazi. Kwa hiyo, Serikali Bungeni iko moja tu hakuna Serikali mbili. Kwa hiyo, akisimama Waziri hapa mbele, Kiti kikishamuita hakuna tena maelezo yanayoweza kutoka hapo. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

NAIBU SPIKA: Jambo lingine ambalo pengine ni la msingi sana ni hili ambalo sisi kama Waheshimiwa Wabunge lazima tuendelee kujifunza. Usije ukafika mahali ukafikiri wewe unafahamu kila kitu na wazo lako wewe ndiyo lazima liwe. Kwa hiyo, ukiwa na wazo lako ni la kwako lakini jifunze na kwa wenzio. Usionekane wewe unasema sana kana kwamba wewe cha kwako ndicho, hapana, jifunze na kwa wenzako.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12:00 Jioni Bunge lillahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 31 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*